Alhamisi Julai 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579973

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Aliyesamehewa na Rais JPM adaiwa kujinyonga

UKURASA 2




UKURASA 13

# Baraza lawajibu Kinana, Makamba

UKURASA 2



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiangalia mita ya maji ya malipo ya kabla, iliyobuniwa na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph, Khadija Mustapha (kulia), kabla ya kufungua Maonyesho ya 14 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

## Waziri Mkuu aionya TCU kunyanyasa wanaosoma nje

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WAZEE WA BARAZA WATAKA MTUHUMIWA MAUAJI KUACHIWA

WAZEE wa Baraza katika kesi ya mauaji inayomkabili Juma Musa, wameomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam kumwachia huru mtuhumiwa huyo kwa...

UKURASA WA 5

### MAKONDA ATOA ONYO SOKO LA MADINI DAR

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amezindua soko la 28 la kimataifa la madini katika mkoa huo, huku akiwaonya wafanyabiashara kuacha...

## NEC yasema haitaongeza muda daftari wapigakura

UKURASA 2

MICHEZO JESHI LA YANGA LIMEKAMILIKA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Sababu za NEC kutoongeza muda daftari wapigakura

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema haitaongeza muda wa zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ambalo limepangwa kisheria kufanyika kwa siku saba katika kila mkoa.

Hayo yamo katika taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, alipokuwa akizungumza na wanahabari mkoani Kilimanjaro kuhusu kukamilika kwa maandalizi ya uzinduzi wa zoezi hilo.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kuzindua zoezi hilo leo katika Uwanja wa Mandela, Manispaa ya Moshi.

"Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi kwa maana ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inao wajibu wa kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura mara mbili, kati ya uchaguzi ulioisha na tarehe ya uteuzi wa uchaguzi unaofuata,"alisema Jaji Kaijage

Jaji Kaijage alifafanua kuwa kabla hawajaingia katika zoezi hili, walifanya uandikishaji wa majaribio katika kata mbili, moja ikiwa ni ya Kihonda iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Kata ya Kibuta iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

"Sasa katika siku hizi saba, tume ilijiridhisha kwamba zinatosheleza na kwa muda ambao tumepanga kuanzia saa 2:00 aubuhi hadi saa 10:00 jioni unajitosheleza. Kwa hiyo hatuna tashuwishi kwamba siku hizi saba zitatosheleza kabisa kwa maeneo yote na kama nilivyosema kwa kila kituo nchi nzima tutatumia siku saba,"alisisitiza.

Aidha, Mwenyekiti huyo wa NEC, alieleza kuwa kwa yule aliyekosa kwa bahati mbaya nafasi kwa sababu ni mgonjwa au amelazwa, ipo nafasi nyingine ya uboreshaji wa pili ambao utaanza pindi uboreshaji wa kwanza utakapokuwa umekamilika Machi mwaka 2020.

Katika uboreshaji huo, jumla ya vituo 37,407 vya kuandikisha wapigakura vitatumika kwa upande wa Tanzania Bara na vituo 407

INAENDELEA UK. 8

# Msekwa awakumbusha Makamba, Kinana kuzingatia Katiba ya CCM

**Na Salome Kitomari**

KATIBU wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu wastaafu wa CCM, Pius Msekwa, ametoa ufafanuzi wa Katiba ya chama hicho kwa baraza kushughulikia malalamiko yaliyotolewa na Makatibu Wakuu wastaafu Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba kuhusu tuhuma dhidi yao na kuomba kutolewa majibu.

Msekwa alisema ametoa majibu ya awali dhidi ya tamko la Kinana na Makamba, kwa kuwakumbusha mambo ya msingi waliyopaswa kuzingatia.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Msekwa alithibitisha kuwa barua iliyosambaa juzi kwenye mitandao ya kijamii dhidi ya tamko la Makatibu Wakuu wastaafu, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba ni ya kwake na kwamba ameamua kuisambaza kwa mitandao ya kijamii kama walivyofanya walalamikaji hao.

"Barua hiyo ni ya kwangu naliwajibu kina Kinana na Makamba, busara inasema barua yoyote lazima ijibiwe," alisema Msekwa na kuongeza:

"Busara majibu yaende kwenye mtandao ili wasome mtandaoni kama ambavyo nilisoma mtandaoni," alisema.

Pia alisema wakati suala hilo likisubiri vikao rasmi vya baraza hilo, yanatolewa majibu ya awali kwa mambo ya msingi ambayo viongozi hao (Kinana na Makamba) waliyasimamia wakati wa uongozi wao.

Vile vile, Msekwa alisema ni wajibu wa kutii Katiba na kanuni zilizopo, ambazo alielezea mamlaka ya kutenda kazi ya baraza hilo ikiwamo muda wa vikao na mipaka yake.

"Kama mnavyojua Katiba ya CCM imekipangia kila kikao chake kazi zake mahususi za kufanya. Kazi ya Baraza zimetajwa na kuainishwa katika ibara ya 127 (3) toleo la 2012 ambayo ni kutoa ushauri kwa chama na kwa serikali zinazoongozwa na chama hicho," alisema.

Alisema kazi za kuangalia mwenendo wa wanachama na viongozi wake na kuchukua hatua stahiki pale inapobidi zimepangiwa vikao vingine vya chama, ambavyo ni vya utendaji kama ilivyoainishwa kikatiba.

Vile vile, alisema maana yake ni kwamba kikatiba Baraza la Ushauri halikupewa mamlaka ya kutenda kazi za kiuendeshaji, badala yake jukumu hilo limetoa kwa vikao vingine ambavyo ni vya viongozi walioko madarakani.

Katibu huyo aliainisha jambo jingine kuwa umuhimu wa kuzingatia miiko ya utoaji ushauri ambayo ndiyo kazi yao, na kwamba ushauri kamwe hauwezi kushinikizwa kwa mshauriwa au kutolewa kama amri.

"Ndiyo kusema kwamba ushauri hauwezi kutolewa pale ambapo hauhitajiki. Na mwenye kuamua kuwapo kwa hitaji hilo, ni yule anayehitaji kupata ushauri, siyo anayetaka kutoa ushauri," alifafanua. Kwa mujibu wa Msekwa, hata pale ushauri unapotolewa unaweza kukubaliwa au kukataliwa na kwamba unapokubaliwa thamani yake inakuwa ni kubwa, kwa maana ya kuondoa tatizo lililokuwapo.

"Lakini pale ushauri unapokataliwa, thamani yake inakuwa ni sifuri kabisa, kwa maana ya kutatua tatizo lililopo," alisema.

Msekwa alisema jambo jingine ni kwamba jukumu la mtu yeyote aliyetuhumiwa la kusafisha jina lake, ni la mtuhumiwa mwenyewe.

Pia alisema: "Mlitafakari suala la kujitokeza hadharani ili kutoa yaliyo moyoni mwenu katika kujibu uwongo wake (mwanaharakati), kusafisha majina yenu, heshima yenu, na rekodi nzuri ya utumishi wenu, lakini mkaona kuwa ni vyema kwanza mkawasilisha malalamiko yenu kwenye baraza, ili jambo

INAENDELEA UK. 8



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akionyeshwa aina tofauti za madini na matumizi yake na msemaji wa wafanyabiashara wa mkoa huo, Osman Tharia, baada ya kuzindua Soko la Kimataifa la Madini jijini humo, jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Aliyepata msamaha wa Rais ajinyonga hadi kufa

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WATU wawili wa Kata ya Myula wilayani Nkasi, mkoani Rukwa wamejinyonga hadi kufa katika matukio mawili tofauti, huku mmoja akiwa amepata msamaha wa Rais baada ya kufungwa jela kwa kosa la kumuua mdogo wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chonga, Makupa Peter, watu hao wanadaiwa kujinyonga bila kuacha ujumbe wowote.

Aliwataja watu hao kuwa ni Cyprian Kasamya (33) na Albert Kayanza, wote wakazi wa Kijiji cha Chonga. Ofisa Mtendaji alisema, Kasamya alijinyonga kwa kutumia kamba ya katani chumbani kwake majira ya saa ya 11 jioni, wakati Kayanza alijinyonga shambani kwa kutumia kamba ya miti na aligundulika majira ya saa mbili usiku. Alisema Kasamya aliwahi kutumikia kifungo jela kutokana na kosa la mauaji ya mdogo wake na alipata msamaha wa Rais.

Hata hivyo, kwa upande wa Kayanza haikujulikana sababu ya kujinyonga kwake.

Katibu Tawala wa Wilaya Nkasi, Cosmas Kuyela, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo mawili, lakini hakupata undani wa sababu zilizowafanya watu hao kujinyonga.

Aliitaka jamii kuacha kujichukulia sheria mikononi na kuamua kujiua kutokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili bali watumie njia nyingine ambazo ni sahihi katika kutatua changamoto zinazowakabili.

## HABARI KITAIFA

# Waziri Mkuu aionya TCU kunyanyasa wanaosoma nje

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), kukaa na taasisi zinazojishughulisha kupeleka Watanzania nje ya nchi kusoma masomo ya elimu ya juu na kufanyia kazi malalamiko yao.

Amesema kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wanafunzi hao kuwa wanaporudi nchini, tume kutovitambua vyuo walivyosoma.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua Maonyesho ya 14 ya Vyuo Vikuu yaliyoandaliwa na TCU na kuvishirikisha vyuo mbalimbali.

"Bado tuna tatizo, Mkurugenzi wa TCU, nilikudokeza kwamba wiki mbili zilizopita nilikuwa Misri nilipata fursa ya kuongea na Watanzania miongoni mwao ni wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma nchini humo," alisema na kuongeza:

"Miongoni mwa malalamiko ni chuo kikuu (anakitaja) inaonekana Watanzania wanaosoma hapo wakimaliza na kupata vyeti vyao havitambuliki na TCU, kuna idadi kubwa ya Watanzania wanasoma hapo.

"Upo umuhimu wa kuona kwa nini cheti hicho hakitambuliki na kama havitambuliki kwa nini wanawapeleka Watanzania pale? Na cha ajabu zaidi ni kwamba miongoni mwao ni wale ambao serikali imewadhamini kwenda kusoma hapo," alisema.

Majaliwa alisema ni muhimu TCU iangalie na kutatua changamoto hiyo ili serikali isije ikapoteza fedha hivyo wawaelekeze Watanzania waende kusoma vyuo ambavyo vinatambulika.

"Ninaielekeza TCU, tunatambua zipo taasisi binafsi zinazoshiriki katika kuwaelekeza na kuwatafutia nafasi Watanzania kwenda kusoma vyuo vya nje, ni muhimu mkazitambua taasisi hizi, tujue nani anafanya kazi kuwasaidia kupata vyuo nje, ni vyema na wao wapewe jukumu la kuanza kuhakiki ubora wa elimu waliyonayo kabla ya kuwaruhusu kuingia chuo kikuu, badala ya kuendelea kuorodhesha orodha na kuwapeleka nje kusoma shahada wakirudi hawatambuliwi kwa sababu hawana sifa," alisema.

Majaliwa aliitaka TCU ikae na taasisi hizo, izisajili na kuzitambua kuwaambia mahitaji ya kwenda chuo kikuu ni yapi ili nao washiriki kuwashauri vijana sifa zinazotakiwa.

"Tume itafute mbinu bora zaidi ikiwa ni pamoja na kuvijengea uwezo vyuo vikuu binafsi ili

INAENDELEA UK. 26

# Wazee wa baraza wataka mtuhumiwa mauaji kuachiwa

**Na Hellen Mwango**

WAZEE wa Baraza katika kesi ya mauaji inayomkabili Juma Musa, wameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam kumwachia huru mtuhumiwa huyo kwa kuwa ushahidi wa Jamhuri haujajitosheleza kumtia hatiani.

Wakiwasilisha hoja zao za majumuisho ya mwisho kwa nyakati tofauti, wazee hao wameiomba mahakama imwone mtuhumiwa hana hatia kwamba hakuna shahidi aliyemwona akifanya mauaji hayo.

Hoja hizo za wazee zilitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo, anayesikiliza kesi ya mauaji ya kukusudia ya Fatuma Mbaga dhidi ya mume wake, Musa.

Mzee wa kwanza alidai kuwa katika ushahidi wa Jamhuri uliotolewa na mashahidi wa Jamhuri, una shaka kwa sababu hakuna shahidi aliyeshuhudia mshtakiwa akifanya mauaji hayo.

Akifafanua zaidi alidai ushahidi wa Jamhuri unaeleza mshtakiwa alionekana siku ya tukio akiwa amebeba begi na kutoweka nyumbani kwake.

Hata hivyo, katika utetezi wake alidai kuwa alisafiri kwenda mkoani Mwanza kumuuguza baba yake mzazi, na baadaye alifariki.

Mshtakiwa alidai kabla ya kusafiri kwenda Mwanza, alimwacha mke wake akiwa mzima na kwamba siku ya pili yake Mei 12, 2015 alipigiwa simu na mwenyekiti wa serikali ya mtaa akimjulisha kwamba mke wake amefariki kwa kupigwa shoti ya umeme.

Pamoja na mambo mengine, uchunguzi wa Jamhuri ulibaini kwamba baba mzazi wa mshtakiwa yupo hai na ni mwajiriwa wa Kiwanda cha Nguo Mwanza (Mwatex).

Alidai mashahidi wote wa Jamhuri waliiambia mahakama kwamba waliukuta mwili wa Fatuma ukiwa kitandani na pasi ya umeme ikiwa pembeni yake.

Mzee wa pili, alidai kuwa ushahidi wa Jamhuri una shaka kwa sababu hakuna shahidi aliyemshuhudia mshtakiwa akimuua Fatuma.

Pia alidai kuwa ushahidi wa mshtakiwa umedai kuwa alipata taarifa kwamba mke wake alikufa kutokana na shoti ya umeme, lakini mwili ulikutwa na majeraha sehemu za siri na uti mgongo umevunjika, mambo ambayo hayahusiani na umeme.

Alidai Jamhuri imeshindwa kuthibitisha kama kweli baba mzazi wa mshtakiwa ni mwajiriwa wa Mwatex na pia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) walikwenda eneo la tukio kuthibitisha kama kulikuwa na shoti ya umeme siku ya tukio au la.

Mzee wa tatu, alidai ushahidi wa Jamhuri umeshindwa kuieleza mahakama kwamba nani alifanya mauaji hayo na kama ni mtuhumiwa nani alimwona.

Wazee hao kwa nyakati tofauti waliiomba mahakama imwachie huru mshtakiwa kwa sababu hakuna ushahidi wa kuthibitisha kosa hilo dhidi yake.

Msajili Mazengo alisema baada ya kusikiliza hoja za majumuisho ya wazee wa baraza na pande zote mbili, mahakama yake itapanga tarehe ya kusoma hukumu na itawajulisha.

Katika kesi ya msingi, Musa anadaiwa kuwa Mei 11, 2015 eneo la Mchikichini, jijini Dar es Salaam, alimuua kwa makusudi mke wake Fatuma Mbaga.

# Ubalozi Marekani yapongeza tuzo Jamii Forum

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani nchini umempongeza mmiliki wa mtandao wa Jamii Forum, Maxence Melo, kwa kutangazwa mmoja wa washindi wa Tuzo ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kwa mwaka 2019. Tuzo inayotolewa na Kamati ya Ulinzi kwa waandishi wa habari.

Taarifa iliyotolewa na ubalozi huo jana kwa vyombo vya habari ilisema pamoja na kukabiliwa na changamoto nyingi za kisheria, Melo na Jamii Forums, wameendelea kuwa mstari wa mbele katika kutetea uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania. Taarifa hiyo ilisema Tanzania inajivunia historia kubwa iliyosheheni mchango mkubwa wa vyombo vya habari, kuanzia mchango wa Radio Tanzania Dar es Salaam katika ukombozi wa Afrika, kuimarisha umoja wa Afrika na kukuza amani na haki.

"Kutambuliwa kwa Maxence Melo na kutunukiwa kwake tuzo hii kunatukumbusha urithi huu muhimu wa historia ya nchi hii; urithi ambao unatishiwa pale ambapo matukio ya ukiukwaji wa haki, unyanyasaji na hata watu kupotea zinapogubika utamaduni wa maendeleo ya kijamii yanayosukumwa na vyombo vya habari," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:

"Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania unatoa wito kwa Serikali ya Tanzania kulinda urithi huu wa kihistoria kwa kuimarisha usalama wa waandishi wa habari na kutokomeza hali ya wale wanaowadhuru kutokuchukuliwa hatua zinazostahili."


SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




TAIFA STARS vs KENYA
JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

## HABARI KITAIFA

# UDOM yawafunda waombaji vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimewataka wanaoomba kuingia vyuo vikuu kuhakikisha wanajaza fomu za kuomba program za masomo kwa kuzingatia sifa walizonazo kwa usahihi ili kuepusha malalamiko hapo baadaye kuwa hawakuchaguliwa wakati wana vigezo. Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Faustine Bee, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) katika viwanja vya Mnazi Mmoja.

Prof. Bee alisema aliwataka wanafunzi wa kidato cha sita ambao wanatarajia kuingia vyuo vikuu, wasome kwa umakini sifa zinazotakiwa kwenye chuo ndipo wajaze. "Ukikosea kuomba programu ambayo haiendani na sifa ulizonazo mwanafunzi husika, utajikuta ameachwa na ukiachwa baadaye unalalamika.Tunasisitiza hili sana, wanafunzi wasome vizuri na wazingatie maelekezo ya vyuo wakati anaomba programu," alisema.

Alisema katika maonyesho hayo, mbali ya kuonyesha programu zinazotolewa chuoni hapo, wanafanya udahili wa moja kwa moja.

"Kwa hiyo mwanafunzi anayekuja kwenye maonyesho atambue kuwa haji tu kwenye maonyesho, atapata fursa ya kudahiliwa moja kwa moja," alisema.

Pia alisema wahadhiri na wanafunzi wa UDOM hushiriki katika kutoa huduma za jamii ambapo kupitia shule tanzu ya tiba UDOM kwa kushirikiana na hospitali ya Benjamin Mkapa walifanya upandikizaji figo kwa mara ya kwanza Tanzania.

"Tunaendelea kuimarisha nguvu na maarifa katika eneo hilo. Pia upo ushiriki wa wanafunzi wetu katika huduma nyingine za kijamii," alisema na kuongeza: "Lengo ni kuwajengea uwezo siyo wa maarifa darasani, pia uzoefu wa kutenda kwa vitendo ili wakimaliza wajiajiri, mfano ni mradi wa ufugaji nyuki."




Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na kibao cha Mtaa wa Jamhuri, kilichokosewa na kuandikwa 'Jamuhri' ambacho kinahitaji marekebisho, katika makutano ya mtaa huo na Azikiwe, eneo la Posta Mpya, jijini humo jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Jamhuri yaomba kesi uhujumu uchumi kuahirishwa siku 14

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kutakatisha fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms, akiwamo wakili mwandamizi wa kujitegemea, Dk. Ringo Tenga na wenzake, umeiomba mahakama kuahirisha kesi ndani ya siku 14 kwa kuwa wanaandaa nyaraka muhimu.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Julai 26, mwaka huu.

Aprili 5, mwaka huu upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

"Mheshimiwa hakimu kesi hii imepangwa kwa ajili ya kutajwa na Jamhuri tunaifahamisha mahakama kwamba upelelezi wake umekamilika tunaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza mchakato wa kusikilizwa," ulidai upande wa Jamhuri.

Mbali na Dk. Tenga, washtakiwa wengine ni Mhandisi na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Hafidhi Shamte maarufu Rashidi Shamte, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa fedha wa kampuni hiyo Noel Chacha na kampuni ya Six Telecoms Limited wanadaiwa kutakatisha Sh. Bilioni nane.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, hivyo kuwafanya wasote mahabusu kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.


Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

## EMPLOYMENT OPPORTUNITIES

**The Tanzania Forest Conservation Group (TFCG)** is a national NGO whose mission is to conserve and restore the biodiversity of globally important forests in Tanzania for the benefit of the present and future generations. TFCG, in partnership with the Community Forestry Network of Tanzania (MJUMITA) and TATEDO is implementing Phase 2 of the 'Transforming Tanzania's Charcoal Sector Project'. The project is financed by the Swiss Agency for Development and Cooperation. As part of this project, TFCG and MJUMITA are seeking applications from qualified Tanzanian women and men for the following positions:

**Finance Officer, Dar es Salaam**

**Qualification and experience**
- A CPA is a requirement
- At least 5 yrs experience of working on financial management in the context of donor-funded projects.

**Responsibilities**
- Contributing to the effective and efficient management of the TTCS project's finances; preparation of financial reports; and ensuring compliance with donor requirements.

**How you can apply**
Job descriptions are available at http://www.tfcg.org/careers.html. Qualified candidates should send applications including a detailed CV, covering letter, contact details (including an e-mail address and phone number) and contacts of three professional referees to: personnel@tfcg.or.tz.

**The deadline for applications is 10 a.m. 31st July 2019.**

Short-listed candidates will be informed of the interview date by **12th August, 2019.**

Applicants who have not received communication by this date should consider their application unsuccessful.

215328102


# Wanahabari wapewa somo kuhusu SADC

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk Hassan Abas, amesema vyombo vya habari vina wajibu wa kuonesha changamoto zinazoikabili Serikali au zinazoweza kuikwanza katika kutimiza ajenda zake kwa faida ya wananchi.

Alisema vyombo hivyo vinawajibika kueleza ukweli, kutumia utafiti na kutumia lugha ya kiungwana pale penye mapungufu.

Dk. Abas alisema hayo mjini Morogoro wakati akifunga mafunzo maalum kuhusu Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa waandishi wa habari, yaliyofadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ).

Mafunzo hayo maalumu ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu masuala ya SADC yalifanyika mjini Morogoro kwa awamu mbili na kushirikisha jumla ya waandishi wa habari 60 wa kutoka vyombo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi.

Dk. Abas alisema mafunzo hayo yamelenga kuwapa elimu na uelewa mpana waandishi wa habari ambao ni wawakilishi na mabalozi wa jamii ya Watanzania zaidi ya milioni 55, wanaosubiri kwa hamu kujua mengi kuhusu SADC wakati Tanzania ikielekea kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali 16 za SADC utakaofanyika nchini mwezi ujao.

Alitaja wajibu mwingine kwa vyombo vya habari ni kwenda mbali kabisa na kauli za kila siku za viongozi, wanasiasa na wanaharakati kwa kuwapa jukwaa wananchi wa kawaida na wadau wengine kupaza sauti zao.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Makonda atoa onyo kwa w'biashara utoroshaji madini

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amezindua soko la 28 la kimataifa la madini katika mkoa huo, huku akiwaonya wafanyabiashara kuacha vitendo vya utoroshaji madini.

Makonda alizundua soko hilo lililopo katika Jengo na National Haousing Posta jijini Dar es Salaam jana, kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kutaka kila mkoa kuwa na soko la madini nchini.

Alisema hataki kuona mkoa huo kuwa chanzo cha matukio ya wizi wa madini ambayo ni mali ya Watanzania, ikapotea bure bila kunufaika nayo.

"Sitaki kuona mkoa wa Dar es Salaam ukiwa na wafanyabiashara wa kutorosha madini, mkoa huu utakuwa sehemu ya kuuza biashara hii muhimu kwa uchumi wa taifa letu," alisema Makonda.

Makonda alisema uwapo wa soko hilo, utasaidia wananchi kununua madini na vito halali na kupunguza matapeli waliokuwa wakiuzia wananchi na wageni madini na vito feki.

Aidha, alisema uzinduzi wa soko hilo umekuja wakati muafaka ambao Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za SADC, ambao wageni wataingia nchini mwezi ujao wakiambatana na wafanyabiashara.

Makonda pia aliwataka wananchi kulitumia soko la madini kwa sababu linatambuliwa na Serikali na madini ya aina zote yanapatikana.

Mbali na hilo pia alipiga marufuku wasafirishaji wa magari ya IT kukamatwa pindi wanaponunua bidhaa zao kwenda nazo nchi jirani au mkoani kwa madai wanafifisha biashara katika mkoa huo.

Alisema askari wa usalama barabarani wamekuwa wakiwazuia wasafirishaji wa magari hayo kubeba bidhaa kwenye magari hayo na kuvitaka vyombo vyenye mamlaka kuangalia suala hilo linalokwamisha biashara katika mkoa huo.

Naye Mtalaamu kutoka Wizara ya Madini, Ally Maganga, alisema masoko 28 yameshafunguliwa hadi sasa na kuwataka wafanyabiashara kufuata sheria.

Alisema asilimia 45 ya wafanyabiashara wa madini wanapatikana katika mkoa wa Dar es Salaam hivyo kuzinduliwa kwa soko hilo kutaboresha biashara hiyo.

Alisema changamoto kubwa inayoikabili sekta ya madini ni utapeli na utoroshwaji wa madini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Godfrey Simbeye, alipongeza kufunguliwa kwa soko hilo kwa sababu wafanyabiashara wengi wanapatikana katika Jiji la Dar es Salaam.

# MISA-Tan yalaani waandishi kudhalilishwa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-Tan), imesema imepokea kwa masikitiko kitendo kilichofanywa na msanii Irene Uwoya, cha kuwarushia waandishi wa habari fedha na kueleza kuwa kimejaa udhalilishaji wa taaluma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na bodi ya uongozi wa MISA-Tan kwa vyombo vya habari, kitendo hicho kimejaa kuidhalilisha taaluma ya habari inayotambulika kwa mujibu wa sheria ya huduma za habari ya mwaka 2016 na Katiba ya nchi.

"Jana (juzi) ilisambaa video ikimwonyesha Irene Uwoya, akiwarushia fedha waandishi wa habari waliohudhuria mkutano wake akizungumzia uzinduzi wa urushaji wa filamu kampuni ya Swahili Inflix," ilisema.

Katika mkutano huo, Uwoya aliwataka waandishi wa habari kuvaa suti siku ya hafla hiyo na siyo wanavyovaa siku zote.

Alisema baada ya maelezo yake,

INAENDELEA UK. 8

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## TAARIFA KWA UMMA

**17 Julai, 2019**


## UWEPO KWENYE SOKO WA TOLEO MOJA LA DAWA BANDIA YENYE JINA GENTRISONE CREAM 10G

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali ulio chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umeundwa tarehe 1 Julai 2019 baada ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 iliyohamisha majukumu ya udhibiti wa chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na kuyapeleka Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

2. TMDA sasa inadhibiti ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

3. TMDA inapenda kuutangazia umma kwamba imebaini uwepo katika soko wa dawa bandia yenye jina **Gentrisone 10g** cream inayoonesha kwenye lebo yake kwamba inatengenezwa na kiwanda chenye jina Shin Poong Pharm Co. Ltd kilichopo Jamhuri ya Korea na kusambazwa hapa nchini na kampuni yenye jina K&C Trading Co. Ltd ya Dar es Salaam.

4. Dawa bandia iliyoko kwenye soko inaonesha kwenye lebo namba ya toleo **(GNTRO X030)** iliyotengenezwa tarehe **21. 04. 2019** na kuisha muda wa matumizi tarehe **20. 04. 2022** na namba ya usajili **TAN00. 368 D07C SHI** kama ilivyoainishwa hapa chini.




5. Dawa hii bandia imefanana kwa kiasi kikubwa na dawa halisi ambapo utofauti wake ni kwenye namba ya toleo na mtengenezaji amethibitisha hajawahi kutengeneza toleo namba **GNTRO X030** lililoko kwenye soko la Tanzania.

6. Uchunguzi uliofanyika kwenye Maabara ya TMDA umethibitisha kuwa dawa hii bandia haina viambato hai vyenye majina ya kitaalam *Betamethasone diproprionate 0.64mg, Clotrimazole 10mg na Gentamycin Sulfate 1mg* ambavyo kikawaida viko kwenye dawa halisi iliyosajiliwa na TMDA na vile vile haina harufu ya dawa.

7. Kufuatia kubainika kwa dawa hii bandia, TMDA imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuondoa kwenye soko jumla ya tubes **4,188** kutoka mikoa ya Mwanza (tubes 1,814) Dar es Salaam (tubes 931), Dodoma (tubes 591), Tabora (tubes 29), Arusha (tubes 6) na Mtwara (tubes 817).

8. Kwa kuwa zoezi la ukaguzi wa dawa husika lilifanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, watuhumiwa mbalimbali wamekamatwa ikiwa ni pamoja na Mwendesha pikipiki mmoja aliyehusika katika kusambaza dawa hii kwenye maduka binafsi ya reja reja ya dawa ambaye anaisaidia Polisi kufahamu mtandao mzima.

9. Kutokana na kuwepo kwa dawa tajwa na kwa mujibu wa taratibu, mtengenezaji na msambazaji wameelekezwa kushirikiana na TMDA katika kuondoa matoleo yote kwenye soko ambayo ni bandia ili wananchi wasiendelee kununua.

10. Kwa taarifa hii wananchi wote ambao wamenunua dawa hii kutoka kwenye maduka ya dawa wanashauriwa kuangalia kwenye lebo na ikiwa wataona namba ya toleo (yaani **GNTRO X030**) kwenye box la dawa husika warudishe waliponunua.

11. Wauzaji wa jumla wote ambao wana dawa husika kwenye stoo au maghala yao wanaelekezwa kama wanazo dawa hizi kwa toleo lililoainishwa kuacha kuzisambaza na wawasiliane na TMDA ili kupewa utaratibu wa wapi pa kuzipeleka.

12. Ifahamike kwamba ni toleo moja tu la dawa hii (yaani **GNTRO X030)** ndilo limethibitika kuwa ni bandia na sio matoleo mengine ambayo bado yako kwenye soko na hivyo wagonjwa wanaosumbuliwa na magonjwa ya ngozi kama vile kuwashwa, upele, kuungua na moto, kuvimba ngozi, fungus za miguuni na maeneo mengine ya mwili wanashauriwa kuendelea kutumia dawa hii kwa kuwa imesajiliwa na kuthibitika inatibu magonjwa haya.

13. TMDA inaendelea kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotengenezwa au kuingizwa nchini ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara kwenye mipaka na kwenye soko ili kubaini bidhaa bandia na duni na kuchukua hatua stahiki kwa lengo la kulinda afya ya jamii.

14. TMDA inaendelea kuwaomba wananchi wote kuendelea kutoa taarifa ikiwa watabaini kampuni, kikundi, mitandao au mtu yeyote anayejihusisha na utengenezaji, usambazaji au uuzaji wa dawa bandia ili hatua ziweze kuchukuliwa kumkamata haraka na kumfikisha kwenye vyombo vya sheria.

**Imetolewa na:**

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA),**
**Mtaa wa Mwanza, Kitalu T, Kiwanja Na.6**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Nukushi: +255 22 2450793**
**Simu bila Malipo: 0800110084**

*215327901*

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Polisi wazingatie weledi mikutano ya ndani kisiasa

**KWA** muda mrefu vyama vya siasa nchini vimekuwa vikilalamikia mikutano yao ya ndani kuzuiwa na Jeshi la Polisi.

Viongozi wa vyama hivyo wamekuwa wakisema kuwa Jeshi la Polisi linazuia mikutano hiyo licha ya marufuku ya serikali ya kuzuia mikutano ya kisiasa kuhusu mikutano ya ndani.

Kutokana na hali hiyo, wadau mbalimbali wamekuwa wakieleza kutokuridhishwa na matukio ya mikutano ya ndani ya vyama vya upinzani kuzuiwa na Jeshi hilo na wakati mwingine kuisambaratisha na kuwakamata baadhi ya wahusika.

Mambo mengine ambayo yamekuwa yakihojiwa na kulalamikiwa ni chama tawala kufanya mikutano ya hadhara na ya ndani pamoja na baadhi ya viongozi wake kwenda kufanya mikutano nje ya maeneo yao kama katazo la mikutano ya kisiasa linavyoeleza bila kuchukuliwa hatua zozote.

Pengine baada ya kusikia malalamiko hayo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, ametoa ufafanuzi suala la mikutano ya kisiasa kwa kusema kuwa mikutano ya ndani haijapigwa marufuku kama inavyozungumzwa.

IGP Sirro alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na askari kwenye ziara yake ya kikazi mkoani Tabora, na kueleza kuwa mikutano hiyo inaweza kusitishwa tu pale itakapoonekana kwamba kuna viashiria vya uvunjifu wa amani.

Alisema kwamba licha ya mikutano hiyo kutopigwa marufuku, ila kama kuna taarifa za tishio la usalama kwenye mikutano huo pokisi wanaweza kuzuia kwa faida ya Watanzania.

IGP Sirro alisema mikutano hiyo inaruhusiwa kunapokuwa na mazingira ya amani na kwamba wahusika wanachotakiwa kuzingatia ni kufuata sheria na taratibu zilizowekwa kila wakati.

Aliongeza kuwa Jeshi hilo linapokuwa limezuia mikutano ya ndani, watu wazingatie sheria na watii kwa sababu askari wanakuwa na taarifa zinazoweza kusababisha vurugu, hivyo sasa tunawataka wahusika watii amri za polisi.

Alisema imekuwa kawaida kwa baadhi ya wanachama wa vyama vya upinzani kupiga kelele na kupinga hatua ya askari kuzuia mikutano ya ndani hali inayosababisha amani kutoweka kwenye eneo husika. Hatupingi katazo la serikali la mikutano ya vyama vya siasa, lakini tunaona ni vizuri usimamizi wa katazo hilo ufanywa na Jeshi la Polisi kwa kuzingatia haki na usawa kwa vyama vyote.

Kadhalika, hatuungi mkono mikutano ya aina yoyote hata kama ni ya ndani kuwa na malengo ya kuvunja amani, hivyo tunavishauri vyama vya siasa kuheshimu na kufuata sheria za nchi. Sirro amefanya jambo zuri kwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusiana na suala hilo ambalo kimsingi, limekuwa likizua mijadala na malalamiko miongoni mwa makundi ya jamii hususan vyama vya siasa.

Ni matarajio yetu kuwa Jeshi la Polisi litakuwa makini katika kusimamia mikutano ya vyama vya siasa iwe ya hadhara ambayo katazo hilo haivihusu hususan ile inayofanywa na viongozi wa kuchaguliwa katika maeneo yao kama wabunge na madiwani pamoja na ya ndani.

Utakumbukwa kuwa taifa letu linaelekea katika uchaguzi; wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, hivyo ni wakati ambao Jeshi la polisi litapaswa kudhihirisha kuwa linatenda haki kwa makundi yote ya jamii pamoja na kutekeleza majukumu yake ya kusimamia haki kwa usawa, ufanisi na weledi.

Kwa kufanya hivyo, malalamiko yasiyo na msingi yatapungua, litaaminika kwa Watanzania wengi pamoja na jumuiya ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Kampeni hizi ziwe chachu kukomesha mimba

**MKOA** wa Lindi kwa sasa uko kwenye kampeni maalum iliyopewa jina la 'msaidie akue, asome, mimba baadaye', ikiwa na lengo la kukomesha mimba za utotoni na kuwalinda mabinti.

Kampeni hizo zinafanyika kutokana na tatizo la mimba kwa watoto wa kike kuwa kubwa mkoani humo, ambapo uzinduzi wa kampeni huyo ulifanyika Februari mwaka huu kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Mpilipili, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Rehema Madenge, akitoa taarifa kuhusu kampeni hiyo, anasema inalenga kuimarisha mifumo ya ulinzi kwa watoto kuanzia ngazi ya kaya hadi mkoa kwa kuwajengea uwezo wataalamu wanaoshughulikia masuala ya ulinzi na usalama wa watoto.

Anafafanua zaidi kuwa huduma kwa waathirika wa mimba za utotoni ni muhimu na endelevu ili kwamba mwenye mimba awe na afya bora na hata mtoto atakayezaliwa ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa mashauri ya watoto na kuwapatia msaada wa kisaikolojia wale waliopata mimba.

Lengo lingine la kampeni ni kusimamia na kuchukua hatua za makusudi kuzuia mimba za utotoni kwa kutoa elimu na kuwajengea uwezo watoto, wazazi, walezi na wadau juu ya madhara ya mimba za utotoni kwa kuhusisha vyombo vya habari na kutumia elimu ya sanaa," anasema Madenge.

Anaongeza kuwa katika mkoa wa Lindi ongezeko la mimba za utotoni lina uhusiano mkubwa na malezi duni ya wazazi au walezi, ambapo wazazi wengi wa maeneo hayo hawako makini kufuatilia malezi na makuzi ya watoto wao.

Mtindo huo wa wazazi inaelezwa kwamba uwafanya watoto hao kuwa huru, kufanya wanachokitaka, kucheza katika mazingira hatarishi, ambako wanakuwa wanajifunza mambo mengi yasiyostahili kwa umri wao.

Nikirejea kwa kile ambacho ninataka kukijadili, ni kwamba kwa muda mrefu baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakilaumiwa kwa kutofuatilia nyendo za watoto wa kike au kumalizana na wale wanaowapa mimba.

Mtindo huu unachangia kukwamisha juhudi za serikali za kupambana na mimba za utotoni, ambazo ni kikwazo kwa watoto wa kike kutimiza ndoto zao na ni hatari kwa afya zao pia.

Wataalamu wa afya wanasema, mimba za utotoni huathiri afya kwa vile wanaopewa mimba ni wale ambao maungo yao bado hayajawa na uwezo wa kuwafanya wajifungue.

Pamoja na maelezo hayo ya wataalamu wa afya, mimba zinasababisha wakose elimu, ambayo ni moja ya haki ya msingi, na pia mabinti wasio na elimu watakuwa na ugumu kupata ajira na kujijengea maisha bora na familia zao.

Licha ya kuwapo kwa kampeni mbalimbali zenye lengo la kumaliza tatizo hilo, bado mimba zimeendelea kuibuka kana kwamba ni jambo la kawaida kwenye baadhi ya jamii.

Nikumbushe kwamba Januari mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa wanafunzi 140 wa shule za msingi na sekondari walikatisha masomo mwaka jana.

Kwamba 54 walikuwa wa shule za msingi na 86 wa sekondari, huku wale wa kidato cha kwanza na cha pili wakiongoza kupata mimba, wakati msingi wakiwa ni wa darasa la sita.

Siyo hapo tu, hivi karibuni mkuu huyo wa mkoa alikaririwa tena na vyombo vya habari akisema kuwa Januari hadi Juni mwaka huu, wanafunzi 60 wa shule za msingi na sekondari wamepata mimba.

Anaweka wazi kuwa mazingira ya mimba yanaashiria kuwa kuna muungano kati ya watendaji na wazazi, kwa madai kwamba wanaowapa mimba wanafunzi hawakamatwi.

Kampeni hizo ziwe chachu kukomesha mimba na ikiwezekana hatua kali zichukuliwe kwa wahusika kuanzia kwa wazazi, watoto na wale wanaowapa mimba ili liwe fundisho kwa pande zote.

Tatizo la wahusika kutochukuliwa hatua kali za kisheria lisiachwe liendelee na pia mtindo wa kumaliza mambo kimyakimya usipewe nafasi ili kusaidia binti kuepuka mimba hizo.

## *Foleni zilivyotutibulia Sabasaba*

***Mhariri,***

*WIKI ya kwanza ya mwezi Julai watu kadhaa hukusanyika jijini Dar es Salaam kwenye maonyesho ya biashara ya kimataifa yanayofanyika Barabara ya Kilwa.*

*Niseme kuwa kwenda kwenye maonyesho haya ulikuwa mzigo. Foleni zinatisha na kuwakatisha watu tamaa. Mathalani, kutoka Tegeta hadi Viwanja vya SabaSaba inamchukua mtu saa 10 kusafiri. Hii ni safari ya saa tano kwenda na tano kurudi.*

*Nikitoa mfano wangu nilitoka Tegeta saa 1 asubuhi Jumamosi iliyopita kwenda SabaSaba. Nilifika viwanjani saa 5 asubuhi nilizunguka kwenye mabanda kwa saa nne na kuondoka Saba Saba saa 9:00 alasiri nilifika nyumbani saa 3 usiku.*

*Tatizo ni foleni. Nikafikiria kuwa pengine maonyesho yangeruhusiwa kufanyika kwa muda wa saa 24 kwa kuwa foleni inaharibu uzuri wa maonyesho hayo na kukwamisha wengi kushiriki.*

***Abudul Azani***
***Tegeta kwa Ndevu***

## *Mbona TANESCO inatuweka hatarini*

***Mhariri,***

*NASHUKURU kwa fursa hii , naomba nitoe ya moyoni kuhusu TANESCO , inavyotufanyia wananchi wengi. Haturidhiki na mchezo wa kupitisha nyaya za umeme mkubwa juu ya mapaa yetu.*

*Ninatoa angalizo kwa kuwa mimi ni mmoja wa wakazi wa maeneo yasiyokuwa na umeme yaliyokaribu na Shule ya Sekondari Mbopo iliyopo wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam.*

*Nashangaa TANESCO kupitisha nyaya za umeme mkubwa unaohitaji kupozwa au kuchochewa mita tatu karibu na paa la nyumba nyingi za wananchi wanaokaa maeneo hayo.*

*Naomba serikali iingilie kati kuepusha majanga.*

***Marina Mosha***
***Mbopo -Dar es Salaam.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Hizi ndizo changamoto za vifungashio vipya



**Na Sabato Kasika**

SASA ni zaidi ya mwezi mmoja tangu serikali ipige marufuku biashara na matumizi ya mifuko ya plastiki, kwa lengo la kutunza mazingira na pia kuepusha watu na athari za kiafya zinazotokana na kufungashia vyakula kwenye mifuko hiyo.

Kabla ya katazo mifuko hiyo ilikuwa inawekea vyakula kama chips, supu, chapati , wala na maharage na vitafunwa vingine vya moto.

Pamoja na katazo hilo kumekuwapo na changamoto mbalimbali zinazotokana na mazoea ya baadhi ya watu, ambayo wakati mwingine yanawafanya wakwame kununua na kuuza bidhaa.

Kuna msemo kwamba "mazoea yana tabu". Hivyo ndivyo inaweza kuwa kwa baadhi ya watu ambao walikuwa wamezoea kununua vitu na kupewa mifuko bure ili kuwekea bidhaa zao lakini sasa utaratibu huo haupo tena.

Utaratibu wa kuuza vifungashio na bidhaa umekuwa ukisababisha baadhi yao kuhangaika huku na kule na kujikuta wakikwama, hasa wale wanaotoka kwenye mihangaika ya kila siku wakiwa njiani kurudi nyumbani.

Kwa hali hiyo ni wazi kwamba kila jambo lazima liwe na athari chanya au hasi, hivyo ni muhimu kufika wakati watu waachane na mazoea ya zamani ya kudhani bado wanaweza kupata mifuko bure.

Wapo wale ambao wamekuwa wakiomba wapewe bure vifungashio hivyo vinavyouzwa kati ya Sh. 300 hadi 1,000, lakini wanajikuta wakikwama na hivyo kulazimika kuvunuunua au kuacha.

Hata hivyo, vifungashio hivyo vipya siyo kubwa vya kuchukua bidhaa nyingi kama ilivyokuwa kwenye mifuko ya plastiki, hali ambayo inawafanya baadhi ya watu kuviona kama havifai na hivyo kuamua kubeba vikapu vyao.

Lakini pamoja na hayo, bado ipo haja ya kuzoea mazingira ya sasa kwamba serikali imepiga marufuku mifuko ya plastiki kwa lengo la kulinda mazingira na kuagiza kuwapo kwa vifungashio vipya.

Hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuzingatia hilo na kutumia vifungashio vipya ambavyo vinapatikana kwa wafanyabiashara wadogo wakiwamo wauza mboga na matunda na hata kwenye maduka.

Vilevile watengenezaji wa vifungashio hawana budi kutengeneza vikubwa ambavyo mteja anatumia kuweka bidhaa nyingi anapokwenda sokoni au dukani, kuliko kuwa na vidogo ambavyo ni kama wateja hawavitaki.

Wateja wanaona usumbufu kununua kifungashio cha kati ya Sh. 500 au 1,000 huku kikiwa hakina uwezo wa kuchukua vitu vingi kwa mara moja.

Kwa mfano mtu anaweza kwenda sokoni akanunua, viazi, matunda mbalimbali, mboga na vitu vingine, lakini hawezi kuweka katika kifungashio kimoja, kwa sababu siyo kikubwa.

Kabla ya marufuku, kulikuwa na mifuko ya plastiki ambayo watu walikuwa wakiitumia kubebea vitu vingi kwa wakati mmoja na tena walipewa bure, lakini utaratibu huo haupo tena.

Hatua hiyo ndiyo imekuwa ikichanganya baadhi ya watua na kusababisha wakutane na changamto ambayo miaka ya nyuma haikuwapo, lakini pamoja na yote hayo, bado kuna haja ya kuacha mazoea.

Marufuku ya vifungashio vya mifuko ya plastiki ni kama bado inaendelea kuwa changamoto hasa kutokana na mazoea ambayo yalikuwapo ya kupewa bure na sasa wanalazimika kuinunua.

Ili kutopoteza wateja wao, baadhi ya wafanyabiashara wa matunda na mboga wa Mbezi Mwisho Dar es Salaam wameamua kuwa na vifungashio vya ziada kwa wateja wao maalum.

Wanachofanya ni kwamba wateja wao ambao ni wa siku zote, huwauzia vitu na kuwawekea katika vifangashio hivyo, ambavyo baadaye huvirejesha hata baada ya siku moja au mbili.

"Kwangu mteja ni mfalme, kwa hiyo ni lazima nibuni mbinu za kuhakikisha ninaendelea kuwa naye kuliko ahamie kwingine, ndio maana nina mifuko ya ziada kwa ajili ya wateja maalumu," anasema mmoja wafanyabiashara hao.

Anasema, katika biashara ni muhimu kuwapo ubunifu na ni lazima kupambana na hali yoyote ile kwa lengo la kufanikiwa katika biashara, ndio maana yeye amefikia kubuni utaratibu huo baada ya kuona wateja wake wanahangaika.

Mfanyabiashara huyo anasema hivyo ndivyo vifungashio mbadala, ambavyo wanatakiwa kuvitumia kuwekea bidhaa za wateja, lakini tatizo ni baadhi ya watu kudhani kwamba vinatolewa bure.

Kwa hali kama hiyo ni vyema watu wakaachana na mazoea wakabiliane na changamoto zinazojitokeza na hatimaye wazizoee, pia wawaombe wazalishaji wa bidhaa hiyo kuongeza ukubwa na kuuza kwa bei nafuu.

**KABWELA NA FADHIL MOHAMMED**



## HABARI KITAIFA

# Msekwa awakumbusha Makamba, Kinana kuzingatia Katiba ya CCM

INATOKA UK. 2

hili lishughulikiwe."

Alisema kiutaratibu siyo sahihi kujaribu kukwepa jukumu hilo la watuhumiwa wenyewe kujisafisha kwa kukanusha tuhuma zinazowahusu, na kujaribu kulihamishia jukumu hilo kwa watu wengine.

"Hii ni kwa sababu watuhumiwa wenyewe ndio wanaojua ukweli kuhusu tuhuma hizo, na kama kweli hazina msingi, ni wajibu wao kufichua ukweli wanaoujua," alisema na kuongeza:

"Umuhimu wa jambo hili unatokana na kuwapo kwa dhana inayosema ukinyamaza kimya bila kukanusha tuhuma zilizoelekezwa kwako, ukimya wako huo unachukuliwa kwamba umekiri ukweli wa tuhuma hizo," alisema na kuongeza:

"Nafurahi na kuwapongeza, kwamba tayari mmetekeleza wajibu huo kupitia vyombo vya habari."

Kadhalika alitoa tahadhari kuwa wasiruhusu machungu ya tuhuma hizo kuwasahaulisha misingi, wakashawishika kutafuta njia za mkato za kuyashughulikia, ambazo zinakiuka Katiba ya chama.

"Madhumuni ya maelezo haya naomba ieleweke kwamba ni kukumbushana juu ya mambo haya ya msingi, ni kuonyesha ugumu uliopo wa kikatiba, kwa baraza kushughulikia malalamiko yenu, kama mlivyoomba," alisema.

Alifafanua kuwa ugumu huo unatokana na mambo manne ambayo ni Katiba ya chama haikutoa jukumu la kufanya kazi za kiuendeshaji, halikupewa mamlaka ya kusikiliza rufani zinazotolewa dhidi ya chama.

"Ni muhimu vile vile, kuzingatia kwamba Baraza, ni chombo maalum cha chama hicho, kilichoundwa na kupewa kazi maalum, iliyotajwa katika Katiba ya chama," alisema.

Vile vile, alifafanua kuwa Baraza hilo siyo kundi lolote tu la wazee wa chama kama yalivyo mabaraza ya wazee mengine, yaliyotajwa katika ibara ya 128 ya Katiba ya chama, ambayo wajumbe wake wanatajwa kuwa ni wazee wote wana-CCM, wenye umri kuanzia miaka 60 ambao kwa kuwa hawakupangiwa jukumu lolote maalum.

Alisema wazee hao wanadhaniwa kuwa wanaweza kushiriki katika utekelezaji wa shughuli zozote za chama kwa kutumia busara za uzee wao, kama watakavyoona wao kuwa inafaa.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa majibu hayo ni ya awali na kwamba anasubiri maelekezo ya baraza. Julai 17, mwaka huu, Kinana na Makamba walitoa tamko kwenda kwa baraza hilo kupitia vyombo vya habari, ambalo Msekwa amekiri kulipokea kupitia kwa Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye.

Mmoja wa walalamikaji, Makamba alisema lengo la waraka wao ni kueleza umma na wana CCM kuwa wao ni watu safi na hawahusiki kwa namna yoyote na tuhuma zinazotolewa na mwanaharakati huyo.

"Sisi ni watu safi hatuhusiki na jambo lolote, hiyo kazi tumeimaliza, sisi ni watu safi maneno yanayosemwa juu yetu ni uzushi, hatuhusiki na hizo tuhuma, serikali tuliitafuta sisi na tulishiriki kumweka Rais madarakani, baraza lijibu, lisijibu sisi tumemaliza kazi yetu," alisema Makamba.

Msekwa athibitisha

Juzi, barua ya Msekwa kwenda kwa Kinana na Makamba, ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii na Nipashe ilimtafuta Msekwa kuthibitisha kama barua hiyo imetoka kwake, lakini simu yake haikupokelewa.

Jana, alipatikana kwa njia ya simu na kuthibitisha kuwa barua hiyo ni ya kwake na ameamua kuisambaza kwa mitandao ya kijamii kama walivyofanya walalamikaji hao.

"Barua hiyo ni ya kwangu nawajibu Kinana na Makamba, busara inasema barua yoyote lazima ijibiwe, waliniandikia kwa njia ya mtandao nami nimewajibu kwa mtandao," alisema na kuongeza:

"Busara ya majibu yaende kwenye mtandao ili wasome mtandaoni kama ambavyo nilisoma mtandaoni," alisema baada ya kuulizwa kama walipelekea majibu ya barua hizo.

Juzi, mmoja wa walalamikaji, Makamba alipoulizwa kama wamepokea majibu ya tamko lao kutoka kwa Katibu Msekwa, alisema hawajapokea.

## Sababu za NEC kutoongeza muda daftari wapigakura

INATOKA UK. 2

kwa Zanzibar.

Pamoja na mambo mengine, Jaji Kaijage alitaja sababu sita zinazohusu uboreshaji wa daftrari la kudumu la wapigakura kuwa ni kuandikisha wapiga kura wapya waliotimiza umri wa miaka 18 ambao ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria.

Uboreshaji huo pia utahusu, kuandikisha wapigakura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 ifikapo Oktoba 2020 na utahusu kuhamisha taarifa za wapiga kura waliohama kata au majimbo yao ya uchaguzi.

Aidha, uboreshaji huo utahusu kutoa kadi mpya kwa wapigakura waliopoteza kadi zao za kupigia kura zilizotolewa na tume mwaka 2015 au ambao kadi zao zimeharibika na kusahihisha taarifa za wapiga kura ambao taarifa zao zilikosewa wakati wa uandikishaji wa mwaka 2015.

Pia utahusu kuandikisha wale ambao wana sifa, lakini hawakujiandikisha mwaka 2015 na kufuta kutoka kwenye daftari taarifa za waliopoteza sifa kama vile waliofariki dunia.

## Wanahabari wapewa somo kuhusu SADC


INATOKA UK. 4

"Huu wakati pia tuwape wananchi fursa ya kueleza matarajio yao kuhusu SADC, wangependa kama Taifa tufaidike nini kwenye SADC na watoe maoni yao mbalimbali kuhusu mkutano ujao," alisema Dk. Abas .

Dk. Abbas alisema ni matarajio yake kuna vyombo vya habari vinatenga muda wa kutosha kufuatilia masuala ya historia ya Tanzania na SADC kwa kuwa wapo viongozi wengi wa Jumuiya hiyo waliowahi kuishi nchini . Mwaka huu Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya hiyo umepangwa kufanyika jijiji Dar es Salaam Agosti 17 na 18, mwaka huu na Rais John Magufuli atapokea kijiti kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mkutano huo utakwenda sambamba na maonesho ya wiki ya viwanda kwa nchi wanachama ambayo yatafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere , Dar es Salaam kuanzia Agosti 5 hadi 9, mwaka huu, na kaulimbiu ni "Mazingira Wezeshi ya Kibiashara kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu ya Viwanda".

Mwakilishi wa GIZ, Dagmore Tawonezvi kutoka Botswana, ambaye pia ni Meneja wa programu ya kuimarisha utengamano baina ya nchi za SADC, alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kuwahabarisha wananchi kuhusu Jumuiya hiyo.




## MISA-Tan yalaani waandishi kudhalilishwa

INATOKA UK. 5

aliwarushia fedha kwa kile alichodai ni kuwatunza waliohudhuria mkutano wake kwa mfumo wa kurusha.

"Kwa mujibu ya video hiyo wapo waliookota fedha hizo, lakini wengine walikataa kwa kudhalilishwa huku wengine wakipambana kuokoa vifaa vyao vya kazi kama kamera, vinasa sauti na mic visiharibiwe na vurugu zilizokuwapo," ilieleza taarifa.

Pia MISA Tan ilieleza katika taarifa yake kuwa, Sheria ya fedha hairuhusu kukebehi fedha ya nchi kwa namna yoyote ile kwa kuwa ndiyo utambulisho wa taifa na tunu.

Taasisi hiyo imewataka waandishi wa habari kuelewa kuwa wao ndiyo walinzi wa taaluma yao hivyo wanatakiwa kutoa taswira njema, itakayoilinda taaluma na utu wao kwa ujumla.

Septemba 18, mwaka jana, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilitoa onyo kwa wanaodhihaki fedha ya Tanzania na kutambua kuwa ni umoja ya alama ya taifa na kwamba kuidhihaki na kukejeli noti na safaru za Tanzania ni kosa la jinai.

Vile vile, BoT ilisema ni dharau kubwa kwa kuwa serikali inatumia gharama kubwa kutengeneza fedha hiyo na kufanya hivyo ni kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu namba 332A cha kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002.

## HABARI KITAIFA

# JPM atoa siku 5 ujenzi wa meli

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

RAIS John Magufuli ametoa siku tano kuanzia jana kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha vifaa vya ujenzi wa chelezo ya kujengea meli na vifaa vya ukarabati wa meli vilivyokwama katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na mchakato wa kikodi, vinafikishwa katika Bandari ya Mwanza.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo juzi alipotembelea Bandari ya Mwanza kwa lengo la kukagua maendeleo ya ujenzi wa chelezo, ukarabati wa meli tano na ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria unaotekelezwa na kampuni mbili kutoka Jamhuri ya Korea kwa gharama ya Sh. bilioni 152.

Akiwa bandarini huko, Rais Magufuli alieleza kutofurahishwa na ucheleweshaji wa takribani mwezi mmoja wa makontena 58 yenye vifaa vya ujenzi vilivyoagizwa na kampuni za ukandarasi za Korea Total Marine Innovation (KTMI) na STX JV SAEKYUNG Construction Ltd kwa sababu ya kusubiri msamaha wa kodi huku akimtaka mkandarasi aache visingizio.

Meneja wa mradi wa ujenzi wa chelezo na ukarabati wa meli, Abel Gwanafyo, alisema ujenzi wa chelezo pamoja na ukarabati wa meli ya MV Victoria na Mv Butiama umepangwa kukamilika ifikapo Machi mwakani.

Kuhusu ujenzi wa meli mpya, Meneja mradi huo, Vitus Mapunda, alisema maandalizi ya vifaa vya meli hiyo itakayokuwa na uwezo wa kubeba tani 400 za mzigo, abiria 1,200 na magari makubwa na madogo 23 yanayohusisha usanifu, ukataji wa vyuma, injini mbili na majenereta matatu yamefikia asilimia 35 na kwamba makontena 300 yenye vifaa hivyo yatawasili nchini Septemba mwaka huu yakitoka Korea.

Baada ya kukagua hali ya meli ya Mv Victoria na Mv Butiama ambazo ukarabati wake umeanza, Rais Magufuli aliwasalimu wafanyakazi walioajiriwa katika mradi huo na kuwaagiza wakandarasi kuhakikisha wanalinda maslahi yao na kuzingatia sheria za usalama kazini.

Rais Magufuli pia aliagiza mitambo miwili ya kunyanyulia mizigo (cranes) iliyokuwa imeuzwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kurejeshwa mara moja.

Rais Magufuli, akiwa njiani kutoka Butimba alikofanya ziara ya kushtukiza kwenye Gereza Kuu la Butimba, alisimama na kuwasalimu wananchi waliokuwa wamekusanyika kwa maelfu katika eneo hilo na baada ya kuelezwa kero ya kukosekana kwa wodi ya wanaume katika Hospitali ya Wilaya ya Ilemela, alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza kuhakikisha jengo la wodi hiyo ambalo limetengewa Sh. milioni 300, linakamilika ifikapo Julai 30, mwaka huu, yaani siku 13 zijazo.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Mji wa Kibara, Jimbo la Mwibara wilayani Bunda mkoani Mara jana. **PICHA: WMN**

# Kilo milioni 2.8 za kahawa zakusanywa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

VYAMA vitatu vya ushirika mkoani Kagera vimekusanya kahawa kilo milioni 2.76 baada ya kupokea Sh. bilioni saba kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kama malipo ya awali kwa wakulima mkoani humo.

Hayo yamebainishwa na Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika mkoani Kagera, Robert Kitambo, wakati akizungumza na Nipashe ukiwa ni mwezi mmoja tangu uzinduzi wa msimu wa ukusanyaji kahawa kwa mwaka 2019/2020.

Alisema kwa mujibu wa takwimu zilizopokelewa hadi sasa tangu msimu huo kuanza kutoka Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Kagera (KCU), Chama cha Ushirika Wilaya ya Karagwe (KDCU) na Magata cha Wilaya ya Muleba kilo hizo zimetoka kwenye vyama vya msingi ambapo wakulima walisubiri msimu kuanza.

Aidha, kila chama kikuu kilifanya makisio ya kufikia malengo ya upatikanaji wa tani, ikiwa ni tangu kutangazwa msimu na hadi ukusanyaji wa kahawa unaendelea na kufikia viwango. KCU ni kilo milioni 1.34 wakati malengo ni kilo milioni 12.6.

KDCU imekusanya kilo milioni 1.6 wakati malengo ni kilo 3,500,000 na Magata kilo elfu 27,005 wakati lengo ni kilo 350,000 kwa kahawa ya maganda pekee.ko;']Alisema malipo ya awali k wa mkulima kwa kilo moja ya kahawa ni Sh. 1,100 ambayo imepangwa kulipwa kwa mfumo wa benki ambayo itaingia ubia na TADB ili kufikia mkulima aliyeko kijijini kupitia mawakala.

Kitambo alisema makisio ya ukusanyaji wa kahawa ikiwa katika hali ya maganda mkoa umepanga kuwa na kilogramu milioni 52 kwa kuwa Bodi ya Kahawa ilitakiwa kuanza ukusanyaji Juni.

## Kortini tuhuma za kuharibu mali, wizi halmashauri

**Na Jumbe Ismailly,**
IGUNGA

WAKAZI wawili wa mjini Igunga mkoani Tabora wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za wizi pamoja na kuharibu mali za halmashauri.

Waliopandishwa kizimbani ni Jovin Rwegasira (36), mkazi wa Mtaa wa Stoo na Saidi Sengo (32), mkazi wa Mtaa wa Mwayunge, mjini Igunga. Mwendesha Mashtaka, Elimajid Kweyamba, alidai washtakiwa hao wanashtakiwa kila mmoja kwa makosa mawili.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Lydia Ilunda, Kwenyamba alidai katika shtaka la kwanza la kuharibu mali kinyume cha kifungu 326(1) cha kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2002, Julai 3, mwaka huu majira ya asubuhi katika ofisi za Halmashauri ya Igunga, washtakiwa wakiwa wakazi wa mji mdogo wa Igunga waliharibu makusudi mashine mbili aina ya POS za kukusanyia ushuru wa taka. Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka huyo, mashine hizo ni IMEI Na. 862037029293452 /862037029304663 pamoja na IMEI 86203702993262/ 862037029304373 zote zikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi milioni 1.7, mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

Kwa mujibu wa Kweyamba, katika tarehe na muda tofauti kati ya Oktoba 19, mwaka jana na Juni 8, mwaka huu mjini Igunga, washtakiwa kwa pamoja waliiba fedha taslimu shilingi 2,308,000, mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, walizokuwa wameaminiwa kuzikusanya kama ushuru wa taka na kuzipeleka Halmashauri ya Igunga.

Alidai kuwa matokeo yake fedha hizo walizitumia kwa matumizi yao binafsi. Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa hao walikana, hivyo kesi hiyo kuahirishwa hadi Julai 22, mwaka huu, na washtakiwa kupelekwa mahabusu.

## Bil. 1/- yajenga ofisi za vijiji 20

**Na Christina Haule,** KILOSA

JUMLA ya Sh. bilioni moja zimetumia katika ujenzi wa ofisi za serikali za vijiji 20 vinavyotekeleza mradi wa mkaa endelevu wilayani Kilosa mkoani hapa.

Hayo yalisemwa jana na meneja mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS), Charles Leonard, wakati akizungumza na wadau wa misitu wakiwamo madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo na maofisa misitu.

Leonard alisema, ujenzi huo umetokana na sehemu ya makusanyo ya mapato ya mazao ya misitu ukiwamo mkaa endelevu na mbao.

Alisema, kufuatia makusanyo ya mapato kwa vijiji 20 vyenye mradi huo tangu umeanzishwe mwaka 2013 hadi 2019, wametenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji na kufanikiwa kujenga ofisi hizo.

"Fedha hizo zimetumika katika ujenzi wa ofisi 20 za serikali za vijiji 20 vya mradi, sambamba na kuweka samani ndani," alisema.

Hata hivyo, alifafanua kuwa kwa miaka hiyo saba, mapato ya ushuru wa mkaa kwa vijiji 20 ni zaidi ya Sh. bilioni 102, mapato ya wazalishaji mkaa ni zaidi ya Sh. milioni 920, ushuru kwenye mbao ni Sh. milioni 69 na halmashauri ni Sh. milioni 260.

Aidha, Leonard alisema mpaka sasa jumla ya vijiji 18 vipo kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi, huku vijiji 2 vikishindwa kufikia malengo kutokana na mgogoro wa mipaka.

Akifungua kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kilosa, Hassan Mkopi, alisema wamejipanga kuendeleza Usimamzi Shirikishi wa Misitu (USM), baada ya Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS), maarufu 'Mkaa Endelevu' kufikia mwisho Novemba 2019.

Mkopi alisema mradi wa mkaa endelevu umefanya mapinduzi ya kijamii, kiuchumi na maendeleo, hivyo wao kama wawakilishi hawanabudi kuuendeleza.

Alisema vijiji 20 ambavyo vipo kwenye mradi vimepata mafanikio makubwa katika USM na uhifadhi, hivyo vinapaswa kutumiwa kama mfano kuendeleza mfumo huo kwa vijiji vipya.

Mshauri wa Maliasili Mkoa wa Morogoro, Nanjiva Nzunda, alisema mradi huo umekuwa na matokeo chanya, hivyo madiwani wanapaswa kuuendeleza baada ya mradi kufikia mwisho.

Mradi huo unaotekelezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (Mjumita) na Shirika la Kuendeleza Nishati Asili Tanzania (TaTEDO) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Uswis (SDC), utafikia kikomo Novemba mwaka huu.

# Wakulima alizeti wanena mbegu chotara

**Friday Simbaya na George Tarimo,** IRINGA

BAADHI ya wakulima wa alizeti katika mikoa ya Iringa na Njombe wamesema kuwa bei kubwa ya mbegu chotara ya zao hilo imekuwa kikwazo kwa baadhi ya wakulima nchini kushindwa kufanya kilimo chenye tija.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa Maonyesho ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo mkoani Iringa, wakulima wamesema bei kubwa ya mbegu za alizeti imekuwa ikiwakatisha tamaa baadhi ya wakulima kushindwa kutumia mbegu hizo.

Walisema mbegu hizo zinawafanya wakulima kuendelea kutumia mbegu za alizeti za kienyeji ambazo zinadaiwa kuwa na mafuta kidogo.

Esta Mkula, mkulima wa kijiji cha Idindilimunyo katika Wilaya ya Wanging'ombe, mkoani Njombe, alisema kumekuwapo na changamoto ya bei kubwa ya mbegu za alizeti kwa wakulima, jambo ambalo limetajwa kuwa kikwazo kwao.

Akitolea mfano wa mbegu chotara aina ya (HYSUN 33), alisema kilo moja inauzwa Sh. 35,000 ambayo inasambazwa na Kampuni ya mbegu ya Bytrade Tanzania ambayo inaweza kupanda kwenye nusu ekari kwa hiyo ili kulima ekari moja ni lazima utumie kilo mbili ya mbegu hiyo kwa Sh. 70,000 wakati mbegu ya kienyeji inauzwa kwa Sh. 15,000.

Ingawa mbegu ya chotara inavumilia magonjwa, inastawi katika maeneo mengi, lakini changamoto kubwa ni bei ambayo ni kandamizi kwa wakulima.

Aliwataka wakulima kulima kilimo cha kisasa kwa kutumia mbegu bora kwa sababu zinakomaa muda mfupi.

Alisema pamoja na mafanikio waliyopata kwa kutumia mbegu bora, kilimo hicho kimepokelewa na wanawake wengi, lakini wanapatwa na changamoto ya wanaume wao kutoshiriki kikamilifu, huku wanawake wengi wakinyimwa ardhi na wanaume kwa ajili ya kilimo.

Kibwana Nyalusi wa Kijiji cha Italula katika Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, alisema bei ya mbegu ya kisasa inauzwa kwa bei kubwa, lakini kama ingeuzwa kwa bei nzuri wakulima wengi wangeitumia ili kuongeza kipato.

Alisema wakulima wengi Wilaya ya Kilolo na maeneo mengine wanatumia mbegu za kienyeji, ambazo inatumia muda mrefu kulinganisha na mbegu chotara.

Wamelishukuru Shirika la Care International Tanzania kupitia mradi wa kilimo cha alizeti usawa na thamani (ALUTA) kwa kuwaunganisha na mradi huo na kuwapatia mafunzo ya kilimo bora cha alizeti.

Naye Ofisa Kilimo kutoka Kampuni ya Bytrade Tanzania, Madaraka Mwalangwa, alisema kuelekea kuanza msimu wa kilimo kwa mwaka 2018/19, wakulima wote wa alizeti nchini wanatakiwa kutumia mbegu bora. Mwalangwa alizitaja sifa za mbegu hiyo kuwa inastahimili hali ya hewa na ukame.

Aliongeza kuwa mbegu nyingi zilizopo sasa hivi kiwango cha mafuta ni 45-48 na uzao wenye tija kuanzia kilo 800 mpaka 1000 kwa ekari. Sifa nyingine ya mbegu chotara huweza kupandwa maeneo mbalimbali na hukomaa baada ya siku 95 mpaka 110.

Meneja wa Ushirika wa Kiufundi (CARE), Fadhili Kasubiri, alisema changamoto ya bei ya mbegu za kisasa wakulima wanatakiwa kujiunga katika vikundi ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo ya mbegu.




Mkaguzi wa nje kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Erasto Juma, akiwasilisha taarifa wakati wa Baraza Maalumu la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga jana, kujadili hoja mbalimbali za ukaguzi wa hesabu za serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30 mwaka huu. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Mwanri aagiza zahanati kupelekewa watumishi

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

KATIBU Tawala Mkoa wa Tabora, ameagizwa kuhakikisha anapeleka watumishi wa sekta ya afya katika zahanati ya Chapera wilayani Igunga ili ianze mara moja kutoa huduma za matibabu kwa wakazi wa eneo hilo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wilayani Igunga wakati wa kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo la kujadili hoja mbalimbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema wakati mkoa ukisubiri ajira za watumishi wapya ni vema Katibu Tawala Mkoa kuangalia uwezekano wa kugawanya watumishi waliopo katika zahanati ya Champera na maeneo ambayo hayana watumishi ili wananchi wa maeneo hayo nao waweze kupata huduma za afya karibu na mazingira yao. Mwanri alisema hoja ya mkaguzi wa nje ni vema ikatatuliwa kwa kugawanya watumishi waliopo katika vitengo vingine katika maeneo yasiyokuwa na watumishi kabisa.

Katika hatua nyingine, Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imeagizwa kuhakikisha inakusanya deni la Sh. milioni 42.4 kutoka kwa wananchi ambao hajawalipia viwanja walivyouziwa.

Mwanri alitoa hoja hiyo na kuungwa mkono na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kufuatia hoja ya kamati ya ukaguzi kutoka ofisi ya mkaguzi wa nje baada ya kubaini deni hilo.

Alisema kiasi cha deni hilo ni lazima kikusanywe na hatua zichukuliwe ikiwamo wahusika kupewa mwezi mmoja ili walipe madeni yao, na wakishindwa viwanja hivyo virejeshwe halmashauri.

Mwanri alisema baada ya mwezi mmoja kuisha, wahusika ambao wameshindwa kulipia viwanja wanyang'anywe na viuzwe kwa wengine ili kulipa deni hilo.

Mkaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya CAG, Erasto Juma, alisema jumla ya mapato ya Sh. milioni 42.4 yaliyotokana na mauzo ya viwanja kwa wanunuzi 76 katika maeneo ya Nkokoto hayakukusanywa.

Alisema ni kiasi cha Sh. milioni 4 tu ndizo zilizokusanywa na kusalia kwa deni hilo.

# Takukuru yajisifu kudhibiti udhaifu ukusanyaji mapato

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara imejisifu kudhibiti mifumo dhaifu ya ukusanyaji mapato kwenye minada katika halmashauri na kudhibiti upotevu mkubwa wa fedha za umma.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mkuu wa Takukuru mkoani Manyara, Fidelis Kalungura, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za taasisi hiyo, kwa waandishi wa habari kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Kalungura alisema tatizo lililopo kwenye ukusanyaji wa mapato kwenye minada ni la mifumo mibovu ambayo haieleweki kwa kuwa haina uwazi katika utoaji wa stakabadhi kwa wananchi ambao wanawakatia.

"Tunafanya uchambuzi wa mifumo ili kugundua namna ambavyo fedha zinavyopotea kupitia mifumo mibovu, ambayo tulipoichambua tuligundua mapato yanayokusanywa na halmashauri zingine ni kidogo ikilinganishwa na kiasi ambacho kilianza kupatikana baada ya sisi kuichambua mifumo," alisema Kalungura.

Alitoa mfano Halmashauri ya Kiteto kuwa ilifanya ukusanyaji wa mapato kwenye minada na kupata Sh. 200,000 pekee kwa mwezi, lakini baada ya Takukuru kuingilia kati na kuifuatilia mifumo halmashauri hiyo inakusanya Sh. milioni nane kwa mwezi na hivyo kuonyesha kuwa mifumo iliyokuwapo ilikuwa dhaifu.

Mtaalamu huyo wa kupambana na kudhibiti rushwa alisema licha ya kuwatumia wakusanyaji wa mapato mifumo dhaifu na kuikosesha serikali mapato, bado wapo wataalamu wa halmashauri ambao wanajificha nyuma ya mifumo hiyo na kuikosesha serikali mapato yake kupitia vyanzo vyake halali kama hiyo minada.

Katika hatua nyingine, alisema kupitia mfumo wa ulipaji wa posho za madiwani za kazi na vikao mbalimbali, taasisi hiyo kuanzia Aprili hadi Juni 30, mwaka huu, imefanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. milioni 7.5, kupitia akaunti ya Takukuru.

Alifafanua kuwa fedha hizo zilizookolewa ni za madiwani wote wa Mkoa wa Manyara, lakini kiasi kikubwa cha fedha hiyo kimetoka Halmashauri ya Simanjiro ambao wamekwisha uelewa mfumo ambao umefafanuliwa vizuri na Takukuru.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho walifuatilia miradi ya maendeleo 25, ambayo ilikuwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 10.4 na fedha hizo zilifuatiliwa na kukaguliwa ili thamani ya fedha hiyo iweze kuonekana na miradi iwe na tija.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, Dk. Wilson Mahera (kushoto), akikata utepe na Mkurugenzi wa Maji kutoka Shirika la Water Boys', Nicole Woods, kuzindua mradi wa maji katika Shule ya Msingi Sekei. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Manesi waonywa kuwaachia wanafunzi wagonjwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MANESI nchini wameonywa kuacha tabia ya kuwaachia wanaofanya mafunzo kwa vitendo kazi za kuzalisha wajawazito, ili kuzuia vifo vinavyotokana na uzembe unaosababishwa na watu wasio na ujuzi, katika utoaji wa huduma za afya.

Pia watoa huduma za afya katika vituo mbalimbali vya afya na zahanati wametakiwa kuhakikisha hakuna vifo vinavyotokana na ujauzito badala yake wasimamie viapo wanavyoapa na kutoa huduma bora ili kinamama waweze kujifungua salama.

Akizungumza jana katika ufunguzi wa kampeni ya 'Jiongeze Tuwavushe Salama', Wilaya ya Arusha, Mkuu wa wilaya hiyo, Fabian Daqarro, alisema kuna malalamiko katika baadhi ya vituo vya afya na Hospitali ya Rufani ya Mount Meru kuwa utoaji wa huduma za afya si nzuri.

Pia alisema baadhi ya wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo huachiwa kazi za kuzalisha kinamama hali inayoleta madhara nyakati za kujifungua.

"Katika wilaya yangu sitaki kusikia kuna vifo vinavyotokana na uzembe mjirekebishe wenye hizi tabia, haiwezekani serikali ijenge vituo vya afya na zahanati, halafu nyie mnasababisha uzembe badala ya kuhudumia wagonjwa nyie manesi mnakunywa chai, acheni tabia hizi msiwaachie wanaojifunza kuwazalisha kinamama," alisema.

Alisema kampeni hiyo ya Jiongeze Tuwavushe Salama, ni endelevu inayowawezesha kinamama kuhudhuria kliniki, kujua kama wanaviashiria hatari na kupanga wapi watakapojifungulia na kuwaomba wajawazito kuhudhuria kliniki, ili kujua afya zao pamoja na watoto waliowabeba tumboni.

Naye Mganga Mkuu wa Jiji, Dk. Simon Chacha, alivitaja viashiria vinavyosababisha wajawazito kutojifungua salama ni pamoja na ucheleweshwaji wa kinamama kufika hospitali au kwenye vituo vya afya ngazi za jamii, ukosefu wa magari ya wagonjwa wa dharura, miundombinu, uzembe wa manesi na ukosefu wa vifaa vya kujifungulia.

Aliwaasa watoa huduma za afya pamoja na maofisa tarafa katika kata mbalimbali za wilaya na Jiji la Arusha, kuhakikisha wanawavusha salama wajawazito na kutoa huduma bora za afya kwa wananchi mbalimbali wanaofika vituo vya afya kupata matibabu.

Awali mzee wa kimila (Laigwanani), Tobiko Kiroini, alitoa rai kwa wataalamu wa afya, kuhakikisha wanatoa huduma za afya hata siku za mapumziko na sikukuu kwa kuwa wagonjwa hawana mapumziko.

"Sasa unakuta mama anakuja kituo cha afya au zahanati siku za sikukuu wanataka kujifungua, halafu unawaambia leo Jumamosi na Jumapili hakuna huduma hii sio sahihi," alisema.

Pia alisisitiza wasichana kuwaeleza wazazi au walezi wao kama wana ujauzito ili waweze kuhudhuria kliniki mapema na kuzuia vifo vinavyotokana na uzazi kwa kuwa baadhi ya wasichana wanaficha ujauzito bila wazazi kujua hali inayowasababishia vifo wanapokwenda kujifungua hospitalini au vituo vya afya.

## TPRI yahimiza matumizi sahihi vifungashio

**Na Mary Mosha,** BABATI

KAIMU mkuu wa kitengo cha udhibiti wa viuatilifu na utunzaji wa mazingira kutoka TPRI, Felex Mwema, amesema utafiti wa awali umeonyesha asilimia kubwa ya wakulima wilayani Babati licha ya kutumia viuatilifu hivyo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, bado hawajui matumizi sahihi ya utunzaji wa vifungashio hivyo na kusababisha madhara kwa afya za watu.

Utafiti huo uliofanyika katika kata tano, ulionyesha wagonjwa zaidi ya 29 walifika hospitali na kupata msaada baada ya kupata madhara yatokanayo matumizi yasiyo sahihi ya vifungashio vya viuatilifu.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wataalamu wa kilimo na wasambazaji wa viuatilifu katika Halmashauri ya Babati, kuwa ukosefu wa elimu ya usafishaji na utunzaji wa vifungashio vya viuatilifu ni hatari kwa jamii zinazozowazunguka.

Alisema ikiwa vifungashio vya viuatilifu havitasafishwa vyema baada ya kumalizika kwa matumizi ya sumu, asilimia 10-14 hubaki kwenye vifungashio hivyo.

"Tumekuja na mpango wa kutoa elimu maalumu kwa jamii ya watu wa Babati kuhusu namna bora ya kusafisha vifungashio hivyo, baada ya kumaliza matumizi na kujenga vibanda ambavyo vitasaidia katika ukusanyaji wa vifungashio, ili kuepuka kuvitupa ovyo kunakoleta madhara," alisema. "Sumu inapomalizika katika kifungashio, kilaze kifungashio kwenye bomba kwa sekunde thelathini, kisha weka maji kiasi yatingishe sekunde thelathini na urudie kwa mara tatu, kisha toboa kifungashio hicho ili kisiweze kutumika kwa matumizi mengine ya binadamu na utapeleka katika eneo lililotengwa kwa ajili ya matumizi mengine," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Babati Elizabeth Mtundu, alikiri kuwapo kwa kuzagaa kwa vifungashio hadi kwenye vyanzo vya maji hasa maeneo ya mashamba ya wakulima na kusema kuwa kupitia mafunzo haya wataalamu wanaweza kufanya mabadiliko makubwa na kuiokoa jamii inayowazunguka. "Hii ni wazi kuwa wataalamu hawa wa kilimo waliopata mafunzo watawafikia wakulima wote wa Babati na viunga vyake ili kutoa elimu hiyo huku tukiahidi sisi kama watendaji tutafuatilia katika kuhakikisha mabadiliko yanaonekana kwa kutokomeza," alisema.



Baadhi ya wataalamu wa kilimo katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara wakifuatilia mafunzo ya namna bora ya kusafisha vifungashio vya viuatilifu baada ya kutumia sumu ili kuepusha athari za kiafya na kimazingira. **PICHA: MARY MOSHA**

# Udhalilishaji kingono waathiri wanafunzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MADHARA yanayotokana na ukatili na udhalilishaji wa kingono dhidi ya wanafunzi wanaodaiwa kufanyiwa vitendo vya ubakaji na ulawiti katika kata ya Kaloleni, Manispaa ya Moshi, yameanza kujitokeza, huku ikielezwa hali hiyo inawaumiza kisaikolojia baadhi yao.

Baadhi ya wanafunzi hao hivi sasa wanatishia kukatisha masomo yao. Sababu wanazotaja wanafunzi hao kutaka kukatisha masomo ili kukwepa aibu hiyo, inaelezwa kuwa ni baadhi ya wanafunzi wenzao wanawaita wahanga hao, majina ya wanaume waliowafanyia ukatili huo.

Kwa nyakati tofauti Nipashe imekuwa ikifuatilia matukio ya aina hiyo katika wilaya sita za mkoa wa Kilimanjaro, ikiwamo Wilaya za Moshi na Rombo ambazo zinatishiwa na ukatili wa kijinsia, kingono, migogoro ya kifamilia, ardhi na mirathi. Uchunguzi wetu katika Kata ya Kaloleni, Manispaa ya Moshi, unaonyesha kuwa watoto walioguswa na ukatili ama udhalilishaji huo wa kingono kwa nyakati tofauti, umesababisha baadhi yao kuingiwa na hofu ya kwenda shule kutokana na watoto wenzao kuwatania kwa kuwataja kwa jina la mtuhumiwa wa tukio hilo.

Alipotafutwa kuelezea hatua ambazo zimechukuliwa hadi sasa na Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Moshi Mjini (Washemom), Shaban Mkwizu, alisema: "Hizo taarifa tunazifuatilia kwa karibu sana na nitatoa taarifa kuhusu hatua tulizochukua baada ya kukutana na wazazi na walimu wa eneo husika na kujadiliana namna ya kumaliza huo unyanyapaa na kuwasaidia watoto hao kuendelea na masomo.

Watoto hao wenye umri chini ya miaka minane ambao majina yao yamehifadhiwa, wamesema hofu hiyo inajengwa na wenzao ambao wanawanyima amani kwa kuwaita majina ya ubini wa mtuhumiwa wa ubakaji.

Walipotafutwa kuzungumzia zaidi madai ya watoto hao, baadhi ya wazazi na walezi wa watoto wanaotajwa, Flomena Pascal, Fatina Amiri na Anna Msuya wameeleza kwa nyakati tofauti kwamba namna pekee ya kuwasaidia watoto hao kuendelea na masomo yao kwa sasa, ni kuonya unyanyapaa huo usiendelee.

Mmoja wa wazazi hao, Anna Msuya alisema: "Mimi nafikiria kumhamisha huyu mtoto shule ili aweze kuepuka hiyo hali na aendelee na masomo yake, lakini kuna kila sababu bodi ya shule na walimu wakawaonya wanafunzi wengine wasiwanyime furaha watoto wanaohusishwa na matukio hayo."

"Huyu mtoto wangu anatumia dawa za kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa na ukimwi (PEP), ndani ya saa 72 tangu kutokea kwa tukio hilo, leo kaniambia haendi shule wenzake wanamuita kwa jina la mtu aliyemfanyia ukatili," alisema mzazi mwingine, Flomena Pascal. Mwalimu wa shule anayosoma mmoja wa watoto ambaye alishafanyiwa ukatili huo wa kingono ambaye ameomba jina lake na shule visitajwe, alikiri mwanafunzi huyo kutaniwa na wenzake wawapo katika michezo yao na tayari wameanza kuchukua hatua.

"Ni kweli shule yetu ina baadhi ya wanafunzi waliofanyiwa ukatili wa kingono, wenzao huwa wanawatania na hivyo kuwaondolea furaha na kujiamini hata wakiwa darasani, tumewaonya wale wanaowatania wenzao na kuhimiza upendo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kaloleni, Ndama Ndama, alikiri kupata taarifa kuhusu matukio hayo ya udhalilishaji kwa watoto, akisema tayari wameanza mipango ya kuwahamisha shule watoto hao ili kuwaondolea adha wanayopata sasa.

"Hili jambo tumelizungumza katika mtaa wetu na tumewasiliana na shule husika na sasa tunatarajia kuwahamishia watoto hawa katika Kata za Pasua na Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, lengo likiwa ni kuwasitiri na kuwapa uhuru zaidi. Hivi karibuni pia hapa kwetu Kaloleni kulitokea tena tukio la udhalilishwaji wa watoto watano, ingawa jambo hilo liko katika vyombo vya sheria," alieleza Ndama.

# Tembo wazua hofu kwa wakazi wa Siha

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKAZI wa maeneo ya Gararagua, Miti Mirefu, Ndumeti na Sanya Juu katika Wilaya ya Siha, wameeleza kuishi kwa hofu, baada ya tembo wanaodaiwa kutoka Msitu wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na Kambi ya Ndarakwai kuvamia mashamba ya wakulima na kuharibu kiasi kikubwa cha mazao ya chakula.

Pia, tembo hao wanadaiwa kuzagaa hadi kwenye vijiji vya jirani na Wilaya ya Siha ambayo ni Tingatinga na Ngereiyani vilivyopo katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha.

Akithibitisha kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu uvamizi huo wa tembo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Godson Ngomuo, alisema kwa sasa tembo hao wanaondolewa mashambani na maofisa wa wanyamapori ili kunusuru chakula kisiendelee kuharibiwa.

"Nimepokea hayo malalamiko kwamba wanyama hao wamevamia baadhi ya maeneo katika wilaya yetu ikiwamo Kata ya Gararagua, Miti Mirefu, Indumeti na Kata ya Sanya Juu, nimeambiwa tembo hao wametokea Kinapa (Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro) na katika maeneo ya Ndarakwai na vijiji vya Tingatinga na Ngeriani katika wilayani Longido," alisema Ngomuo.

Diwani wa Kata ya Gararagua, Zakaria Lukumai, alisema katika kata yake, vijiji vya Magadini na Mawasiliano, tembo hao wameharibu vibaya mazao ya wakulima.

Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Lazaro Mwafuko, alipoulizwa kuhusu hatua walizochukua kuwaondosha tembo hao alisema, "Gari letu ni bovu na halipo, lipo Temesa (Wakala wa Ufundi na Umeme), kwa ajili ya matengenezo," alisema.

Hata hivyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Barnaba Mbwambo alisema malalamiko hayo yanafanyiwa kazi.

Aidha, kutokana na majibu hayo, Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo limetaka baadhi ya magari yake yatumike kuwafukuza wanyama hao hadi hapo gari hilo la maliasili litakaporejea.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, alisema makundi ya tembo hao ni mengi na yanatembea kwa makundi kati ya 50 na 80.

# Wajifungulia nje ya zahanati kisa huduma

**Na Mary Mosha,** ROMBO

WANAWAKE wanaoishi katika kijiji cha Nguduni, Kata ya Mahida, Wilaya ya Rombo, wanalazimika kujifungulia nje ya zahanati ya Mahida kutokana na kukosa huduma, wanapofikishwa katika zanahati hiyo nyakati za usiku.

Wananchi wa kijiji hicho walitoa malalamiko hayo jana, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agnes Hokororo, aliyekwenda kusikiliza kero za wakazi hao.

Catherine Tarimo, alimweleza mkuu huyo wa wilaya kuwa wakati wa usiku wamekuwa wakifika katika zahanati hiyo na kukosa huduma, wakielezwa na wahusika kwamba hakuna daktari wa zamu, wala wahudumu.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), hapa kuna mambo ya ajabu sana, wanawake hasa kinamama wajawazito wanapokwenda au kupelekwa katika zahanati ya Nguduni, lugha zinakuwa gongana, wanaambiwa hakuna daktari wala muhudumu muda huu, kwa hiyo changamoto iliyopo hapa ni hiyo tusaidie," alifafanua zaidi, mkazi mwingine, Aurelia Shayo.

Kwa mujibu wa Aurelia, kutokana na wanawake wajawazito kukosa huduma nyakati za usiku, hali hiyo imechangia baadhi ya kinamama kujifungulia nje ya zahanati hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mahida Nguduni (VEO), Agness Kauki, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, alikiri kupokea taarifa kuhusu kinamama hao kujifungulia nje ya zahanati.

Akijibu malalamiko hayo ya wananchi wa Nguduni, Hokororo alisema serikali inafuatilia kujua ukweli wa malalamiko hayo ya wananchi na itachukua hatua kali, iwapo itajiridhisha kwamba watumishi wa zahanati hiyo wamekiuka maadili ya kazi yao waliyoapa kuitumikia.

"Nawahakikishia kwamba nitachukua hatua kwa kumwajibisha mganga mkuu wa wilaya kwa kushindwa kusimamia watu wake na hata kujua kama kuna jambo kama hili," alieleza Hokororo.

ama
ALHAMISI JULAI 18, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



**Makazi yenye miaka 9000 yagundulika Yerusalemu**

Ukurasa 17



KITISHO SARATANI

Vinywaji vyenye sukari vinaleta saratani?

Ukurasa 20



Ukurasa 16

## BINGWA MUHIMBILI AFUNGUKA KISA BODABODA KUKWEPA KOFIA NGUMU



# Hawa ni miongoni mwa maelfu wanaoangamia, yumo kakakuona

Ukurasa 19

## WHO: Vyakula vya watoto wachanga vina kiwango cha sukari kupita kiasi



TAFITI mpya mbili zilizofanywa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kanda ya Ulaya zimebaini kuwa vyakula vinavyotangazwa kwa ajili ya watoto wenye umri wa chini ya miezi sita vinakiuka kanuni na vina kiwango cha juu cha sukari kupita kiasi.

Tafiti hizo zimefanywa kwa kukusanya takwimu kutoka vyakula au vinywaji 7955 vinavyouzwa kwa ajili ya watoto wachanga kutoka maduka 516 kwenye miji minne ya Vienna, Austria; Sofia, Bulgaria; Budapest, Hungary; na Haifa, Israel kati ya mwezi Novemba mwaka 2017 hadi mwezi Januari mwaka jana.

Taarifa hiyo ya WHO kanda ya Ulaya iliyotolewa karibuni jijini Brussels nchini Ubelgiji, imesema katika miji yote hiyo minne, idadi kubwa ya bidhaa kati ya asilimia 28 hadi 60 ilitangazwa kuwa inafaa kwa ajili ya watoto wenye umri wa chini ya miezi 6 kinyume na kanuni ya WHO inayokataza vyakula hivyo kutangazwa hivyo kwa kuwa watoto wenye umri wa chini ya miezi 6 wanapaswa kunyonya maziwa ya mama pekee.

Halikadhalika, katika miji mitatu, nusu ya bidhaa zilikuwa na zaidi ya asilimia 30 ya sukari na viambato vingine ambavyo vinachochea mtoto kupenda vyakula vyenye sukari.

Akizungumzia tafiti hizo, Mkurugenzi wa WHO kanda ya Ulaya, Dk. Suzanna Jakab amesema lishe bora tangu utotoni imesalia kuwa jambo la msingi katika kuchochea ukuaji wa mtoto na hali nzuri ya baadaye kiafya.

Dk. Jakab anasema kuepusha sukari kupita kiasi utotoni kunasaidia kuzuia uzito kupita kiasi, utipwatipwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo huchochewa na lishe duni.

Na hivyo kwa kuzingatia vipimo sahihi itakuwa rahisi kufikia lengo namba 3 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG) la kusongesha afya na ustawi kwa watu wote.

WHO inasema kuwa ijapokuwa vyakula kama matunda na mboga za majani kiasili vina sukari ambayo inafaa kwa watoto, bado vyakula vya rojo vinavyouzwa kibiashara vina kiwango cha juu cha sukari na kutia hofu kubwa. **HABARI UN**

MAZINGIRA

# Teknolojia ya kupanda mimea ndani ya maji inahitajika vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

KILIMO cha haidroponiki ni sayansi ya kisasa ya kuotesha mazao bora yenye tija kwa muda mfupi zaidi bila kutumia udongo kabisa, badala yake mimea hupandwa kwa kutumia maji na virutubisho vilivyoyeyushwa majini (hydroponic nutrients).

Hydro ni neno la Kilatini linalomaanisha maji. Hivyo, badala ya kupanda ardhini unaweza mbegu ndani ya maji.

Mathalani, kuzalisha chakula cha mifugo kiitwacho hydroponics fodder hiki ni chakula au kimea kinachooteshwa kwa kutumia mbegu za shayiri au ngano ili kupata mlo wa mifugo mfano kuku, ng'ombe, sungura, nguruwe, mbuzi na kondoo.

Hata hivyo, haidroponiki zinaweza kutumiwa kulima mboga za aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya familia na pengine kilimo. Ili kuotesha mbegu kwa utaratibu huu utahitaji kuwa na banda maalum la kuoteshea lenye ukubwa wowote, dumu la lita 20 la maji.

Ili kufanikisha hatua hiyo unahitaji kuwa na virutubisho vya Haidroponiki (Hydroponics Nutrients), Sprayer (chupa ya kunyunyiza maji yenye matundu madogo ili maji yamwagike kama mvua), kwa mbegu za shayiri au ngano ni vyema kuchagua mbegu ambazo hazijashambuliwa na wadudu na pia unatakiwa uwe na chombo cha kuloweka mbegu, unaweza kutumia ndoo ya aina yoyote kwani itatakiwa uziloweke kwa siku chache.

Madhumuni ya sayansi hii ya uoteshaji wa mbegu mbalimbali ni kwa ajili ya kupata majani ya kulisha mifugo kama vile, kuku, mbuzi, ng'ombe, kondoo. Ila kama ni mboga zinaweza kulimwa mathalani nyanya zikaitwa hydrponic tomatoes kulingana na aina ya mbegu husika.

### FAIDA YA HAIDROPONIKI

Ili kupatia picha halisi ni vyema kufahamishwa faida zilizopo za matumizi ya hydroponic fodder kwa mifugo.Kwa uchache baadhi ya faida hizo ni unafuu mkubwa ikilinganishwa na gharama za chakula cha kununua madukani au viwandani. Kuna kiwango kikubwa cha virutubisho na vitamini zaidi ya chakula cha kawaida cha mifugo, hupunguza magonjwa ya mfumo wa hewa kama vile mafua kwa mfugaji na mifugo kwani hakina vumbi kabisa. Chakula kinachozalishwa kwa utaratibu huu kina protini na nishati nyingi zaidi mara tatu ya inayopatikana kwenye vyakula vya kawaida vya mifugo kama kuku.



Mimea iliyooteshwa kwa kutumia teknolojia ya haidroponiki. **PICHA : MTANDAO**

> **Mmea huu unaoteshwa katika chombo maalum 'tray' ambacho kipo katika hali ya usafi na kina matundu kiasi ili kusaidia maji yasituame wakati wa kumwagilizia.**

Mifugo ikila misosi hii hukua haraka sana kutokana na wingi wa protini ambayo hufanya kazi ya kujenga mwili na kukuza. Chakula hicho ni laini sana na kitamu kwa kuku na mifugo yote.

Umeng'enyaji wa chakula hicho huongezeka kutoka asilimia 30 kwa chakula cha kawaida hadi 95 kwa chakula cha haidroponiki hivyo chakula kingi kutumiwa na mwili mwa mifugo.

Haidroponiki, kama ilivyoelezwa ni utaratibu wa kuotesha mimea kwa kutumia maji bila kuhusisha matumizi ya mchanga wala udongo au kuitoipanda kabisa katika ardhi.

Mmea huu unaoteshwa katika chombo maalum 'tray' ambacho kipo katika hali ya usafi na kina matundu ya kiasi ili kusaidia maji yasituame wakati wa kumwagilizia.

### UTARATIBU

Uoteshaji wa mbegu za ngano kwa njia hii ni ili itumike kama chakula cha mifugo mfano, kuku, ng'ombe, sungura na nguruwe Ili kuotesha mbegu kwa utaratibu huu, utahitaji vifaa kama trei ya plastiki au alminium yenye matundu inapendeza ikiwa na umbo la mstatili.

Unatakiwa kuwa na chupa ya kunyunyizia maji, mbegu za shairi au ngano au nyanya chagua zile ambazo hazijatobolewa na wadudu. Ni muhimu pia kuwa na chombo cha kulowekea mbegu , wakati mwingine unaweza kutumia ndoo yoyote.

Chujio la plastiki ni muhimu kama hakuna unaweza kutumia kitambaa safi.

Mbegu hizo zinapandwa kwenye chombo chenye uwezo wa kuingiza maji tena yasituame.

### TANZANIA

Pengine ni muhimu kuanzishwa teknolojia hiyo hapa Tanzania kwa vile kuna maji ya kutosha, maeneo mengi yenye kuwezesha kilimo hicho au kifanyike mijini na vijijini.

Vyuo vya Ufundi kama Taasisi ya teknolojia Dar es Salaam, (DIT), vinavyohaulisha teknolojia hiyo vina nafasi ya kuifikisha mijini na vijiji ili Watanzania wengine nao wafaidike.

Pengine changamoto ni kupata hizo kemikali na virutubisho, suala ambalo pia kutumia teknolojia linaweza kupatiwa ufumbuzi.

MAZINGIRA

# Ndiyo wakati wa kuhimiza viwanda vya kemikali asilia

Na Gaudensia Mngumi

WADAU wa kilimo na mazingira watakubaliana na ukweli kuwa matumizi ya kemikali kudhibiti magonjwa

ya mimea ni jambo linaloongeza hasara kuliko faida.

Ni kwa sababu kemikali za viwandani zinahusishwa na kuleta maradhi kama saratani, kuharibu ikolojia na hata kuchangia uchafuzi wa mazingira, hivyo mchango wake ni hasara zaidi kuliko tija.

Zama hizi serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda ndiyo wakati wa kuwahimiza wawekezaji kwenye viwanda vya viuatilifu vya asilia visivyo na kemikali za sumu.

Pamoja na serikali kusaidia uwekezaji ihusike pia kwenye utafiti na upatikanaji wa dawa pamoja na mbolea za asili ambazo hazitokani na kemikali za viwandani ili kulinda mazingira na afya za Watanzania.

Ni dhahiri kuwa walaji wengi duniani wanapenda kutumia mazao yaliyozalishwa kwa njia ya kilimo hai (organic farming) kisichotumia kemikali wala sumu za kuua wadudu.

Kwa hiyo kukiwa na viwanda wakulima watapata dawa hizo ili kudhibiti magonjwa aidha soko la mazao yao ni la uhakika kwa kuwa duniani kila mmoja angependa kula chakula kisicho na mabaki ya taka za kemikali.

Kadhalika, ni vyema wakulima wakaelezwa umuhimu wa mbolea na viuatilifu visivyo na kemikali za sumu kwenye kutunza mazingira na bayoanuai.



Mbegu, matunda na majani ya mwarobaini pia pilipili ni malighafi zitakazotumiwa kuzalisha kemikali kwenye viwanda vya viatilifu asilia. **PICHA:MTANDAO.**

**UTAFITI**

NI dhahiri kuwa ili dawa mbalimbali zitumike kwenye kuzalisha mazao na ili ziwe na tija ni sharti kuzifanyia utafiti ili kufahamu viwango vya sumu vinavyoweza kuua au kudhibiti wadudu katika mimea bila kuleta madhara.

Lakini pia kufahamu athari zake kwa afya na mazingira ili ifahamike iwapo

kuna tija ama hasara kiafya kwa mlaji na mazingira. Hapa ni lazima taasisi zifanye utafiti, pengine ni wakati wa serikali kubeba jukumu hilo sasa.

Kwenye maeneo mengi mimea kama mwarobaini, aloevera na minyaa inatajwa kuwa inafaa. Ni wakati wa kuhimiza ujenzi wa viwanda ili kupata viuatilifu hivyo kwa wingi.

Sehemu nyingi za Tanzania matumizi ya mwarobaini kama kiuatilifu cha asili, yanafanyika na mmea huo unaelezwa kuwa umeshafanyiwa utafiti na kugundulika kuwa unaweza kudhibiti baadhi ya wadudu kwenye mimea.

Wizara ya Kilimo inapohamasisha ujenzi wa viwanda ihimize dawa kama hiyo izalishwe ili iendelee kutumiwa na wakulima katika

maeneo mbali mbali kukabiliana na magonjwa na wadudu waharibifu, pia ifanikishe ulinzi wa mazingira na afya za walaji.

Dawa kama DDT zinaelezwa kuwa zinapoingia ardhini au kwenye maji zinadumu kwa karne nyingi.

Mathalani, DDT iliyotumika miaka mingi iliyopita itaendelea kuonyesha athari kubwa kwa miaka mingi ijayo kwa wanadamu walioila na kwenye mimea kutokana na sumu hiyo kuendelea kubaki majini na ardhini.

Kuna maelezo kwenye mitandao kuwa DDT imesababisha watu wengi kupata saratani, wanyama na mimea waliathirika pia, ikiwamo kuku kutaga mayai yenye kaa kaa laini na yasiyoweza kutamiwa na kuzalisha vifaranga. Hili likitokea ni kuua kizazi cha wanyama husika.

Inaelezwa kuwa dawa kama hizi sumu yake inajikusanya kwenye seli za mafuta kwenye miili ya wanyama na binadamu na

na kuleta madhara yanayosababisha vifo na kwa ujumla huvuruga mfumo mzima wa ikolojia duniani.

**MATUMIZI HATARISHI**

Viwanda vya kemikali za asili vinahitajika kwa sababu, kuna dawa ambazo zinadaiwa kuwa zikutumiwa zinaondoka haraka

kwenye mazingira .

Hivyo zinaweza kutumiwa kunyunyuziwa mboga na matunda, lakini wanaozitumia hawazitumii kwa usahihi kutokana na uzembe au kutojali afya za binadamu.

Kwa mfano wanapulizia kwenye nyanya, matango, mchicha au kabichi na baada ya muda mfupi huvuna na kupeleka mazao sokoni yakiwa na kemikali hizo . Hali hiyo si salama kwa vile bado kuna sumu.

**MBOLEA ASILIA**

Pamoja na sumu zinazonyunyiziwa kwenye mimea kuna mbolea zinazowekwa

ama kuikuza au kuipandia nazo zina kemikali ambazo wakati mwingine huendelea kuleta athari kwa watumiaji na mazingira na ekolojia nzima.

Kuna baadhi ya wakulima ambao humwagilia mbolea ya chumvichumvi kwenye mboga na kuziuza muda mfupi baadaye, jambo linalosababisha wateja kula mbolea hiyo.

Hilo linaweza kutokea kwa sababu sumu hubakia na kuhatarisha maisha kwa kuwa haijachakatwa kikamilifu na kufyonzwa na mmea hali inayotishia afya ya walaji ambao hula 'nitrogens' ambayo ni kemikali kubwa kwenye mbolea ya chumvichumvi.

> **Kuna maelezo kwenye mitandao kuwa DDT imesababisha watu wengi kupata saratani, wanyama na mimea waliathirika pia, ikiwamo kuku kutaga mayai yenye kaa kaa laini na yasiyoweza kutamiwa na kuzalisha vifaranga.**

Masuala ya kilimo hai au cha kijani ni muhimu zama hizo kuboresha afya za watu

na mazingira kwa kuzingatia ufugaji na ukulima usiotumia viuatilifu vya kemikali za sumu.

Pamoja na kuhamasisha viwanda hivyo ni vyema pia kuwawezesha wanavijiji nao ili wajenge viwanda vidogo vya kuzalisha kemikali asilia kwa manufaa yao.

Wazalishaji wa mboga na matunda wakifundishwa na kuwezeshwa kuhusu kilimo hai watazalisha mazao ya aina mbali

mbali kwa gharama nafuu huku wakiepuka kemikali.

Kwa ujumla kutumia mbolea za asilia kunaboresha ardhi na kuzalisha chakula kisicho na kemikali za sumu tena mkulima hana gharama kubwa.

Kemikali na dawa za viwandani zina gharama kubwa lakini zina taathira kiafya na mazingira lakini dawa za asili kama mwaroabini, pilipili, aloivera, majivu na mkojo wa sungura ni nafuu na hulinda afya.

Mwi

PICH

AFYA

# BINGWA MUHIMBILI AFUNGUKA KISA BODABODA KUKWEPA KOFIA NGUMU

- Ni chanda na pete kwa magonjwa ya ngozi
- Bodaboda wakiri uchafu, wadai 'hamna jinsi'
- Abiria kinamama wafunguka mazito ya kwao
- Darasa la bure lapatikana jijini Kigali, Rwanda

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

LICHA ya Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, kutomlazimisha abiria wa pikipiki kuvaa kofia ngumu au 'helmet' kwa usalama wake, kumekuwapo changamoto ya matumizi ya kofia hizo. Hofu ni kuambukizana magonjwa ya ngozi na uchafu wa helmet unaotokana na ukweli kuwa haifuliwi.

Sheria hiyo inamtaka dereva wa chombo cha moto cha magurudumu mawili au matatu kuvaa kofia ngumu, lakini kuna malalamiko kwamba iko kimya kwa abiria wa chombo hicho.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kutovaliwa kwa kofia hizo, ni miongoni mwa vitu vinavyochangia vifo kwenye ajali za pikipiki.

Kikosi kinaeleza kuwa mwaka 2017 kulikuwa na ajali 1,459 zilizosababisha vifo 728 na majeruhi 1,090.

Takwimu za ajali kwa mwaka 2018 zinaeleza kuwa zilikuwa 876 na zilisababisha vifo vya watu 366 na majeruhi 994.



Dereva wa pikipiki akiwa na kofia ngumu huku abiria wake wote wakiwa hawajavaa kofia. **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI.**

**VIFO VYA KOFIA**

Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabara mkoani Dodoma, Nuru Selemani, anasema kati ya Januari na Desemba mwaka jana, zilitokea ajali za pikipiki 350 mkoani Dodoma na kusababisha vifo vya watu 60.

Anasema, asilimia 90 ya vifo vya ajali za pikipiki zilitokana na kutovaa kofia ngumu na mkuu wa kikosi hicho, anasema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya waendesha pikipiki kutofuata taratibu, kanuni na sheria za usalama barabarani kwa kuogopa zaidi askari badala ya kufuata sheria zinazowaongoza na kulinda maisha yao.

"Kumekuwapo na jitihada mbalimbali za kupunguza ajali ikiwamo ukamataji wa makosa ya usalama barabarani, kutoa elimu kwa makundi yote ya watumiaji wa barabara,"anasema Selemani.

**ABIRIA WAHOFU**

Abiria wengi wanapohojiwa na Nipashe, wanabainisha hofu yao iko katika kofia ngumu wanazopewa na waendesha pikipiki, kwamba ina hatari ya kuwaambukiza magonjwa ya ngozi.

> **"Tunajua umuhimu wa kuvaa kofia ngumu kuzuia madhara kichwani pale inapotokea ajali, lakini wenzetu hawa waendesha pikipiki, kofia zao ni chafu, hata hazisafishwi, unakutana na uchafu na harafu vinatisha nikiweka tu lazima kujikuna sana na kuwa na mba kichwani,"anasema.**

Mkazi wa jijini Dodoma, Mussa Enock, anasema tatizo la kukwepa kuvaa kofia hizo, linatokana na uchafu uliokithiri, hali inayowahatarishia kupata magonjwa ya ngozi. Enock anafafanua:

"Nimenyoa kipara sasa kama kuna maambukizi ya magonjwa ya ngozi ni rahisi kupata, kofia zao unazopewa kuvaa unakuta hadi zina ukurutu."

Rhoda Chikoti, mkazi wa kijiji cha Bahi sokoni kilichopo wilaya ya Bahi, anasema kofia hizo licha ya kuwa chafu, pia ni kikwazo kwake kwa kumsababishia mba na kuwashwa ngozi mara nyingi.

"Tunajua umuhimu wa kuvaa kofia ngumu kuzuia madhara kichwani pale inapotokea ajali, lakini wenzetu hawa waendesha pikipiki, kofia zao ni chafu, hata hazisafishwi, unakutana na uchafu na harafu vinatisha nikiweka tu lazima kujikuna sana na kuwa na mba kichwani,"anasema.

Rhoda anashauri kuwa ni vyema kofia zikafanyiwa usafi ili abiria waweze kuzivaa wakati wote wanapotumia usafiri huo.

Mkazi wa mtaa wa Kinyambwa jijini Dodoma, Sara Moses anasema muundo wa kofia hizo kwa wanawake hasa wanaosuka si mzuri hivyo kumlazimu kutovaa.

"Mtu umesuka msuko wako, ukitaka kuvaa hiyo kofia ya pikipiki huwezi maana haitakaa wala kufunga. Pia mimi naogopa kupata maradhi kwa kuwa kila kofia ninayopewa ni chafu hadi zinatoa harufu,"anasema.

Mkazi wa Mtaa wa Nkuhungu jijini Dodoma, Zuhura Selemani, anasema: "Kuvaa kofia najisikia kinyaa, kwa sababu inavaliwa na watu wengi, kila mtu ana jasho lake, wengine vichwani wana upele, au ugonjwa wa ngozi, kwa kweli kwenye kofia waangalie utaratibu mwingine wa kutukinga na ajali."

**MADEREVA WA BODA**

Dereva wa pikipiki, Sulupice Lyatonga katika kituo cha bodaboda Swai jijini Dodoma, anakiri abiria wamekuwa wakigoma kuvaa kofia wanapopewa, akilalamika kuwa baadhi ya kofia zao ni chafu, kwa kuwa hawajui namna ya kuzisafisha.

"Kweli wanalalamika ni chafu lakini sisi hata hatujui tuzioshaje jamani, labda zitengenezwe ambazo zina kitu kwa ndani kuzuia uchafu,"anasema.

Emmanuel Shija, dereva kwenye kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, anasema kofia walizo nazo zipo chini ya ubora na kwamba baada ya mwezi mmoja huvunjika, huku zikiwa na uchafu ulionasa.

"Kofia ikioshwa si chini ya siku tatu ndio ikauke. Sasa hapo mtu hataweza kuvaa haijakauka na pia tunakosa hata huo muda wa kuzifua, kama kuna uwezekano abiria atembee na kofia yake,"anasema Shija.

Anaeleza kuwa kofia zenye kiwango cha chini bei yake ni kati ya Sh. 17,000 hadi 25,000 huku zenye kiwango bora inauzwa Sh. 60,000.

"Hata ajali zinapotokea huwasababishia madhara hasa kwa mtu ambaye hajavaa kofia ngumu kupona kwake na gharama za matibabu kubwa," anasema Shija.

Shija anaeleza kuwa kofia hizo zinaonyesha zimethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), lakini baada ya muda mfupi zinaharibika.

Dereva katika kijiwe cha Bihawana, jijini Dodoma, Godfrey Shirima, anaomnba litolewe tamko la kumtaka abiria ambaye kila siku anapanda usafiri huo awe na kofia yake na si mwendesha pikipiki kuwa na kofia mbili.

BINGWA WA NGOZI

Bingwa wa tiba ya magonjwa ya ngozi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk.Andrew Foyi, anasema kuna hatari ya kuambukizwa magonjwa ya ngozi na chawa, kwa kuwa kofia hizo zinatumiwa na watu tofauti.

"Kuna vimelea au wadudu kama chawa. Pia, mtu anapata mapunye, upele... akikataa kuvaa ni haki yake. Maana hata mimi nikipanda ukipewa hiyo kofia kuna harufu kali na uchafu huwa naogopa,"anasema Bingwa.

Anabainisha kuwa, binadamu hubeba chembe chembe za bakteria za aina mbalimbali kwa kuchangia vitu kama vile kofia, nguo, viatu na soksi kuna uwezekano wa kusambaza magonjwa.

"Kwa kweli kuna uhusiano wa kupata magonjwa ya ngozi, licha ya umuhimu wa matumizi ya kofia. Madereva wanatakiwa kujiwekea utaratibu ya kufanyia usafi kila baada ya siku moja, ili kuwaepusha abiria wao na hofu ya kupata magonjwa ya ngozi," anashauri binhgwa huyo.

Mtaalamu huyo anasema kofia hizo zinapaswa kusafishwa kwa maji ya moto, sabuni na dawa ya kuua vijidudu, kisha zianikwe

Huku akisisitiza hakuna haja ya kubadilisha kofia hizo kama baadhi ya waendesha pikipiki walivyoshauri, bali wanachopaswa kuzingatia usafi.

**MAELEZO YA TBS**

Ofisa Viwango Mwandamizi wa TBS, Yona Afrika, anasema kiwango kinachotumika kukagua kofia hizo anakitaja kwa jina ' TZS 1478 cha mwaka 2013', ambacho kimeweka matakwa ya viwango vya ubora wa kofia ngumu..

"Miongoni ni namna ya kuzuia mgongano, yaani mtu akigongana na kitu kigumu isipasuke, kuzuia kuchomwa na vitu vya ncha kali kufika kwenye kichwa cha binadamu," anasema.

Afrika anasema ndani ya kofia hizo, kuna muundo wake na plastiki maalum na kitambaa ambacho kinaongeza ulaini wa kuweza kukaa vizuri kwenye kichwa.

"Kile kitambaa cha ndani unaweza kufua kwa kutumia brashi laini na inatakata, hizi kofia huwa kuna mikanda ambayo inazuia mtu akipata ajali isidondoke na huwa kuna vipimo ambavyo vinatumika kupima kiwango cha kofia,"anasema.

Anaeleza kuwa kofia hizo zipo za aina mbili zinazokubalika hapa nchini ambayo ipo inayozunguka hadi kwenye kidevu(full helmet) na nyingine haifuniki kidevu, bali inafunika masikio(three quarter).



Kofia laini inayovaliwa na abiria wa pikipiki nchini Rwanda.

"Huwa inatokea kuna kofia hizi zipo chini ya viwango, kuna shehena kadhaa za 'helmet' zimekamatwa bandarini na zimeteketezwa,"anasema.

Anabainisha kuwa kofia ambazo zinapita katika utaratibu wa kawaida zinakaguliwa na zikiwa chini ya viwango zinachomwa moto au kurudishwa zilipotoka.

"Kuna kofia nyingine zinaingia kwa njia ya panya ambazo wakati mwingine ni changamoto kwa taasisi nyingi sana, lakini tunaendelea kukagua na kuchukua hatua kwa kofia feki tunazokutana nazo,"anasema.

**MAREKEBISHO SHERIA**

Mwanasheria wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Deus Sokoni, anasema serikali inatarajia kuifanyia marekebisho ya kukabili idadi kubwa ya ajali hizo.

Kwa mujibu wa gazeti la kila siku la 'The New Times' la nchini Rwanda, watumiaji pikipiki jijini Kigali nchini humo wamewekewa kofia laini(smart cover) ambazo zinafunika kichwa kwa ndani kabla ya kuvaa kofia ngumu ili kujikinga na magonjwa ya ngozi.

Hatua hii inaweza kuigwa na madereva au abiria wa pikipiki kwa kutembea na kofia hizo laini kama njia ya kuepuka magonjwa hayo na kuvaa kofia ngumu ili kuzuia madhara pindi ajali inapotokea.

Uvaaji wa kofia ngumu kwa abiria wa bodaboda ni muhimu kwa kuwa tafiti zinaonyesha zinaweza kuzuia majeraha makubwa kichwani pindi anapopata ajali.

> **"Kuna kofia nyingine zinaingia kwa njia ya panya ambazo wakati mwingine ni changamoto kwa taasisi nyingi sana, lakini tunaendelea kukagua na kuchukua hatua kwa kofia feki tunazokutana nazo,"anasema.**

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani(WHO), matumizi sahihi ya kofia ngumu yenye viwango hupunguza hatari ya majeraha kwa asilimia 42 na kwa kichwani kwa asilimia 69.

Hivyo, pamoja na kugoma kuvaa kwa madai ya kuambukizwa magonjwa ya ngozi, ni vyema sasa kila abiria na dereva akatembea na kofia laini kama ilivyo nchini Rwanda ambayo itamkinga na maambukizi hayo lakini pia itapunguza majeraha na vifo vinavyotokana na kutovaa 'Helmet'.

Asasi mbalimbali ikiwemo Mabalozi wa Usalama Barabarani(RSA),Chama cha Wanahabari Wanawake(Tamwa) na Chama cha Wanasheria Wanawake(TAWLA) pamoja na wadau wengine wamekuwa wakihimiza matumizi ya kofia ngumu ili kupunguza vifo vitokanavyo na ajali za barabarani.

## Makazi yenye miaka 9000 yagundulika Yerusalemu



Nchini Israel makazi ya kale yenye miaka zaidi ya 9,000 yamegunduliwa. **PICHA: MTANDAO.**

MAELFU ya vitu, vito vya thamani, mbegu na vifaa vya kilimo yamepatikana katika eneo la jadi la makazi yaliyodumu kwa miaka 9,000 nchini Israel.

Wana akiolojia wanaamini eneo hilo ambalo liko karibu na Motza, Magharibi mwa mji wa Jerusalem, wakati mmoja walikuwa wanaishi watu takribani 3,000.

Wachimbaji walipata mabaki ya jengo kubwa lenye vyumba kadhaa ambavyo watu walikuwa wakiishi wakati mmoja na kupata maeneo mengine ya matambiko yaliyokua yakitumiwa na wakazi hao.

Vitu vingine vilivyopatikana ni pamoja ncha ya mkuki uliyotumika kwa shughuli za uwindaji na pengine kujilinda. Bangili tofauti zilizotengenezwa kutokana na mawe pia zilipatikana. Zilikuwa ndogo zikiashiria kuwa zilikuwa zikivaliwa na watoto, watafiti wanasema.

Mamlaka ya Israel inayosimamia vitu vya kale inasema uvumbuzi huo utabadilisha mawazo ya wanahistoria wa kale katika eneo hilo ambalo liliaminiwa kuwa makazi ya Yudea enzi hizo.

Picha: Mamlaka ya Israel inayosimamia vitu vya kale.

***BBC***

AFYA

# Upi ukweli kuhusu vyakula, vichocheo vinavyoongeza hamasa tendo la ndoa?

**Na Mwandishi Wetu**



Pweza. **PICHA: MTANDAO**

UPUNGUFU wa nguvu za kiume ni jambo ambalo pengine haliwahusu kinababa wa Tanzania pekee, hali hiyo inawatatiza na watu wa mataifa mengine.

Tatizo hilo linaendelea kupatiwa majibu na eneo mojawapo ni vyakula gani vinavyoweza kuimarisha tendo la kujamiina?

Ukweli ni kwamba kama kungekuwa na ushahidi kwamba chakula cha aina moja kinaweza kuimarisha tendo la ndoa na kukuzidishia hamu ya kujamiiana, huenda kungekuwa na uhaba mkubwa wa chakula hicho.

Lishe bora, kufanya mazoezi na afya ya akili yote yanaweza kuimarisha tendo la ndoa. Lakini kuna vyakula maalum vinavyoweza kukuongezea shauku ya kufanya hivyo?

Viungo vinavyoweza kuchochea hisia ya furaha- kutokana na homoni ya endorphins, vina virutubisho vinavyohusishwa na kuimarika kwa tendo la ndoa, au kwa jumla vinahusishwa na utajiri na ufanisi na mara nyingi hutajwa kuwa vichochezi vya kuimarisha tendo hilo la kujamiiana.

Ni vyema kutizama historia na sayansi iliyomo kwenye fikra hizi na tutafakari kuhusu vyakula vinaweza kweli kuimarisha tendo la ndoa.

Hata hivyo, hakuna uthibitisho baina ya kula chaza na kuongezeka kwa hamu ya kufanya tendo la ndoa, lakini cha kujiuliza ni hiki uvumi ulitoka wapi?

**BAHARI NA NGONO**

Simulizi au ngano za kale zinaeleza kwamba wakati Aphrodite - mungu wa tendo la mapenzi alipozaliwa kutoka povu jeupe na kufufuka kutoka baharini ndipo chakula cha baharini kilipoonekana kuwa ni kichochezi cha kuimarisha hamu ya tendo la ndoa.

Lakini kuna habari nzuri kwa wanaopenda kula chaza, inaelezwa kuwa wana madini ya zinc ambacho ni kirutubisho muhimu kinachotumika kutengeneza homoni ya 'testosterone.'

Utafiti umebaini kwamba zinc inaweza kusaidia kutibu matatizo ya wanaume kuzalisha na huenda zinaweza kuongeza ubora wa manii (mbegu za kiume).

Vyanzo vingine vya zinc hupatikana katika nyama nyekundu, mbegu kama za tango na ufuta, korosho na lozi lakini pia maziwa na hata jibini.

**CHOKOLETI INAHUSIKA**

Kula chokoleti nyeusi kunaweza kumpa mtu hisia ya awali unapompenda mtu, kwa mujibu wa utafiti, kwa sababu ina 'kemikali ya mapenzi' phenylethylamine (PEA).

PEA, ambayo huwapo katika miezi ya kwanza ya mahusiano huchangia kuwapo kwa homoni inayomfanya mtu kujihisi vizuri na kuchochea raha katikati ya ubongo.

> **Utafiti umebaini kwamba zinc inaweza kusaidia kutibu matatizo ya wanaume kuzalisha na huenda zinaweza kuongeza ubora wa manii (mbegu za kiume).**

Ni kiwango kidogo cha PEA kipo katika chokoleti na kuna shaka iwapo kiwango hicho kinaendelea kuwapo wakati kinaliwa.

Cocoa pia ina 'amino acid tryptophan,' na husemekana kuongeza msukumo wa damu na viwango vya serotonin (homoni nyingine ya furaha).

Basi uhusiano baina chokoleti na tendo la ndoa ulianza vipi? Huenda ni katika karne ya 16.

Hernán Cortés alikuwa mtawala wa Kihspania katika karne hiyo aliyeidhibiti inayojulikana hii leo kama Mexico chini ya ufalme wa Castile.

Inadhaniwa ndiye raia wa kwanza Ulaya kugundua chokoleti. Alimuandikia barua mfalme akimueleza kwamba amegundua kinywaji cha kokoa kinasaidia "kuimarisha kinga na kukabiliana na uchofu".

Lakini raia wa zamani wa Castile huenda walihusisha nguvu hizo na chokoletina hakuna uhakikisho kuunga mkono ushahidi wa kuimarisha tendo la ngono.

**PILIPILI VIPI**

Swali jingine ni hili pilipili huchangamsha tendo la ndoa? Hizi zina kitu kinachojulikana kama 'capsaicin,' ambayo utafati umeainisha kuwa inaweza kuchochea homoni ya endorphins (ya kujihisi furaha).

Husaidia pia kuharakisha ufanyaji kazi mfumo wa kusaga chakula tumboni na huongeza ujoto mwilini na kasi ya moyo unavyopiga, mambo ambayo huwa wanadamu wanayahisi wakati wa tendo la ndoa. Lakini ni lazima kuhakikisha kwamba unakumbuka kuosha mkono unapotayarisha pilipili.

**POMBE**

Watu wanaamini pombe hasa kali kama konyagi inahusika, hivi pombe husaidia au hutatiza?

Pombe inaweza kuongeza hamu kwa kuondosha kujizuia, lakini kama anavyoeleza Macbeth wakati akiwa amelewa, "huchochea hamu, lakini huondosha uwezo".

Hisia hupungua kwa wanaume na wanawake kwa kunywa pombe nyingi, na katika kipindi cha muda mrefu inaweza kupunguza uwezo wako wa kushiriki tendo la ndoa na hata mara nyingine katika hali mbaya zaidi kuchangia matatizo ya kushindwa kabisa kushiriki tendo hilo. Zaidi ya hapo harufu ya pombe haivutii!

**VICHOCHEO**

Vichocheo vya kuongeza hamu ya kujamiina vinaweza kugawanywa katika makundi matatu.

Vinavyoshughulikia hamu, uwezo wa kushiriki tendo na raha inayotokana na tendo lenyewe.

Hakuna vilivyothibitishwa kisayansi kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa binaadamu, kutokana na ugumu wa kupima ufanisi

Ni harufu ya kuiva na kuoza kwa tunda pekee ndiyo iliyoweza kuthibitishwa, na hufanya kazi kwa wadudu wa matunda wanaoruka.

Dk Krychman, mtaalamu wa afya ya ngono anasema anadhani watu hula vichochezi hivyo kwasababu ya imani kwamba vitafanya kazi, na anauliza iwapo jambo linakusaidia, je unajali kwanini inafanya kazi? Vichochezi vingi huwa ni vinywaji, lakini imeshauriwa kuepuka dawa zinazotokana na mimea iwapo hazina taarifa ya usalama au yoyote inayotajwa kuwa ya miujiza.

**MATATIZO YALIYOPO**

Iwapo hamu ya tendo la ndoa imepungua, huenda una tatizo la afya , kwa hivyo daima mshauri daktari, wala si kukimbilia kula dawa za mitaani au vichocheo unavyovisikia kwa wengine. ***BBC.***

MAZINGIRA



# Hawa ni miongoni mwa maelfu wanaoangamia, yumo kakakuona

Na Mwandishi Wetu

UKATAJI wa misitu, uchafuzi wa mazingira baharini na nchi kavu, kuchafua maji na hali ya hewa ni baadhi ya mambo yanayotishia kuangamiza mazingira asilia duniani.

Hili ni onyo lililotolewa hivi karibuni na zaidi ya wataalamu 500 kutoka mataifa 50 katika ripoti yao inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN).

Sambamba na hilo aina zaidi ya 100,000 za viumbe zinazoelekea kuangamia zainishwa kuna gorilla, ndege mimea na hata kakakuona.

Ripoti hiyo iliangazia uharibifu unaokumba mazigira asilia duniani katika kipindi cha miaka 50 na jinsi maisha ya baadaye ya mamia ya viumbe yalivyo hatarini.

Ripoti hiyo pia inatoa mwongozo wa dharura wa hatua za kuchukuliwa kuokoa mazingira

Kwa hivyo ni vyema watu wakajiuliza wanafahamu nini kuhusu mazingira na afya ya viumbe kadhaa vinavyoishi duniani?

Mazingira asilia yanakabiliwa na tishio la kuangamizwa. Kutathmini orodha ya IUCN ya viumbe hai wanaokabiliwa na tishio la kuangamia ni hatua muhimu katika suala la uhifadhi mazingira.

**MAANGAMIZO**

Karibu viumbe hai 100,000 wamechunguzwa na imebainika kuwa kufikia sasa kubaini ni wapi wanakabiliwa na tishio la kuangamia.

Kati ya hao zaidi ya robo au 25,000 wanakabiliwa na tishio la kuangamia, miongoni mwa chura wa kipekee wanaopatikana Madagascar anayefahamika kama 'salamanders', na mimea kama vile conifers na orchids.

Uchunguzi haujakamilika lakini mpaka sasa hatuna idadi kamili ya viumbe hai vilivyopo duniani.

Inakadiriwa kuwa viumbe hai hivyo ni kati ya milioni mbili hadi trillioni moja, lakini wataalamu wengi wanasema ni karibu milioni 11 au chini ya hapo.

Wanasayansi wanaamini kuwa dunia inakabiliwa na tishio la kuangamia katika miaka kadhaa ijayo.

"Sasa kuna ushahidi wa kutosha kuwa ulimwengu unapoteza viumbe hai kwa kiwango kikubwa," Prof Alexandre Antonelli, Mkurugenzi wa Sayansi katika bustani la Royal Botani, Kew, aliiambia BBC.

Mara ya mwisho hali kama hiyo ilishuhudiwa karibu miaka milioni 66, ilisababishwa na asteroid kugonga dunia, alisema kuwa sasa hivi hali hiyo inachangiwa na binadamu.

Viwango vya uharibifu sasa ni karibu mara 1,000 zaidi ya ilivyokua kabla wanadamu kuingilia kati na kuongeza uharibifu kwa zidi ya mara 10,000.

> **"Sasa kuna ushahidi wa kutosha kuwa ulimwengu unapoteza viumbe hai kwa kiwango kikubwa," Prof Alexandre Antonelli, Mkurugenzi wa Sayansi katika bustani la Royal Botani, Kew, aliiambia BBC.**

**TABIANCHI**

Miongoni mwa vitu vinachangia uharibifu wa mazingira ni mabadiliko ya hali ya hewa

Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni mabadiliko ya hali ya hewa bado ni tisho kubwa katika uhifadhi wa mazingira.

Vitu vingine vinavyochangia uharibifu huo ni kupotea kwa mazingira asilia kutokana na kilimo,ufugaji, uchongaji mbao, uwindaji, uvuvi, na shughuli za uchimbaji madini .

Wanyama kama vile kakakuona (pangolin) wanakabiliwa na tishio la kuangamia kutokana na uwindaji haramu.

Ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza mbao umechangia kupungua kwa idadi ya tumbili wakipekee nchini Myanmar.

Kuongezeka kwa shughuli ya kilimo pia kumetajwa kuwa sababu ya baadhi ya wanyama kama vile chui kutoweka.

"Serikali zimejikita zaidi katika suala la mabadiliko ya tabia nchi na kusahau kuangazia uharibifu wa mali asilia unaotokana na uharibifu wa ardhi, Mwenyekiti wa Jukwaa la Intergovernmental science-policy Platform on Biodiversity and Ecosystem Services 'IPBES', Prof Sir Bob Watson, aliiambia BBC.

"Vyote vitatu ni muhimu kwa afya ya binadamu."

**MABILIONI WAATHIRIKA**

Wanyama na mimea wanaangamia kadri makazi asilia yanavyoharibiwa. Uharibifu kutokana na shuguli za binadamu umeathiri karibu watu bilioni 3.2 hali ambayo pia ina athari kwa mazingira duniani, kwa mujibu wa IPBES.

Hali ambayo imechangiwa zaidi na ukulima usiyokuwa na tija na uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na katika baadhi ya sehemu, upanuzi wa makaazi katika maeneo ya mijini, ujenzi wa barabara na uchimbaji madini.

Uharibifu wa ardhi unatokana na ukataji wa misitu, huku kimataifa hali hiyo ikidhibitiwa kupitia upandaji wa miti.

Karibu hekari milioni 12 ya misitu duniani katika maeneo ya tropiki yaliangamia mwaka 2018, hii ikiwa ni karibu viwanja 30 vya mpira vinavyoharibiwa kila dakika kwa mujibu wa ripoti ya hivi karibuni.

**MAKAZI ASILIA**

Kwa mujibu wa IPBES, ni robo tu ya ardhi duniani ambayo haijaathiriwa na shughuli za binadamu.

Hali hii inatarajiwa kuimarika kwa kiwango kidogo ifikapo mwaka 2050.

"Suala la matumizi ni changamoto kubwa ya uhifadhi wa mazingira tunalokabiliana nalo," Prof Mercedes Bustamante wa Chuo kikuu cha Brasilia anaiambia BBC.

Tangu mwaka 2001, Indonesia imepoteza mamilioni ya hekari ya misitu ya mvua lakini hali hiyo ilibadilika mwaka 2018 uharibifu huo ulipungua kwa asilimia 40.

Hii ni kutokana na sheria kali zilizobuniwa na serikali kuhakikisha misitu inalindwa dhidi ya moto.

Katika maeneo ya kusini mashariki ya Asia misitu katika nyanda za chini ya visiwa vya Borneo na Sumatra, IPBES inakadiria kuwa aina tatu ya ndege na karibu robo ya wanyama wataangamia ikiwa uharibifu wa misitu utaendelea.

**MISITU YATOWEKA**

Baadhi ya misitu mikubwa duniani inatoweka na eneo la Amazon linalofahamika kwa kuwa na misitu ya tropiki ambayo ina mimea na wanyama wapya wanaogunduliwa kila mwaka ina hatari kubwa.

Rondônia, iliyopo magharibi mwa Amazon, ni moja ya sehemu zilizoharibiwa sana katika eneo hilo.

Miti inakatwa ili kufanya shughuli za kilimo, kutengeneza mbao, kufanya shughuli za kuchimba madini au kulisha mifugo.

Kadri muda unavyosonga ndivyo misitu inavyoharibiwa na maeneo hayo kugeuzwa kuwa makazi ya watu.

*BBC*

AFYA



Vinywaji mbalimbali vya sukari vinahofiwa kusababisha saratani. Unakunywa kiasi gani? Tafakari matumizi yako. **PICHA: MTANDAO.**

KITISHO SARATANI

# Vinywaji vyenye sukari vinaleta saratani?

## Juisi za matunda zisizoongezwa chochote zimo

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI hii, Rais John Magufuli, akiwa mkoani Mwanza, ameeleza kushtushwa na ongezeko la saratani kanda ya ziwa na kuagiza utafiti wa kina ufanyike kuujua ukweli wa mambo.

Kwenye mikoa hiyo, taarifa za kitabibu zinasema kuwa asilimia 50 ya wagonjwa wenye maradhi hayo wanatoka mikoa ya ukanda huo, jambo ambalo anasema linahitaji kufanyiwa uchunguzi na hatua kuchukuliwa ili kuwaokoa watu na maangamizo.

Wakati hayo yakijiri hapa nchini, mwishoni mwa wiki iliyopita, watafiti wa afya nchini Ufaransa nao wanaguswa na suala la ongezeko la saratani wakitafiti na kuibuka na unywaji vimiminika vyenye sukari.

Wanasema vinywaji vya sukari ikiwamo juisi ya matunda vinaweza kuongeza hatari ya kupata saratani. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na mwanasayansi wa Ufaransa.

Anabainisha kuwa uhusiano huo ulifichuliwa na utafiti uliochapishwa katika jarida la matibabu nchini Uingereza uliowachunguza watu 100,000 kwa kipindi cha miaka mitano.

Wanasayansi hao kutoka Chuo Kikuu cha Sorbonne Paris Cite wanadai kwamba ongezeko la viwango vya sukari katika damu huenda ndiyo sababu kuu ya ongezeko la saratani.

Hata hivyo, utafiti huo haukupata ushahidi kamili na wa kuridhisha kuhusu hofu hiyo na kwamba watafiti wametaka uchunguzi zaidi kufanywa.

**VINYWAJI NI VIPI**

Swali ambalo wengi wanajaiuliza ni hili je ni nini kinachohesabika kama kinywaji cha sukari?

Watafiti wao wakijibu wanasema kwamba ni kinywaji kilicho na zaidi ya asilimia tano (5) ya sukari. Vinywaji hivyo ni pamoja na maji ya matunda ambayo hayajongezwa sukari.

Hizo ni kama juisi za maembe, matikiti, mapapai, machungwa na pesheni.

Vinywaji visivyo na pombe na vile vya kuongeza nguvu, chai na kahawa yenye sukari, pia vinahusika.

Kundi hilo pia lilichunguza vinywaji visivyo na kalori vinywaji vilivyo na sukari yake ya asili lakini hawakubaini uhusiano wowote na saratani.



**KIWANGO CHA ATHARI**

Je hatari ya saratani ni ya kiwango gani? Ni swali lililohitaji maelezo. Utafiti huo pia ulifichua kwamba unywaji wa mililita 100 za ziada za vinywaji vilivyo na sukari kwa siku ikiwa ni chupa mbili kwa wiki kutaongeza hatari ya saratani kwa asilimia 18.

Kwa kila watu 100 katika utafiti huo kuna 22 walio na saratani.

Hivyo basi iwapo wote watakunywa mililita 100 kwa siku itasababisha aina nyingine nne za saratani na kuongeza jumla hiyo kufikia watu 26 kwa 1,000 katika kipindi cha miaka mitano, kulingana na maelezo ya watafiti hao.

Kati ya visa 2,193 vilivyopatikana wakati wa utafiti huo aina ya saratani 693 zilikuwa zile za matiti , 291 zilikuwa za tezi dume na visa 166 vilikuwa vile vya saratani ya mwisho wa utumbo.

Walieleza kuwa jinsi utafiti huyo ulivyofanyika inamaanisha unaweza kupata mifano katika data lakini hauwezi kuielezea.

Hivyo basi kwa mujibu wa wachambuzi ulionyesha watu waliokunywa sana takriban mililita 185 kwa siku walikuwa na visa vingi vya saratani ikilinganishwa na wale waliokunywa chini ya mililita 30 kwa siku.

Na maelezo yanasema kuwa vinywaji vya sukari vinasababisha saratani.

Lakini pia watu wanaobugia vinywaji vya sukari wanaweza kuwa na matatizo mengine ya kiafya.

Kwa msingi wa utafiti huo hauwezi kusema kwamba vinywaji vya sukari ndiyo chanzo cha saratani na kwamba kupuguza kiwango cha sukari katika chakula ni muhimu sana.

Huku utafiti huo ukishindwa kutoa ushahidi kamili kuhusu sukari na saratani, unaonyesha kuwa na mpango wa kupunguza kiwango cha sukari , anasema Dk Amelia Lake kutoka chuo kikuu cha Teesside.

UNENE KUPINDUKIA

Je tatizo hilo linahusishwa na kunenepa kupitia kiasi? Unene kupindukia ni sababu moja inayosababisha saratani na matumizi ya juu ya vinywaji vya sukari husababisha mtu kunenepa mno. Hata hivyo, utafiti huo unasema si visa vyote.

Kunenepa kupitia kiasi kunakosababishwa na kunywa vinywaji vingi vya sukari huhusishwa lakini hawakuelezea uhusiano wote kwa kina.

Dokta Mathilde Touvier mmoja wa watafiti hao alliambia BBC.

**WAZALISHAJI**

Je watengenezaji wa vinywaji vya sukari wanajiteteaje? Muungano wa watengenezaji vinywaji visivyo na pombe nchini Uingereza wanasema kuwa utafiti huo hautoi ushahidi. Mkurugenzi Mkuu Gavin Prtington, anaongeza : "Vinywaji vyetu ni salama na ni miongoni mwa vitu vyenye lishe bora."

Sekta ya utengenezaji wa vinywaji hivi ina jukumu katika kusaidia kukabiliana na kunenepa kupitia kiasi na ndio sababu wamepunguza kiwango cha sukari na kalori.

*BBC*





# Wenye ulemavu walalamika usimamizi mbovu sheria

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATU wenye ulemavu mkoani Mbeya wamelalamikia usimamizi mbovu wa baadhi ya sheria na miongozo iliyowekwa na serikali kwa madai kuwa imeshindwa kutekeleza haki za watu hao na kusababisha kutoshiriki ipasavyo kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo Jiji la Mbeya, Damas Mwambenje, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe jinsi watu wenye ulemavu wanavyoshiriki kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi ikiwamo vikao, pia kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwambenje alisema serikali imejitahidi kutunga na kuandaa sheria nzuri zinazomlinda mtu mwenye ulemavu, lakini changamoto ni usimamizi mbovu na utekelezaji mdogo wa viongozi waliopewa dhamana ya kutekeleza sheria hiyo hali inayosababisha kundi hilo kutoshirikishwa katika ngazi za maamuzi ikiwamo serikali za kijiji, kata, wilaya na mkoa.

Alisema baadhi ya viongozi wameshindwa kutekeleza sheria zinazomlinda mwenye ulemavu na kutoa mfano kuwa tangu kuanzishwa kwa Baraza la Mkoa mwaka jana, hakuna kikao kilichokaa ili kuwasilisha changamoto zinazowakabili wenye ulemavu.

"Sheria na miongozo ya kuwalinda na kuwatetea watu wenye ulemavu zipo na zimeelezwa vizuri, lakini changamoto iliyopo ni utekelezaji wake kuwa mdogo, wengi hawashirikishwi kwenye mikutano ya mitaa," alisema Mwambenje.

Aliiomba serikali na jamii kulithamini kundi hilo kwa kutengeneza mazingira wezeshi ikiwamo miundombinu ya taasisi za umma na utoaji wa taarifa kutoka kwa viongozi kuanzia ngazi ya mitaa, kijiji na kata ili kushiriki na kuwasilisha maoni au changamoto zinazowakabili.

Kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, Mwambenje alisema hadi sasa hakuna maandalizi yoyote kwa watu wenye ulemavu katika kushiriki uchaguzi.

Alisema wanasubiri utaratibu wa viongozi endapo watashirikishwa na kushauri kutengenezwa kwa miundombinu rafiki maeneo ya kupigia kura ili kuwawezesha wenye ulemavu kutumia haki yao ya kikatiba.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Uzunguni B jijini Mbeya, Uswege Luhanga, alidai mtaa wake umejitahidi kuwashirikisha watu wenye ulemavu kushiriki katika ngazi mbalimbali za uamuzi.

Alisema watu wao ni chachu kubwa katika kushauri na kujitokeza kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha, linalosaidia kuchagiza jitihada za serikali kusaidia jamii, Festo Sikagonamo, alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha watu wenye ulemavu kutoshiriki kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi ni kuendelea kudumisha mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Alisema mila na desturi hizo zinasababishwa na imani zilizojengeka katika jamii kuwa kuzaa mtoto mwenye ulemavu ni mkosi hivyo hufichwa ndani hadi wanapokua na kuzeeka, pia mitizamo ya watu kuwa wenye ulemavu hawawezi kuongoza kwa sababu ya hali walizonazo.

"Matokeo ya kutowashirikisha wenye ulemavu ndiyo haya tunayaona sasa vingi vilivyofanyika ikiwamo miundombinu ya kutolea huduma kama benki, shule havikuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu," alisema Sikagonamo.



Mmoja wa wafanyakazi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, akimwagilia moja ya mashamba darasa ya kilimo bora cha viazi mviringo yaliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walimu 9 wapewa mil. 14/- kwa kufaulisha vizuri

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WALIMU tisa wanaofundisha kidato cha sita Shule ya Sekondari Ivumwe inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mbeya, wamepewa motisha ya Sh. milioni 14.7 na uongozi wa shule baada ya wanafunzi 186 wa kidato cha sita kufanya vizuri na kupata daraja la kwanza na la pili.

Shule ya Sekondari Ivumwe imekuwa na mwendelezo mzuri wa matokeo ya kidato cha sita na ikizitoa kimasomaso baadhi ya shule zinazomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM, Mkoa wa Mbeya na sehemu nyingine nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, juzi alihudhuria hafla ya kuwapongeza walimu wa Shule ya Sekondari Ivumwe, ambao walifanya vizuri katika matokeo ya kidato cha sita.

Chalamila alisema aliwakabidhi kiasi cha Sh. milioni 14.7 walimu wa Shule ya Ivumwe kwa matokeo mazuri na kuahidi kuongeza dau la zawadi kwa matokeo yajayo.

"Sekondari ya Ivumwe ni shule unayoweza kuidharau kwa kuiangalia kwa sababu sio maarufu sana, lakini ina siri kubwa wanafunzi wengi wanaosoma hapo wanafanya vizuri hii ni kwa sababu ya mshikamano walionao walimu kwa kushirikiana na mkuu wao, lakini pia wanafunzi kukubali kujifunza," alisema Chalamila.

Alisema kiasi hicho cha fedha kilichotolewa na uongozi wa shule kama motisha kwa walimu kiwe chachu kwao na shule nyingine zinazomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM mkoani Mbeya katika Shule ya Sekondari Meta, Sangu na Mporoto.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya ambaye pia ni Mjumbe wa Baraza la Wazazi Taifa Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, alisema shule hiyo imewatoa kimasomaso Jumuiya ya Wazazi na kushauri chama kiweke nguvu zaidi ili kuendelea na matokeo mazuri shuleni hapo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Ivumwe, Emily Muhondwa, alisema motisha zinazotolewa kwa walimu zimekuwa zikichangia matokeo mazuri na lengo la shule ni kufuta daraja la tatu.

Muhondwa alisema shule yake katika matokeo ya kidato cha sita ambayo yametangazwa hivi karibuni imeshika nafasi ya pili kimkoa na kitaifa nafasi ya 60 kati ya shule 595.

## Takukuru yafuatilia matumizi miradi ya maendeleo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mbeya, imefuatilia matumizi ya fedha na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 14.5 kwa lengo la kujiridhisha iwapo miradi inatekelezwa kwa ubora na thamani halisi ya fedha.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema katika kipindi cha robo ya mwaka kuanzia Mwezi Aprili hadi Juni, mwaka huu, taasisi hiyo ilikagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya maji, ujenzi, elimu na afya.


Alisema ukaguzi huo ulisaidia kubaini kasoro ndogondogo katika utekelezaji wa miradi ikiwamo ucheleweshaji wa kumalizana kutoa ushauri ili kuepuka kasoro nyingine zisijitokeze.

"Mbali na kufanya ukaguzi wa miradi pia taasisi hii imewaelimisha wataalamu wa halmashauri wanaohusika katika ujenzi wa miradi kuwa kila mmoja anapaswa kujitambua na kutoa mchango wake ipasavyo katika kuisaidia jamii badala ya kuacha mambo yaharibike," alisema Julieth.

Alisema wataendelea kutoa elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa kwenye taasisi za umma na binafsi ili kila mmoja atambue wajibu wake na awe balozi katika kupinga rushwa.

Alisema katika kipindi cha robo ya mwaka kilichoishia mwezi Juni, walitoa elimu kwa wananchi 19,171 kupitia semina 37 kwa watumishi 2,046 wa taasisi mbalimbali za umma na binafsi, pia waliimarisha vilabu vya wapinga rushwa katika shule za sekondari na msingi 151.

Vile vile katika robo ya mwaka ijayo ambayo imeanza mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu wamejipanga kuendelea kuelimisha wananchi kufanya uchaguzi kwa uhuru na haki na kuwashtaki mahakamani wote watakaokutwa na tuhuma za vitendo vya rushwa.





# Soko la zabibu laliza wakulima

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UMOJA wa Wakulima wa Zabibu (Uwazamaha) wameomba kuundwa kwa bodi ya zao hilo ili kusaidia changamoto ya masoko.

Ombi hilo lilitolewa jana na mwenyekiti wa umoja huo, Saratiel Wiliam, wakati wa mkutano wao na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, uliofanyika katika Kijiji cha Hombolo.

Alisema zao hilo kila mwaka limekuwa likikumbwa na changamoto ya kukosa soko la uhakika, hali inayowakatisha tamaa wakulima.

"Wakulima tuna changamoto ya soko la uhakika kila mwaka Mkuu wa Wilaya, tunaomba kuundwa kwa bodi ya zao la zabibu ili itusadie kuondokana na changamoto hii ya soko ambayo imekuwa ikijitokeza kila msimu wa mavuno ya zabibu," alishauri.

Alisema wanaamini kuundwa kwa bodi hiyo kutasaidia kutafuta masoko na wawekezaji wa ndani ya nje ili kuepuka hasara ambayo imeanza kuwakatisha tamaa wakulima wa zao hilo.

Aliongeza kuwa wawekezaji wanaonunua zao hilo kwa sasa nchini, hawana uwezo wa kununua zabibu zote zinazozalishwa katika mkoa huo.

Julius Sombe, mkulima wa zabibu mkoani Dodoma, aliiomba serikali kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kununua mashine za kukamua mchuzi wa zabibu.

Sombe alisema mchuzi huo unaweza kuhifadhiwa kwa zaidi ya miaka 10 bila kuharibika na anaamini utaratibu huo utamsaidia mkulima kuuza zao hilo nje ya nchi kwa muda anaotaka.

"Tumekuwa na changamoto ya bei ya zabibu, mwaka jana tuliuza kilo moja Sh. 1,200 na wanunuzi walikuwa wanatukopa, unakuta unamdai Sh. milioni 10, lakini mnunuzi anakulipa fedha kidogo kidogo, unakuwa huoni faida ya kilimo," alisema.

Katambi aliwaomba wakulima hao kuwa na uvumilivu kutokana na wanunuzi kuiahidi serikali kuwa watanunua zabibu zote. Alisema wenye viwanda vya zabibu wanahitaji kiwango cha sukari kiwe juu, hivyo wametuma wataalamu wao kupima kiwango hicho.

Katambi alisema serikali itaendelea kuwaita wawekezaji zaidi ili kusaidia kuwekeza viwanda zaidi vya zabibu na kuwasaidia kutafuta soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Alisema ili kuwavutia wawekezaji, serikali imepunguza kodi ya mchuzi wa zabibu ili kuwavutia wawekezaji zaidi kwenye biashara hiyo.

# Machinga walilalamikia jiji kuwaondoa ofisi za CCM

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndogo, maarufu machinga, waliokuwa wanafanya biashara nje ya uzio wa ofisi za makao makuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma, wameulalamikia uongozi wa jiji hilo kwa kuwavunjia vibanda vyao pasi na kupewa taarifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, mwenyekiti wa wamachinga hao, Inocent Mushi, alisema walikuwa wakifanya biashara kwenye eneo hilo kwa muda mrefu, lakini jiji limeamua kuwaondoa kwa kuvunja vibanda vyao.

"Sisi hatupingi kuondoka hapa ila tunacholalamika ni kuharibiwa mali zetu, wangetupa taarifa, tungetoa mali zetu kuliko hasara tuliyopata," alisema.

Mushi alibainisha kuwa machinga 65 walikuwa wanafanya biashara katika eneo hilo na walifuata utaratibu kwa kuuomba uongozi wa CCM na uliwaruhusu kufanya biashara nje ya eneo lao kwa masharti waliojiwekea.

Aliyataja baadhi ya masharti hayo kuwa kutakiwa kuacha nafasi ya barabara kuu na kutoziba mageti ya kuingilia ndani ya ofisi za makao makuu ya chama hicho.

"Sasa tunashangaa jana (juzi) askari wa jiji walifika katika eneo la biashara majira ya saa tano usiku kuanza kuvunja vibanda vyetu bila taarifa ya kuondoa bidhaa zetu, jambo ambalo limesababisha hasara kubwa," alisema.

Alidai wamachinga wote waliokuwa wanafanyabiashara kwenye eneo hilo, walikuwa na vitambulisho vilivyotolewa na Rais John Magufuli kwa ajili ya wajasiriamali na watoa huduma wadogo.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema uongozi wa Jiji utawatafuta eneo lingine la biashara kwa ajili ya wafanyabiashara hao.

"Eneo hili siyo salama sana kutokana na kuwa karibu sana na barabara kuu, jambo ambalo linaweza kusababisha ajali," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, akiangalia mkungu wa zabibu, alipotembelea moja ya shamba la wakulima katika Kijiji cha Hombolo, Wilaya ya Dodoma, mkoani Dodoma jana, wakulima hao wamedai kukabiliwa na changamoto ya soko la uhakika la zao lao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wahandisi Ruwasa wapewa angalizo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka wahandisi wa mikoa na wilaya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kuhakikisha hawakwamishi jitihada za upelekaji wa huduma za maji vijijini.

Aweso alitoa rai hiyo jana jijini hapa katika kikao cha menejimenti wa wakala huo wa mikoa na wilaya nchini kilicholenga kujadili uendeshaji wa sekta ya maji.

Alisema watendaji waliopata nafasi hizo wanapaswa kufanya kazi kwa ufanisi ili kuhakikisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini inafikia asilimia 85 au zaidi ifikapo mwakani.

"Najua mliopata nafasi za uongozi mmekutana na changamoto nyingi, nendeni mkazitendee haki nafasi zenu ili kuiboresha sekta ya maji vijijini," Aweso alisema.

Naibu Waziri huyo, alisema umebaki mwaka mmoja wa fedha ili kufikia malengo yao, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano katika kutimiza azma ya serikali katika sekta ya maji.

"Kuna baadhi ya wataalamu wameiangusha sana sekta ya maji kutokana na kwamba imekuwa desturi yao kuona miradi ya maji ni sehemu ya kujipatia fedha kwa kuwa tenda zao walipewa kirahisi kirahisi, lakini awamu hii hakuna urahisi kwenye kazi unayokabidhiwa," alisema.


Alibainisha miradi mingi wanashindwa kuimaliza kwa wakati licha ya serikali kutoa fedha nyingi.

"Hii ni kutokana na uzembe wao, miradi hiyo inachelewa kukamilika au ikikamilika inashindwa kutoa huduma ya maji, hatutakuwa tayari kuwavumilia makandarasi wa aina hiyo," alisema.

Aweso alisema makandarasi wasiofanya kazi vizuri, majina yao yatawekwa wazi ili kuhakikisha ndani ya wakala hawapati nafasi ya kutekeleza miradi.

"Sisi serikali tunaamini Ruwasa itakuwa mwarobaini wa changamoto zote za miradi ya maji na walioharibu miradi wakibainika, serikali haitasita kuwachukulia hatua," alisema.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema lengo la serikali ni kuona Watanzania wote wanapata maji safi na salama kwa kuwa huduma hiyo ni haki yao.






Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akimkabidhi zawadi ya kompyuta mpakato mwanafunzi bora wa sayansi kidato cha sita, Wahda Mbarak, wa Shule ya Feza Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Eneo jipya la maziko lasimamishwa

**Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema eneo jipya lililotengwa kwa ajili ya kuzika watu halitoanza kutumika mpaka mgogoro wa ardhi uliojitokeza umalizike kati ya wamiliki waliojitokeza na serikali Visiwani Zanzibar.

Msimamo huo umetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mohamed Aboud, alipokuwa akizungumzia mgogoro wa ardhi wa eneo

hilo baada ya linalotumika la Mwanakwerekwe kujaa.

Alisema tayari Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, ameagiza watu wanaodai kumiliki eneo hilo wakae pamoja na serikali kutafuta ufumbuzi kabla ya kuanza kutumika.

"Serikali imewataka walalamikaji kuwasilisha vielelezo vya ushahidi zikiwamo nyaraka za hati miliki ili serikali ijiridhishe, lakini haiwezi kuruhusu watu kuanza kuzika katika eneo la Kama kabla ya kupatikana makubaliano na wahusika," alisema Waziri Aboud.

Alisema kama wahusika watathibitisha kwa vielelezo upande wa serikali upo tayari kufanya mazungumzo ya kuwalipa fidia kwa kutumia utaratibu wa kisheria, lakini kama watagoma ipo tayari kutafuta eneo lingine," alisema Waziri Aboud.

Alisema mawasiliano na wahusika yameanza kufanyika.

Akizungumza kwa niaba ya wanafamilia ya wamiliki wa eneo hilo, Qussay Juma Mugher, alisema mgogoro wa ardhi katika eneo hilo umeanza

kujitokeza mwaka 2002 baada ya sehemu ya ardhi kuvamiwa na Jeshi la

Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) na malalamiko kuwasilishwa Ofisi ya Katibu Mtendaji, Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Zanzibar.

Qussay alisema kwa mujibu wa nyaraka za serikali kabla ya Mapinduzi na baada, babu yake Marehemu Sultan Ahmed Mugheiry, alianza kumili eneo hilo la ardhi lenye ukubwa wa karibu heka 70 mwaka 1932 kabla ya kumilikiwa na watoto wake kufariki kwa kuuawa kwa kuchomwa visu na wapinga harakati za ukombozi wa Waafrika Zanzibar.

Vile vile alisema: "Baada ya kutokea ajali ya MV Spice Islander mwaka 2011, serikali ilichukua sehemu ya ardhi na kutumika kuzika watu waliokosa kutambuliwa na ndugu na jamaa bila ya wahusika kushirikishwa, lakini tulikubali bila kinyongo," alisema.

Hata hivyo, alisema msimamo wa wanafamilia ni kuwa hawataki sehemu ya shamba lao kugeuzwa sehemu ya kuzikia, wanachotaka serikali irejeshe eneo lao pamoja na ardhi iliyochukuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar.

# Saud Arabia yakabidhi tani 100 za tende

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

SERIKALI ya Saud Arabia imeikabidhi msaada wa tende tani 100 Serikali ya Zanzibr kwa ajili ya kuwapatia wananchi mbalimbali wa Zanzibar.

Hafla ya makabidhiano hayo imefanyika Ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria na kuhudhuriwa na Waziri wa Katiba na Sheria wa Zanzibar, Khamis Juma Mwalim na mwakilishi wa Serikali ya Saud Arabia, Zyad Abdullah Abdullah Abuhasbu.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya tende hizo, Waziri Mwalim, alisema wizara yake itahakikisha inasimamia ugawaji wa tende hizo kwa walengwa waliotarajiwa.

Alisema Serikali ya Saud Arabia imekuwa na uhusiano mzuri wa kidugu na Zanzibar na kutoa misaada mbalimbali ya kimaendeleo.

"Tunawashukuru sana ndugu zetu wa Saud Arabia kwa misaada yao wanaotupatia, uhusiano wetu ni wa historia na wa muda mrefu," alisema.

Vile vile, aliiomba serikali ya Saud Arabia kuendelea kuisaidia Zanzibar katika huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Naye Mwakilishi wa Balozi wa Saud Arabia, Abuhasbu, aliishukuru Serikali ya Zanzibar kwa ushirikino wao na kukubali kupokea msaada huo kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.

"Huu msaada wa tende umeletwa na wananchi wa Saud Arabia kwa ajili ya ndugu zao wananchi wa Zanzibar kutokana na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya nchi mbili hizi," alisema.

# Wazazi, walimu kushirikiana elimu ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wazazi kuendelea kushirikiana na walimu kuhakikisha elimu ya watoto wao inakuwa nzuri hasa watoto wa kike ili kuwa viongozi wa baadaye.

Akimkabidhi zawadi mwanafunzi bora wa kidato cha sita, Wahda Mbarak kutoka Shule ya Feza Zanzibar, ofisini kwake Mazizini mjini Unguja, alisema ushirikiano wa wazazi, walimu na wanafunzi unasaidia kuleta matokeo mazuri kwa watoto.

Alisema imani yake ni kubwa kwa kuwa nafasi aliyoipata ni kuwa kila mzazi angetamani mtoto wake aipate, lakini yote ni mipango ya Mungu pamoja

na jitihada za wazazi wake.

Pia alisisitiza ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inaendana na mitaala inayotolewa na Wizara ya Elimu.

Pia alimpongeza mwanafunzi huyo pamoja na uongozi wa Shule ya Feza Zanzibar kwa kutoa mwanafunzi bora na kuutaka uongoziwa shule hiyo kuelimisha shule nyingine za binafsi katika kushirikiana na serikali kwa kufuata mitaala pamoja na sera kama zilivyopangwa na mipangilio yote ya serikali ili kufikia malengo ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi wao.

Vile vile, alimtaka mwanafunzi huyo kuhakikisha anachagua fani inayotakiwa

katika soko la ajira nchini hasa katika fani za sayansi ili kusaidia upatikanaji wa wataalamu, wakati atakapoanza elimu yake ya juu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Feza Zanzibar, Ally Yusuph Nungu, alisema lengo la kutoa elimu ni kufurahia matokeo mazuri kwa watoto wao kama walivyopata nafasi ya kwanza Zanzibar kati ya shule 31 za kidato cha sita na kupata mwanafunzi wa saba kwa wanawake Tanzania nzima, kati

ya wanawake 38,000 waliofanya mitihani yao ya kidato cha sita, mwezi Mei, mwaka huu.

Kwa upande wake mwanafunzi Wahda, aliyefaulu katika masomo ya Sayansi kwa kidato cha sita na kupata mwanafunzi bora wa saba kitaifa, alisema jitihada zake pamoja na kuwasikiliza walimu na wazazi wake zimemwezesha kupata matokeo mazuri ya mtihani huo.

Aliwataka wanafunzi wa kike kusoma kwa bidii ili taifa liwe na wataalamu wengi wanawake katika fani mbalimbali na kuiletea nchi maendeleo.

# Waganga tiba mbadala wapewa angalizo

**Na Hamisi Nasiri,**
NACHINGWEA

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Rukia Muwango, amekutana na waganga wa tiba asili na tiba mbadala wilayani humo na kuwataka kuwa waadilifu na waaminifu wanapotekeleza majukumu yao.

Wito huo aliutoa katika kikao maalumu alipokutana na waganga hao ambacho kililenga kusikiliza kero zao na kuendeleza kuwaeleza kanuni na sheria.

Alisema serikali inawapongeza waganga hao kujisajili kwa wingi kama sheria inavyoelekeza, na kwamba hadi sasa waganga ambao wamejitokeza na kujisajili ni 125 na waganga 55 maombi yao bado yako mezani yanafanyiwa kazi.

Muwango alisema ili waganga hao waweze kufanya kazi zao vizuri, ni lazima wawe waadilifu na waaminifu pale wanapotekeleza majukumu yao na kuacha kufanya kazi kinyume cha utaratibu.

Mnatakiwa kuwa makini na wakweli katika kutibu wagonjwa wenu, na sio kuwadanganya na mwisho wa siku mgonjwa anapoteza maisha ndani ya vyumba vyenu, hii ni hatari na sio sawa," alisema Muwango. Alisema kundi hilo ni muhimu kwa jamii ambapo watu wengi wanalikimbilia kwa ajili ya kupata tiba mbadala, hivyo serikali imeona kuna umuhimu wa kukutana nao ili kutoa maelekezo ya kutambua taratibu za serikali zinavyowataka katika kutoa tiba zao kwa jamii.

Alisema waganga wa tiba asili na tiba mbadala pia wanatakiwa wawe mstari wa mbele katika kushiriki suala la ulinzi na usalama kwa vile wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa wakifanya matukio ya uhalifu kwenye jamii baada ya kudanganywa na baadhi ya waganga wasio waadilifu kwenye shughuli zao za tiba asili na tiba mbadala.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha watu hao kufanya mauaji kutokana na dhana potofu wanazopewa na waganga.

Mkuu huyo wa wilaya alisema pia wapo baadhi ya waganga wa tiba asili wamekuwa wakitumia nyara za serikali kama kifaa maalumu kwenye shughuli zao, ikiwamo kutumia mikia ya wanyama ambao ni mali ya serikali bila kufahamu kuwa nyara hizo zinaweza kuwaletea matatizo na kujikuta wakiwa mikononi mwa sheria.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya mbolea ya Petrobena, Peter Kumalilwa (kushoto), akimkabidhi Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Anthony Mavunde, zawadi ya mchele baada ya kuzindua msimu wa uvunaji mpunga kwenye shamba la hekari 50 la kikundi cha Agri-Ajira wilayani Kilosa, Mkoa wa Morogoro. Petrobena imekifadhili kikundi hicho cha vijana waliohitimu Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA). **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaitaka Chavita kufanya sensa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imekitaka Chama cha Viziwi Tanzania (Chavita) mkoani Morogoro, kufanya sensa ya kujua idadi yao ili watambuliwe na kuingizwa kwenye mipango ya maendeleo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, James Ihunyo, wakati wa kongamano la siku mbili la uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya alama kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika wilaya hiyo lililoitishwa na Chavita Mkoa wa Morogoro.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Robert Selasela, Ihunyo alisema pamoja na serikali kusaidia jamii ya watu wenye ulemavu katika masuala mbalimbali ikiwamo mikopo bado jamii hiyo inatakiwa kujua idadi yao ili wasaidiwe.

Alisema wilaya haina takwimu halisi za idadi kamili ya viziwi, hali hiyo inapelekea halmashauri kushindwa kutimiza azma yake ya kusaidia kuwapatia mikopo ama kuwashirikisha katika masuala yanayowahusu.

Mkuu huyo wa wilaya alisema licha ya Chavita mkoa kutoa mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na usalama, bado viziwi wengi wilayani hawajapatiwa mafunzo ili kujua alama zao, hivyo kufanya wengi wao kushindwa kuwasiliana na jamii zinazowazunguka.

Alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoshiriki kongamano hilo kuwa vimepata vitu vipya ili kwenda kuwa mabalozi wazuri, na kuhamasisha kila uchao lugha za alama na kuwafanya watu wengi waijue lugha hiyo.

Awali katika risala yao walemavu hao wa kutosikia, walisema wanaiunga mkono serikali kwa juhudi za kukuza uchumi wa nchi na kuomba kushirikishwa katika uchumi wa viwanda.

Aidha, Chavita Morogoro wameiomba halmashauri kuwawezesha gharama za nauli ili waweze kushiriki Wiki ya Kimataifa ya Viziwi Duniani itakayofanyika kitaifa mkoani Iringa, na pia wilaya iwasaidie ili kuyafanya mafunzo ya alama kuwa endelevu. Mratibu wa kongamano hilo, Henry Mtasiwa, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo katika taasisi hizo kutokana na watu wengine kufika katika ofisi kwa matatizo mbalimbali wakiwamo viziwi.

Kongamano hilo limefadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Civil Society.

## Wapigia debe uwekezaji utalii

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WADAU wa utalii mkoani Kagera wamesema sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa mkoa na nchi, na kutekeleza sera ya serikali ya viwanda endapo utafanyika uwekezaji wa kutosha ambao utavutia watalii kutembelea mkoa huo kwa wingi.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa utalii katika Manispaa ya Bukoba, Mkurugenzi wa Kampuni ya utalii ya Kiroyera Tours, Marry Kalikawe, alisema sasa ni muda muafaka kwa wananchi kuchangamkia fursa ya uwapo hifadhi mpya za taifa za Burigi wilayani Chato, Ibanda wilayani Kyerwa na Rumanyika wilayani Karagwe, kwa kuanzisha miradi ya kiuchumi.

"Kuwa mdau kuna ujenzi wa hoteli, kuna upishi wa chakula, wanaofanya kilimo cha mazao mbalimbali, tunavyozidi kuwa na hoteli nyingi na sehemu za burudani, shughuli zote hizo zinawezesha uundaji wa vitu unaweza kusaidia viwanda kukua," alisema.

Alisema kuwa wao kama waongoza utalii wako tayari kushirikiana na watu wote na kuwa wananchi wakihabarishana watawezesha utalii kukua kwa kasi. "Kuwapo kwa mbuga za wanyama pekee haitoshi, inabidi kuajiri watu wanaoweza kufanya shughuli za utalii, kununua magari ya watalii, maana tumekuwa na utalii wa utamaduni kabla ya mbuga hizi kupandishwa hadhi, kwa hiyo inabidi kujipanga vizuri katika uwekezaji," alisema.

Mdau mwigine, Edward Mjungi, alisema kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kukuza uchumi wa mkoa na uchumi wa mtu mmoja mmoja kutumia sekta ya utalii, maana vyanzo vya utalii vipo na asili zake zipo. Mjungi alisema mkoa wa Kagera umekuwa mkoa wa pembezoni, na ilikuwa haionekani kama wanaweza kuwekeza katika utalii maana utalii ni mzunguko, lakini kwa sasa kuna utashi wa serikali na wanachokitafuta sasa ni utashi wa jamii, ili watambue kwamba hiyo ni fursa kiuchumi. "Sasa tusilale Wanakagera tuamke, tukilala tutatoa fursa kwa wananchi wa mikoa ya Kaskazini kuja kuchangamkia fursa hizi, na sisi kubakia kuwa watazamaji," alisema Mjungi. Mkuu wa mkoa wa Kagera, Marco Gaguti, alisema mkutano huo ni moja ya maandalizi ya wiki ya uwekezaji Kagera, na kuwa uwapo wa hifadhi mpya tatu ni kichocheo cha kuziunganisha kiuchumi Tanzania na nchi jirani ikiwamo Rwanda na Uganda.

"Kwa hiyo upo umuhimu kwa wananchi wa mkoa wa Kagera kuona maeneo haya na kuwekeza katika fursa za kutoa huduma za kitalii, ikiwamo masuala ya ujenzi wa hoteli, kambi za watalii, kufanya usafiri na usafirishaji na kuandaa shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinahusiana na masuala ya utalii," alisema.

## Mtuhumiwa shambulizi la kigaidi atiwa mbaroni

**ISLAMABAD, Pakistan.**

MAAFISA wa usalama nchini Pakistan wamemkamata Hafiz Saeed, mtuhumiwa wa shambulizi la siku nne katika mji wa Mumbai nchini India mwaka 2008, akikabiliwa na mashitaka ya kufadhili ugaidi.

Hatua hiyo imekuja siku chache kabla ya ziara ya Waziri Mkuu, Imran Khan wa Pakistan mjini Washington, Marekani.

Khan ameapa kuyaangamiza makundi ya wanamgambo wa itikadi kali yanayoendesha harakati zao nchini Pakistan.

Saeed, ambaye yuko kwenye orodha ya Marekani ya magaidi wanaosakwa, ni muasisi wa Lashkar-e-Taiba, kundi la wanamgambo linalolaumiwa na Marekani na India kwa kufanya mashambulizi ya Mumbai, ambayo yaliwauwa zaidi ya watu 160.

Anakanusha kuhusika kwa vyovyote na shambulizi hilo akisema mtandao wake, ambao una seminari 300 na shule, hospitali, kampuni ya uchapishaji na huduma za dharura kwa wagonjwa, hauna mahusiano na makundi ya wanamgambo.

## Trump: Mimi si mbaguzi

**NEWYORK, Marekani.**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesisitiza kuwa yeye si mbaguzi baada ya mashambulizi yake kupitia Twitter dhidi ya wabunge wanne wanawake kukemewa vikali.

Katika ukurasa wa Twitter aliwataka wanawake hao wasio na asili ya Marekani, "kuondoka" kuelekea kwenye nchi zao walipotoka.

Kitendo hicho kiliamsha ghadhabu kubwa,Trump alikataa shutuma kuwa yeye ni mbaguzi: "sina asili ya ubaguzi mwilini mwangu!"alisema Bunge la wawakilishi linajiandaa kupigia kura makubaliano ya pamoja ya kukemea kauli zake, huku hatua hiyo ikitegemewa kupita kutokana na kuwepo wawakilishi wengi wa Democrats.

Awali, wabunge Alexandria Ocasio-Cortez, Ilhan Omar, Ayanna Pressley na Rashida Tlaib walitangaza kupuuza matamshi ya Trump wakidai yanalenga kuwaondoa kwenye mstari. Wabunge hao waliwataka watu nchini humo kupuuza maneno yake.Rais Trump hakutamka majina ya wanawake hayo kwenye ukurasa wa Twitter, lakini yaliyokuwemo kwenye matamshi yake yalionesha wazi kuwapo kwa uhusiano na wabunge hao.

Alisababisha hasira baada ya kusema wanawake "ambao asili yao wanatoka kwenye nchi ambazo serikali zake ni zina machafuko" warejee makwao.

# Jeshi, upinzani wakubaliana kugawana madaraka Sudan

**KHARTOUM Sudan.**

JESHI la Sudan limesaini makubaliano ya kugawana uongozi na upinzani.

Baraza tawala la kijeshi na viongozi wa upinzani nchini Sudan, wamesaini makubaliano ya kugawanya uongozi baada ya mazungumzo ya usiku kucha kumaliza mzozo nchini humo.

Kumefanyika sherehe zilizomalizika hivi punde katika hoteli ya Corinthia katika mji mkuu wa Khartoum. Makubaliano hayo yanatazamia miaka mitatu ya uongozi wa pamoja utakaofuatwa kwa uchaguzi mkuu.

Baada ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, viongozi wa pande zote wamezungumzia kizazi kipya katika taifa ambalo limeshuhudia ghasia na mauaji ya mamia ya waandamanaji tangu kutimuliwa kwa kiongozi aliyekuwepo Omar El Bashir Aprili mwaka huu.

Katika makabiliano na jeshi yaliogeuka kuwa ghasia zilizosababisha vifo vya watu , waandamanaji walitaka jeshi likabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia.

Utiaji saini wa makubaliano hayo, unaonekana kuthibitisha makubaliano yalioidhinishwa mapema mwezi huu. Yanaeleza kwamba jeshi litakuwa uongozini kwa miezi 21 ya kwanza, na baada ya hapo utawala wa kiraia utaidhinishwa katika miezi 18 itakayofuata, na kufuatwa kwa uchaguzi mkuu.

Makubaliano ya pili kuhusu masuala ya katiba yanatarajiwa kukamilishwa Ijumaa wiki hii.

***BBC.***



Viongozi wa baraza la mpito la kijeshi nchini Sudan wakati wa kutia saini makubaliano ya kugawana madaraka. **PICHA BBC**

# Mataifa makubwa yataka maridhiano Libya

**TRIPOLI, Libya**

MATAIFA makubwa yakiwamo yanayomuunga mkono kiongozi wa waasi, yametoa wito wa kusitishwa mapigano nchini Libya, yalionya kuwa umwagaji damu unazidisha hali ya kibinadamu ambayo imeelezwa kuwa janga.

Marekani, Ufaransa, Uingereza na Italia zimeungana na Misri na Umoja wa Falme za Kiarabu - mataifa mawili ambayo kwa pamoja na Saudi Arabia yanamuunga mkono mbabe wa kivita Khalifsa Haftar katika kuelezea wasiwasi juu ya machafuko yanayoendelea katika mji mkuu wa Libya Tripoli.

Mataifa hayo sita "yanatoa wito wa kupunguza mara moja mzozo na kusitisha mapigano ya sasa, na yanahimiza kurejea kwenye mchakato wa kisiasa unaoongozwa na Umoja wa Mataifa," ilisema taarifa ya pamoja.

Wameonya kuwa mapigano yamechochea dharura inayoongezeka ya kibinadamu, kuzidisha mzozo na wahamiaji, na kuelezea hofu kwamba makundi ya itikadi kali yatashamiri kukiwa na ombwe la usalama.

Libya imegawika kati ya serikali ya maridhiano ya kitaifa mjini Tripoli, ambayo inaungwa mkono na Umoja wa Mataifa, na serikali ya mjini Tobruk inayoongozwa na Marshal Khalifa Haftar.

Kituo cha kuwazuia wahamiaji wa Kiafrika kilishambuliwa katika kampeni ya Haftar kuutwaa mji mkuu Tripoli, Julai 3, 2019.

Haftar pia anaudhibiti mji wa mashariki ya Benghazi ambako wakaazi wake waliandama Jumapili kupiga madai ya Uturuki kuiunga mkono serikali ya mjini Tripoli.

Muftah Mohamed alikuwa mmojawapo wa washiriki wa maandamano hayo na anasema wanaliunga mkono jeshi la LNA na kutoa wito wa kususiwa kwa Uturuki.

"Tunaliunga mkono jeshi la LNA, tunatoa wito wa kususiwa Uturuki, Fayez Surraj na majambazi na wahalifu wote mjini Tripoli. Na sisi ni washindi, na kutoka ushindi hadi ushindi, bado tunalipa gharama.

Hatumuogopi yeyote, hatuiogopi Uturuki, tumeunda jeshi imara na Polisi," alisema.

Karibu watu 1,100 wameuawa katika kampeni ya Haftar iliyodumu kwa mwezi mmoja akijaribu kuutwaa mji mkuu Tripoli kutoka serikali ya maridhiano ya kitaifa inayotambuliwa na Umoja wa Matifa. ***DW.***

# ATCL yaanza safari za India

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, jana alizindua safari ya kwanza ya ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwenda katika Jiji la Mumbai, India.

Akiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, Kamwelwe alisema hatua hiyo ni muhimu kwa shirika hilo kujitanua katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga kimataifa.

Kamwelwe alisema kuanza kwa safari hiyo na nyingine kutasaidia kukuza uchumi, kuiunganisha Tanzania na mataifa mengine na kukuza sekta ya utalii nchini.

Alisema wapo Watanzania wengine wanasoma, wanaokwenda kupatiwa matibabu na wanaoishi India na raia wa India wanaokuja nchini, hivyo kuanzishwa kwa safari hizo kutarahisisha uhusiano wa mataifa hayo.

"Hapa tulipo ni kwenye uwanja wa ndege mpya (Terminal III), ambao mwekezaji ni serikali, ndege ya ATCL mwekezaji ni serikali, hivyo mmiliki ni wananchi na ninaamini mtatunza uwekezaji huu kwa manufaa ya taifa," Kamwelwe alisema. Aliongeza kuwa serikali itaendelea kufanya kila linalowekezana kufungua fursa kwa kila Mtanzania kwa kufuata taratibu na sheria za nchini.

Waziri huyo aliutaka uongozi wa ATCL kufanya kazi kwa ufanisi ili kampuni hiyo ikue na kuleta faida kwa taifa na kukuza uchumi kwa ujumla.

"Tunaamini ATCL pia itaendelea kufungua fursa kwa nchi nyingine ili Tanzania kuunganishwa na mataifa mengi kwa uchumi wa taifa letu," Kamwele alisema.

"Leo (jana) tunapanda ndege kwenda India moja kwa moja kwa saa saba, tena bila hata kuchimba dawa, si mnaona jamani, hapo ukipanda ndege ni moja kwa moja mpaka Mumbai."

Kuanza kwa safari hizo za India kumefanyika ikiwa ni wiki mbili tangu shirika hilo lizindue safari zake za Tanzania-Johannesburg, Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa shirika hilo, safari ya kwanza ilianza jana na ya pili itakua Julai 19 kwenda moja kwa moja Mumbai.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa shirika hilo, gharama ya safari ya Dar es Salaam-Mumbai, ni Dola za Marekani 378 (Sh. 869,232).




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael (kulia), akiongea na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, wakati akitangaza washindi 5 wa tiketi za kwenda kushuhudia mashindano ya kombe la Mataifa ya Afrika nchini Misri kupitia promosheni ya SOKA LA AFRICA inayoendeshwa na kampuni ya Tigo, (kushoto) mtaalamu wa huduma za ziada kutoka kampuni hiyo, Ikunda Ngowi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakulima mpunga wafurahia kilimo cha umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu, MVOMERO**

WAKULIMA wa mpunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro wamesema kilimo cha umwagiliaji kimewaletea neema kwa kuboresha na kuinua kipato katika familia zao.

Wakizungumza jana wakati wa ziara ya waandishi wa habari na wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji waliotembelea skimu ya umwagiliaji ya Dakawa, wakulima hao walisema kutokana na kilimo cha umwagiliaji, vipato vyao vimeongezeka na kubadilisha mtindo wa maisha yao kuwa bora.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima Wadogo Kilimo cha Umwagiliaji Mpunga Dakawa (Uwawakuda), Thomas Kakema, alisema kabla ya kuanzishwa kwa ushirika huo hali ya maisha ya wakazi wa Dakawa ilikuwa duni.

Kakema alisema kwa sasa wakulima wengi wamejenga nyumba za kisasa za kuishi kutokana na kipato wanachokipata baada ya mavuno, pia wamepata fursa za mikopo ya kilimo kutoka taasisi mbalimbali za fedha.

"Upatikanaji wa mikopo mikubwa ya zana za kilimo kama vile matrekta na mashine za kuvunia ni moja ya mafanikio makubwa waliopata wakulima wetu," alisema Kakema.

Alisema kilimo cha umwagiliaji katika skimu ya Dakawa kimeleta ajira kwa wakazi wa Dakawa na maeneo ya jirani hususan vijana ambao wamefungua biashara mbalimbali zinazowasaidia kuhudumia familia zao na kuchangia pato la taifa kwa ujumla.

Akizungumza awali kuhusu hali ya uzalishaji wa mpunga katika skimu ya Dakawa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Florent Kyombo, alisema kutokana na serikali kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 2.0 za awali hadi 6.5 kwa hekta.

Kyombo alisema sababu za kuongezeka kwa uzalishaji ni pamoja na maji kufika shambani kwa wakati, kushuka kwa gharama za uzalishaji zilizokuwa zikichangiwa na gharama kubwa za usafirishaji na pembejeo na kuimarika kwa usimamizi wa wataalamu na wakulima wenyewe kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu.

Alisema kuongezeka kwa uzalishaji huo kumechangia kuwapo kwa chakula cha kutosha ndani ya wilaya yake, Mkoa wa Morogoro na mikoa jirani.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ina jumla ya skimu 11 za umwagiliaji ambazo zinafanya kazi na bado jitihada zinafanyika ili kuendeleza maeneo mengine ili yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji.

## 26 wafanyiwa upasuaji moyo JKCI

**Na Romana Mallya**

WAGONJWA 26 miongoni mwao wakiwa ni watoto 14 wamefanyiwa upasuaji wa moyo wa kufungua kifua katika kambi maalum ya matibabu ya siku 14 inayofanyika katika Taasisi ya Moyo, Jakaya Kikwete (JKCI).

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Upasuaji, Dk. Anjela Muhozya, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza watoto hao ni wale wenye matatizo ya moyo ya kuzaliwa nayo ambayo ni matundu, mishipa ya damu ya moyo na valvu kutofanya kazi vizuri.

"Watu wazima 13 wamefanyiwa upasuaji wa kubadilishwa valvu moja hadi tatu ambazo hazikuwa zinafanya kazi vizuri na kupandikizwa mishipa ya damu ya moyo," alisema.

Dk. Muhozya, alisema matibabu hayo yanafanywa na wataalamu wa taasisi hiyo kwa kushirikiana na wenzao kutoka Shirika la CardioStart International la nchini Marekani. Daktari huyo ambaye pia ni bingwa wa usingizi na wagonjwa walioko katika uangalizi maalum (ICU), alisema katika kambi hiyo walipanga kufanya upasuaji kwa wagonjwa 40.

"Kati ya hao, watoto 20 na watu wazima 20, hadi sasa wameweza kufanya upasuaji kwa wagonjwa 26 ambao hali zao zinaendelea vizuri na wengine wamesharuhusiwa kutoka ICU na kupelekwa wodini kwa ajili ya kuanza mazoezi pamoja na kuendelea na matibabu mengine," alisema.

Aliongeza: "Katika watoto tuliowafanyia upasuaji, mtoto mmoja alikuwa na tatizo kubwa la valvu zake tatu kutokufanya kazi vizuri, leo hii tunamfanyia upasuaji na kumwekea valvu nyingine tatu."

Dk. Muhozya alisema kuwapo kwa kambi hiyo kumesaidia kwa kiasi kikubwa wagonjwa waliohitaji matibabu ya utaalamu wa hali ya juu kufanyiwa upasuaji wakiwa Tanzania.

Kasilda Koka, ambaye mtoto wake wa kike amefanyiwa upasuaji katika kambi hiyo aliishukuru serikali na wafanyakazi wa JKCI kwa kumpokea na kumfanyia upasuaji kwa kutumia bima ya afya.

"Mwaka 1999 wakati huduma za upasuaji wa moyo hazikuwapo hapa nchini nilimpeleka mwanangu ambaye alikuwa na tundu katika moyo kutibiwa nchini India ambako nilitumia gharama kubwa," alisema na kuongeza:

"Mwanangu alikuwa na shida ya valvu moja kutofanya kazi vizuri ameweza kufanyiwa upasuaji hapa nchini na kuwekewa valvu nyingine kama mnavyomuona anaendelea vizuri," alisema Kasilda.

## Waziri Mkuu aionya TCU kunyanyasa

*INATOKA UK. 3*

visaidie kuongeza udahili. Ni wakati mwafaka kwa tume kujipambanua kwenye uwezeshaji na ushauri ili kuondoa taswira hii," alisema.

Pia Majaliwa aliitaka TCU itafute mbinu bora zaidi na kuvijengea uwezo vyuo vikuu binafsi ili visaidie kuongeza udahili kwa sababu lengo la serikali ni vishiriki katika maendeleo kwenye sekta ya elimu ya juu nchini.

"Tume itafute mbinu bora zaidi ikiwa ni pamoja na kuvijengea uwezo vyuo vikuu binafsi ili visaidie kuongeza udahili. Ni wakati mwafaka kwa tume kujipambanua kwenye uwezeshaji na ushauri ili kuondoa taswira hasi miongoni mwa jamii kwamba kazi kubwa ya TCU ni kuvifungia vyuo vikuu badala ya kuvisaidia kutatua changamoto zinazovikabili," alisema.

Kuhusu idadi ndogo ya wahitimu wa elimu ya juu, Waziri Mkuu alisema takwimu za kimataifa za ushiriki wa elimu ya juu zinaonyesha kwamba kufikia mwaka 2017 ni asilimia moja hadi tatu tu ya Watanzania kwa kila Watanzania 100 wenye umri chini ya miaka 25 wanapata elimu ya Chuo Kikuu.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PLOT NA NYUMBA VINAUZWA**

Ploti na nyumba vinauzwa mtoni kijichi wilaya ya temeke. Ploti ni mbili kwa moja ni nzuri na kubwa saana kwa matumizi yote ya kibiashara na makazi. Mawasiliano: 0688 640101

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**Philomena Erick Mathew** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye **index namba S5121/0036** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2018 katika shule ya Sekondari Hope and Joy. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa : **WMB/RB/2402/19**

115326602


### KUPOTEA KWA CHETI



**Veronica Asantieli Moshi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4010-0117** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Lupanga Practising . Yeyote atakaeiona atoae taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MBU/RB/44519/2019**

115326902


### KUPOTEA KWA CHETI.



**INNOCENT CLAVERY LOBOZI** (Pichani) amepotelewa na cheti cha kidato cha NNE cha Kashozi Sekondari, chenye **index namba : 50406-122** kilichotolewa mwaka 1990 na BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA).
Taarifa za upotevu ziliripotiwa kituo cha police na kupewa kumbukumbu namba **KAG/BUK/RB/122891/2019.**
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha police , au awasiliane na mhusika kwa namba **0757285513.**

1153327402

### KUPOTEA KWA CHETI.



**INNOCENT CLAVERY LOBOZI** (Pichani) amepotelewa na cheti cha Ualimu Daraja 'A' chenye **index namba: E.504-0086** cha chuo cha ualimu Katoke kilichotolewa mwaka 1993. Taarifa za upotevu ziliripotiwa kituo cha police na kupewa kumbukumbu namba **KAG/BUK/RB/122908/2019.**
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha police, au awasiliane na mhusika kwa namba **0757285513.**

1153327402

**IN THE HIGH COURT OF DISTRICT DELEGETE AT HAI**

**PROB AND ADMNI CAUSE NO.20 OF 2019**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE ......ELIZABETH ELIUFOO URASSA**

**BY ....ELIUFOO PENDAELI URASSA.......**

**NOTICE OF MENTION OF PETITION**
**(Made under rule 68(4)**

**TO WHOM IT MY CONCERN**

**TAKE NOTICE** That the above petition has been set for mention on 30 day of August 2019 before Hon. D.J.Msoffe -RM.

Dated at HAI this 12 day of July 2019

DISTRICT DELEGETE HAI
RESIDENT MAGISTRATE HAI

215327102

**FORM II**

**CITATION**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINTINKU**

**USIMAMIZI WA MARTHI No. 01**

**Ombi la LAURENT NDAHANI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu YOHANA AMATI @ MSOTI**

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 15/7/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 29/7/2019

Tarehe 29/07/2019
Sahihi


215327202

### KUPOTEA KWA KADI

**John Chacha Nyamhanga** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 478 BLN** aina ya CHEVROLET,yenye chasis namba **HR-525-706553** na engine namba M13A yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **1909/2019**

115326802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Raphael M. Mhetela** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1005/0225** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Kishimba. Yeyote atakaeiona atoae taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taarifa: **MBT/RB/1202/19**

115326702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: KAWE**
**Usimamizi wa Mirathi No. 124/2019**

Ombi la **PROTAS PIRMIN NYONI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **PIRMIN SIXBERT NYONI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 02/08/2019.
kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ya PIRMIN SIXBERT NYONI.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe ..................................

115327602

### VOLUNTEERS VOLUNTEERS

Wataalamu wa kujitolea wanahitajika katika asasi ya Mpakani Tunaweza Organization (TUNAWEZA) ya ubungo jijini Dar es Salaam, Katika sekta za:

- **IT au Tehema**
- **Uhasibu**
- **Ufuatiliaji na Tathmini**
- **Uratibu/Coordination**
- **Rasilimali watu**

Tuma barua ya maombi na wasifu wako ( CV) katika barua pepe hii tunaweza. **women@yahoo.com**.

**Mawasiliano**
**0654762076/ 0762997181**

115327301

### KUPOTEA KWA CHETI




**UPENDO ELIEZA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Forodhani Dar es Salaam kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 1982

**Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa polisi:**
**MOS/RB/4869/19**

115328002

### KUPOTEA KWA CHETI



**Fortunatus Palapala Malima** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0332/0734** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Morogoro.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DOM/RB/461/2019**

115327502

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SAID JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 327 AQY.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/B.I/I/VOL VII/019.**

115328402

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz , au

piga simu: 0767 223311

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# SENEGAL VS ALGERIA FAINALI YA KIBABE



Mahrez

**CAIRO, Misri**

MICHUANO ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), inafikia tamati leo wakati fainali yake inapigwa kwenye Uwanja wa Taifa wa Cairo ikiwakutanisha miamba ya soka barani hapa, Algeria dhidi ya Senegal.

Timu hizo ambazo zilianza mashindano katika kundi moja moja na Tanzania na Kenya ziliibuka na ushindi dhidi ya wapinzani wao na kukata tiketi ya kukutana tena kwenye fainali.

Kwenye hatua ya makundi, Algeria iliilaza Senegal bao 1-0, je matokeo hayo yatajirudia leo Ijumaa usiku kwenye fainali, ama Senegali italipiza kisasi na kubeba kombe.

Goli la kujifunga la Tunisia katika muda wa nyongeza liliwavusha Senegal hadi hatua ya fainali ya michuano hiyo ambayo kwa mara ya kwanza ilishirikisha timu 24.

Nusu fainali ya kwanza ilizikutanisha Senegal na Tunisia.

Japo wengi waliipigia chapuo Senegal kushinda mchezo huo, lakini ushindi haukuwa rahisi, na Tunisia walipambana hadi dakika za mwisho.

Dakika 90 zilimalizika bila timu yoyote kupata ushindi, huku pande zote mbili zikikosa penalti katika kipindi cha pili.

Ushindi ulipatikana kwa Senegal ndani ya dakika 30 za nyongeza.

Kipa wa Tunisia, Moez Hassen, alifanya makosa katika dakika ya 100 kwa kuokoa vibaya mpira wa krosi na kumgonga beki wake, Dylan Bronn na kuzama wavuni.

Katika dakika za mwisho za mchezo huo kukatokea 'tafrani' baada ya mwamuzi kutoa penalti golini mwa Senegal kwa madai kuwa kiungo Idrissa Gana Guaye aliunawa mpira.

Hata hivyo, penalti hiyo ilikataliwa baada ya mwamuzi kwenda kujihakikishia kwenye teknolojia ya maamuzi ya usaidizi wa video, VAR.

Hii ni mara ya pili kwa Senegal kutinga hatua ya fainali, kwani mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2002 ambapo walipoteza kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Cameroon.

Safari ya Tunisia kutaka kulichukua kombe hilo kwa mara ya pili ilifikia mwisho hapo.

Mchezo wa pili wa nusu fainali ulizikutanisha Algeria na Nigeria ambayo ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kushinda.

Nigeria ndiyo timu pekee kati ya zilizocheza nusu fainali ambayo imeshinda kombe hilo zaidi ya mara moja. Imenyakua mara tatu, mara ya mwisho ikiwa mwaka 2013.

Hata hivyo, ndoto zao za kuchukua kombe hilo kwa mara ya nne zilizimwa kwa kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa mbweha wa Jangwani, Algeria.

Algeria ilitangulia kuandika goli katika dakika ya 40 ya mchezo baada ya mchezaji wa Nigeria William Troost-Ekong kujifunga.

Nigeria wakarejea mchezoni kwa goli la kusawazisha lililofungwa kupitia mkwaju wa penalti na Odion Ighalo katika dakika ya 73.

Mshambuliaji wa Manchester City, Riyad Mahrez ndiye aliyepeleka kilio nchini Nigeria kwa kupachika bao la ushindi kwa Algeria katika dakika ya 95.

Algeria sasa ipo mbioni kulinyakua kombe hilo kwa mara ya pili.

Mara ya kwanza na ya mwisho kwao kulinyanyua kombe hilo ilikuwa 1990, hata Mahrez ambaye ni nahodha wa kikosi cha sasa alikuwa bado hajazaliwa.

Timu tatu zenye mafanikio makubwa zaidi Afrika - Misri, Cameroon na Ghana - ziling'olewa kwenye hatua ya mtoano au maarufu kama 16 bora.

NANI ANAPEWA NAFASI

Senegal ndio chaguo la wacheza kamari wengi kwamba inaweza kutwaa taji hilo hivi leo.

Japo Algeria ndiyo timu ambayo imeonyesha kiwango kikubwa zaidi na ukomavu wa hali ya juu kwenye mashindano hayo hadi sasa.

Imeshinda michezo yote ikiwamo ushindi wa 1-0 dhidi ya Senegal - katika hatua ya makundi.

Baada ya hapo wakaitandika Guinea 3-0 kwenye hatua ya mtoano, na kisha kuwaondoa Ivory Coast kwa penati kwenye robo fainali, na leo kuwanyuka mabingwa mara tatu Nigeria kwenye nusu fainali.

Senegal ilimaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi C na kisha kuwatoa Uganda kwenye hatua ya mtoano halafu ikawafunga Benin katika hatua ya robo fainali na baadaye waliing'oa Tunisia kwenye hatua ya nusu fainali.



Mane



# RODGERS:

## LEICESTER IMEKATAA OFA MBILI ZA MAGUIRE

**LEICESTER, England**

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers, amethibitisha kwamba klabu hiyo tayari imekataa ofa mbili za kumuuza beki wake wa kati, Harry Maguire.

Licha ya ofa hizo, mchezaji huyo wa kimataifa wa England alicheza katika kipindi cha pili wakati Leicester ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Scunthorpe kwenye mchezo wa kirafiki Jumanne usiku.

Maguire amekuwa akiwaniwa na klabu pinzani za jiji moja, Manchester United, lakini hakuna ofa yoyote iliyofikia kiasi wanachokitaka cha pauni milioni 90 za kumuuza mchezaji huyo.

"Harry ni mchezaji mwenye ubora wa hali ya juu na hakuna klabu iliyokaribia kiasi cha thamani yake ambayo klabu imekiweka," amesema Rodgers akiwaambiwa waandishi wa habari.

"Hadi sasa klabu zote zimeshindwa kufikia kiasi cha fedha tunachokitaka na kwa vyovyote hatutaweza kumuuza kwa bei ya chini tofauti na thamani yake."

Aliongeza kusema kwamba: "Klabu haina tatizo, kwani tukimpoteza tayari tuna wachezaji wengi wa kuwaangalia."

Kiasi cha pauni milioni 90 kinachotakiwa na klabu hiyo kitavunja rekodi iliyowekwa na Virgil van Dijk ambaye alinunuliwa kwa pauni milioni 75 na kuwa beki ghali zaidi duniani, wakati alipojiunga na Liverpool kutoka Southampton Januari mwaka 2018.

United ilionekana kama ndio iliyokuwa na nafasi kubwa zaidi ya kumsajili Maguire, lakini Pep Guardiola alijitosa kwenye mbio hizo kwa ajili ya kutafuta beki wa kuziba pengo la nahodha, Vincent Kompany ambaye ameondoka klabuni hapo baada ya kumaliza mkataba wake.

Kutakiwa huko kwa Maguire hakukumzuia Rodgers kumpa beki huyo dakika 45 za kucheza pale katika dimba la Glanford Park.

## TOTTENHAM YAMWACHA DANNY ROSE



**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham imemwacha Danny Rose kwenye ziara yake ya maandalizi ya msimu mpya barani Asia wakati wakiwa na nia ya kutaka kumuuza beki huyo wa kushoto wa England, kwa mujibu wa gazeti la The Telegraph.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 29, amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa, lakini anaweza kuondoka kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 25.

Wakati pande zote mbili klabu na mchezaji mwenyewe wakiwa na furaha kuachana baada ya kucheza mechi 198 na kufunga mabao 10 katika mashindano yote, lakini kama hatauzwa atabakia kwenye kikosi hicho msimu ujao.

Rose alichelewa kujiunga na wachezaji wenzake wa timu hiyo baada ya kutoka kuichezea England kwenye mashindano ya Ligi ya Uefa, wakati England ilipomaliza nafasi ya tatu.

Wachezaji kama Victor Wanyama, Serge Aurier na Davinson Sanchez, ambao walikuwa na timu zao kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), na Copa America, hawatasafiri kwenda Asia, huku Eric Dier anaendelea kuuguza majeruhi yake jijini London.

Rose ni mmoja kati ya wachezaji nane ambao Tottenham imewaweka sokoni kwa ajiili ya kutafuta fedha za kununua nyota wapya.

Tayati Spurs imefanya usajili ulioweka rekodi klabuni hapo kwa kumsajili Tanguy Ndombele kwa pauni milioni 55.45 kutoka Lyon ya Ufaransa.

Wachezaji wengine waliowekwa sokoni ni pamoja na Kieran Trippier, Serge Aurier, Wanyama, Vincent Janssen, Cameron Carter-Vickers, Josh Onomah na Marcus Edwards.

## BRUCE KOCHA MPYA NEWCASTLE

**NEWCASTLE, England**

KLABU ya Newcastle imethibitisha kwamba imemteua Steve Bruce kuwa kocha wao mpya kwa mkataba wa miaka mitatu.

Bruce amejiunga na Newcastle baada ya kuiacha klabu ya Sheffield Wednesday Jumatatu wiki hii.

Baada ya kupewa mikoba hiyo, Bruce aliwaambia waandishi wa habari: "Nina furaha kubwa kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Newcastle United. Hii ni klabu yangu ya ujanani na ilikuwa klabu ya baba yangu, hivyo ni wakati muhimu zaidi kwangu na familia yangu."

"Kuna changamoto kubwa mbele yetu, lakini mimi na wenzangu tupo tayari kwa hilo. Tutajiimarisha sisi wenyewe kwa kujitolewa kwa kila kitu ili kuwawezesha mashabiki kuwa na timu yenye mafanikio na watakayojivunia."

Wasaidizi wa muda mrefu wa Bruce, Steve Agnew na Stephen Clemence, pia wamemfuata kocha huyo kwenye umri wa miaka 58 kwenda pale kwenye dimba la St James' Park.

Newcastle ilithibitisha kwenye taarifa yake Jumatano kwamba, Bruce alitarajiwa kukutana na kikosi hicho bada ya mchezo wa kirafiki dhidi ya Wolves mjini Nanjing.

Ujio wa Bruce hautarajii kutuliza hasira za mashabiki wa klabu hiyo ambao hawakuridhishwa na kuondoka kwa kocha, Rafa Benitez.

Benitez aliondoka klabuni hapo baada ya kuka kwa muda wa miaka mitatu kwa kushindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na sasa ni kocha huyo mwenye umri wa miaka 59 ni Kocha wa Klabu ya Dalian Yifang.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL KUSAJILI 'MAJEMBE' MANNE

Kocha Emery aeleza wako tayari kutumia gharama kubwa ili...

**LONDON, England**

UNAI Emery amewahakikishia mashabiki wa Arsenal kwamba wapo kwenye mipango ya kusajili wachezaji wakubwa wanne kabla ya kufungwa kwa pazia la usajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Kocha huyo Emery hadi sasa amefanya usajili mmoja tu wa kipindi hiki cha majira ya joto kwa kumchukua mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 18 kwa ada ya pauni milioni 6 kutoka klabu ya Ituano ya nchini humo.

Pia ofa ya ya kutaka kuwasajili nyota wa Crystal Palace, Wilfried Zaha na beki wa Celtic, Kieran Tierney zilikataliwa, na sasa wapo kwenye mbio moja na wapinzani wao wa London Kaskazini, Tottenham kuwania kumsajili beki wa St Etienne, William Saliba ma kiungo wa Real Madrid, Dani Ceballos.

Emery amesema: "Tunazungumzia kuhusu wachezaji wakubwa kwa sababu tunaanza kufikiria kuhusu timu yetu na kikosi chetu kwa sasa.

"Tuna wachezaji wazuri na vijana ambao wanaweza kuendelea kuimarika na kuisaidia timu kwa siku za usoni, lakini tunapawa kusajili wengine wakubwa.

"Lakini kwa sasa tunahitaji wachezaji wakubwa na malengo yetu ni kuwasajili watatu hadi wanne kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu kuelekea msimu ujao.

"Kwa sasa tunamahitaji makubwa ya kuimarisha kikosi chetu na hivyo tunataka kufanya usajili wa wachezaji wakubwa na wa gharama kubwa.

"Tunaingia sokoni kwa utulivu na umakini mkubwa. Tunahitaji kupata wachezaji bora kwa baadhi ya nafasi, kwa uhakika tunataka kufanya usajili wa nguvu."

Hata hivyo, Arsenal inatajwa kuwa huenda ikakosa saini ya kiungo mchezeshaji wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nabil Fekir ambaye ana umri wa miaka 25 kwa sababu ya kushindwa kumwondoa kwenye kikosi chake kiungo Mjerumani Mesut Ozil (30).

Mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Marc Overmars, ameitaka klabu hiyo kuhakikisha inamuuza Ozil na kufanya mchakato wa kumsajili Hakim Ziyech ili kukiimarisha kikosi hicho.

Overmars anaamini Ziyech ni bora zaidi na ataweza kuisaidia Arsenal kuliko kuendelea kubaki na Ozil ambaye ameshindwa kuwa kwenye kiwango bora wakati wote.

## KWA UFUPI

**PSG YAIKATALIA BARCA**
PARIS St-Germain imeitupilia mbali ofa ya Barcelona ambayo inamhusisha kiungo wa Croatia, Ivan Rakitic na kiungo mchezeshaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho na dau la pauni milioni 41 kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wake Mbrazil, Neymar (26). ***(L'Equipe, via Express)***

**MILAN, UNITED KUTETA**
INTER Milan wanatarajia kukutana na mabosi wa Manchester United kwa ajili ya kufanya tathmini ya usajili wa straika wa Ubelgiji, Romelu Lukaku (26), lakini ikisema kuwa watakuwa tayari kulipa pauni milioni 60 kwa mkataba wa miaka mitatu na kiasi kingine cha pauni milioni 15 kitajumuishwa kwenye motisha. ***(Sun)***

**CEBALLOS KUTUA ARSENAL**
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania na Real Madrid, Dani Ceballos, ambaye ana umri wa miaka 22, anakaribia kukamilisha mchakato wa kusajiliwa na Arsenal. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**ERIKSEN ATAJWA ATLETICO**
KIUNGO wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), ni mmoja kati ya wachezaji wanaotakiwa na Atletico Madrid ambayo inasaka kiungo mchezeshaji katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Evening Standard)***

**ROMA KUMTOA ZANIOLO**
ROMA imeweka wazi haina uwezo wa kutoa pauni milioni 25 ili kumsajili beki wa Tottenham, Toby Alderweireld lakini wako tayari kumtoa kiungo wao Mtaliano, Nicolo Zaniolo (20), kuwa sehemu ya kumsajili beki huyo wa kati Timu ya Taifa ya Ubelgiji, mwenye umri wa miaka 30. ***(Mirror)***

**ROSE AJIONDOA SPURS**
BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose (29), hatasafiri na kikosi cha Spurs kuelekea Singapore kwa ajili ya ziara ya maandalizi ya msimu mpya kwa sababu anatarajia kuuzwa. ***(Telegraph)***

**MANDZUKIC ANUKIA EVERTON**
EVERTON wameweka wazi nia yao ya kutaka kumsajili straika wa Juventus, Mario Mandzukic (33), huku ikisubiri kuona kama mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Croatia atakuwa kwenye sehemu ya mipango ya Kocha mpya wa mabingwa hao wa Serie A, ambao sasa wako chini ya Maurizio Sarri. ***(Telegraph)***

**MIGNOLET KUONDOKA LIVERPOOL**
WAKALA wa golikipa wa Liverpool, Simon Mignolet, amesema kuwa mlinda mlango huyo anataka kuondoka klabuni hapo na kwenda kutafuta timu ambayo atapata namba kwenye kikosi cha kwanza. ***(Les Sports Plus - in French)***

**BAILLY AKARIBIA MILAN**
AC Milan inatarajia kuacha mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Eric Bailly (25), baada ya kuachana na mpango wa kuwania nyota wa mlinzi wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren. ***(Tuttosport, via Mail)***

**UNITED YAMGANDA FERNANDES**
MANCHESTER United imewasilisha ofa kubwa ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

**CITY KUMWACHA MANGALA**
BEKI wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Eliaquim Mangala, anaweza kuondoka Manchester City akiwa mchezaji huru. Beki huyo mwenye umri wa miaka 28 alikuwa ndiye mlinzi ghali kwenye historia ya Uingereza baada ya mwaka 2014, kusajiliwa na City kwa dau la pauni milioni 42 akitokea Porto. ***(Mail)***

**FIRPO AKARIBIA BARCA**
BARCELONA imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa kushoto wa Real Betis na Timu ya Taifa ya Vijana ya Hispania ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Junior Firpo katika kipindi hiki cha majira ya joto ili kum-

## HABARI MICHEZO

# TAMBWE AFUNGUKA KLABU CECAFA ZINAVYOMGOMBEA

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Yanga, Amissi Tambwe, amesema kuwa ameshaanza mazungumzo na klabu mbalimbali za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ambazo zinahitaji huduma yake, imefahamika.

Tambwe ni mmoja wa wachezaji ambao hawakuwa kwenye mipango ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili, Tambwe, raia wa Burundi, alisema kuwa ameachwa na Yanga kwa sababu hakuwa "chaguo" la Zahera, lakini anaamini kiwango chake bado kiko juu na atapata klabu mpya ya kuichezea.

Tambwe alisema kuwa hatafanya uamuzi wa haraka wa kusaini mkataba mpya, mpaka pale atakapojiridhisha kuhusu historia ya timu atakayokubali kuichezea katika msimu mpya.

"Nilikuwa si sehemu ya mipango yake, niligundua hakuwa akinipenda, hakunihitaji na uamuzi huu kwangu ninaona kwamba amemfungulia njia mpya, tayari nimeanza kufanya mazungumzo na timu kubwa zikitaka kunichukua," alisema Tambwe.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba aliwataka wachezaji vijana kutokata tamaa kwa sababu kwenye mpira, makocha huwa na maamuzi yanayoumiza na kufurahisha.

"Zahera ameamua kuniacha kwa sababu zake binafsi, lakini naamini Mungu atanisaidia na milango imeshaanza kufunguliwa kwa sababu ninajiamini kuwa kiwango changu kipo juu, sitaweza kukosa timu ya kuichezea,"alisema Tambwe.

Hata hivyo, Tambwe alisema kwamba uamuzi wa kuwaacha wachezaji wengi ambao ambao waliitumikia timu hiyo msimu uliopita ambao ulikuwa na changamoto haukuwa sahihi kwa maendeleo ya klabu hiyo.

"Tulivumilia kipindi chote Yanga ilipokuwa na hali mbaya kifedha kwa sababu tulikuwa na mapenzi na timu yetu, mwisho wa siku tumekuja kuachwa bila kutarajia ,"alisema mmshambuliaji huyo wa zamani wa Simba.

Amewashukuru mashabiki na wanachama wa Yanga kwa kumpa ushirikiano katika muda wote alioitumikia klabu hiyo na kuwataka wale waliosikitika kutokana na kuachwa, wakubaliane na uamuzi huo ambao ni wa kawaida kwenye maisha ya soka.




Wasanii wa Kituo cha Baba Watoto wakitoa burudani kuelekea kampeni ya kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki iitwayo "Plastiki Noma", ambao watashiriki kufanya usafi kwenye daraja la Selander jijini Dar es Salaam leo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KMKM yawasajili Babi, Mngwali CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIUNGO wa zamani wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Abdi Kassim, ni mmoja kati ya wachezaji 30 ambao wataitumikia KMKM katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, imefahamika.

Tayari Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limeshatuma majina ya wachezaji hao ambao wataitumikia KMKM katika michuano hiyo inayotarajiwa kufanyika kuanzia mwezi ujao.

"Katoka orodha ya wachezaji 30 watakaoitumikia KMKM ni pamoja na mchezaji mkongwe na maarufu Zanzibar na Tanzania Bara, Abdi Kassim 'Babi'.

Wachezaji wengine waliomo kwenye orodha hiyo ni Mudathir Mohammed, Emil Mwafiyuma, Iliyasa Mohammed, Khamis Khamis, Richard Jaka, Hassan Abdallah, Ventiraus Kamanya, Alex Mwambisi, Salum Shukuru, Is-haka Mwinyi, Faki Sharif, Samir Said, Optitus Lupokenya, Mudrik Abdallah na Haji Mngwali.

Nyota wengine ni Adam Abdallah, Kheri Jecha, Nassor Nassor, Mussa Abdulrahman, Abdulnassir Mohammed, Hafidh Abdallah, Abdulrahman Ali, Ibrahim Khatib, Juma Mohammed, Fahad Seif, Salum Bajaka, Broun Costa na Vuai Jecha.

KMKM wataiwakilisha Zanzibar katika michuano hiyo baada ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu visiwani hapa msimu wa mwaka 2018/19.

## Wasanii Musoma kuchuana Nanenane

**Na Sabato Kasika**

VIKUNDI 14 vya ngoma za asili na kwaya kutoka katika Kata 14 za Musoma Vijijini, vinatarajia kuchuana katika sherehe za wakulima (Nanenane), zitakazofanyika mapema mwezi ujao kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Suguti mkoani Mara.

Waandaji wa sherehe hizo, wamesema kuwa kikundi kitakachoibuka mshindi, kitapata zawadi ya kikombe na fedha taslimu Sh. milioni 3.1. Msaidizi wa Mbunge wa Musoma Vijijini, Fedison Masawa, aliliambia gazeti hili kuwa, vikundi vilivyothibitisha kushiriki ni pamoja na Insuka kutoka katika Kata ya Nyakatende, Bugoji Ngoma, Suguti, Kiriba na Nyambono ambavyo vitachuana katika upande wa sanaa ya ngoma.

Masawa alivitaja baadhi ya vikundi vitakavyopambana kwa upande wa kwaya ni Jipe Moyo kutoka Kata ya Rusoli, Pambazuko (Makojo), Musanja Group ( Musanja), Ujamaa (Bugoji), Jitambue (Murangi), Mshikamano (Bukima), Mugango (Mugango) na Ifulifu iliyoko kwenye Kata ya Ifulifu. Alisema kuwa mshindi wa kwanza wa kwaya na ngoma atazadiwa Sh. milioni moja na kikombe, huku mshindi wa pili wa kwaya na ngoma akipewa Sh. 700,000 na kikombe wakati watakaoshika nafasi ya tatu watapata zawadi ya Sh. 400,000 pamoja na kikombe.

"Kazi na utamaduni wetu, maendeleo na utamaduni wetu, tunatarajia Agosti 8 mwaka huu kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Suguti, vitajaa watu kutoka maeneo mbalimbali ya jimbo letu kuja kushuhudia mashindano hayo," alisema Masawa.

## Mbeya City FC kuwavaa Wamalawi

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kujiimarisha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, timu ya Mbeya City ya jijini Mbeya inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Ard Marck Tiger ya Malawi.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inashiriki timu 20, inatarajia kuanza kufanyika ifikapo Agosti 23 mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, alisema kuwa maandalizi ya mchezo huyo yameshakamilika baada ya wageni wao kukubali kuthibitisha kushiriki mechi hiyo.

Mwambusi alisema kuwa wamejipanga kufanya mazoezi ya kiwango cha kimataifa kwa sababu wanafahamu ushindani utaongezeka zaidi katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.

"Mazungumzo na timu hiyo yanaendelea vizuri, tunatarajia kila kitu kitakwenda sawa, pia tumeshaanza kuzungumza na timu nyingine iitwayo Lilongwe FC, ili tucheze nao pia," alimaliza Mwambusi ambaye amerejea Mbeya City akitokea Azam FC.

Michezo
Alhamisi Julai 18, 2019
Nipashe



## Arsenal kusajili 'majembe' manne

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Simba, Ibrahim Ajibu (kushoto), akifuata maelekezo kutoka kwa kocha wa viungo wa timu hiyo, Adel Zrane, katika mazoezi ya mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara yanayoendelea mjini Rustenburg, Afrika Kusini. **PICHA: SIMBA SC**

# JESHI LA YANGA LIMEKAMILIKA

## ●●●Ushindani wa namba wazidi kuongezeka huku wakimsubiri Zahera...

**Na Faustine Feliciane**

JESHI limekamilika! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya wachezaji wote wa Yanga kuwasili kambini mkoani Morogoro kwa ajili ya kushiriki maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hatua hiyo inakuja baada ya wachezaji wa kimataifa waliosajiliwa na Yanga kupata vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini.

Kikosi hicho ambacho kinanolewa na Kocha Msaidizi, Noel Mwandila, sasa kinamsubiri Kocha Mkuu Mkongomani Mwinyi Zahera, ambaye bado hajarejea kutoka likizo baada ya Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kutolewa kwenye mechi za fainali za Kombe la Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa kikosi cha Yanga sasa kipo kamili na kila mchezaji anashiriki vema programu za mazoezi zilizoandaliwa na benchi la ufundi la timu hiyo.

Saleh alisema kuwa wanafurahi kuona kila mchezaji anaonyesha bidii kwenye mazoezi, na hii inadhihirisha kwamba hakuna nyota atakayekuwa na namba ya kudumu kwenye kikosi hicho.

"Taarifa ambazo tunazo hapa kambini ni kuwa kocha mkuu atawasili nchini wakati wowote wikiendi hii, kwa sasa wachezaji wote tuliowasajili wamefika na wanaendelea na programu za mazoezi ambazo zinasimamiwa na Kocha Mwandila, ambaye anafuata maelekezo ya Zahera," alisema.

Mratibu huyo alisema kuwa ari ya mazoezi katika kikosi hicho ni kubwa na wachezaji wanadai kwamba muda wa kuanza ligi unachelewa.

"Kila kinachofanyika kocha Zahera anafahamu kwa sababu ni programu ya maandalizi ya msimu mpya, alishiriki kuiandaa, mambo mengine atakuja kuyaongeza yeye (Zahera) kama mkuu wa benchi la ufundi atakapofika," alisema Saleh.

Kiongozi huyo alisema kuwa wachezaji wote wa kigeni waliosajiliwa wapo tayari kuanza kutokana na kukamilisha taratibu za kupata vibali.

Aliwataja wachezaji hao wa kimataifa waliosajiliwa ni pamoja na Patrick Sibomana, Juma Balinya, Maybin Kalengo, Farouk Shikalo, Issa Bigirimana, Lamine Moro, Sadney Urikhob na Mustapha Selemani.

Kabla ya kuwakaribisha AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika mechi ya kirafiki kwenye tamasha la Siku ya Mwananchi litakalofanyika Agosti 4 mwaka huu, mabingwa hao wa kihistoria wataivaa Dodoma FC kwenye mchezo mwingine wa kirafiki

## Mastaa Simba wafanya kweli

**Na Faustine Feliciane**

IKIWA ni siku ya tatu tangu kuanza kambi ya maandalizi ya msimu mpya huko Afrika Kusini, benchi la ufundi la Simba limeongeza kasi ya mazoezi huku Kocha Mkuu, Patrick Aussems akifurahishwa na jitihada za wachezaji wake wageni.

Aussems aliiambia Nipashe jana kuwa anafurahi kuona kila mchezaji anajituma na kufuata kikamilifu maelekezo yote anayoyatoa.

Mbelgiji huyo alisema kuwa anaamini atakuwa na kikosi chenye ubora zaidi katika msimu ujao baada ya wachezaji wapya kuufahamu vema mfumo unaotumika katika timu hiyo inayoshikiliwa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mwaka wa pili mfululizo.

"Bado tuna siku chache huku tangu timu imefika hapa, lakini naona juhudi za wachezaji wangu kwenye mazoezi ninayotoa, hii ni dalili nzuri kwetu," alisema Aussems.

**Alisema kuwa amelazimika kuandaa programu maalumu kwa ajili ya kuhakikisha wachezaji wake wote wanafahamu vitu vya msingi, kabla ya baadhi ya nyota wake kurejea nchini ili kujiunga na kambi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo itajiandaa kuwavaa Kenya katika mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani (CHAN).**

Simba inatarajia kuweka kambi ya wiki mbili huko Afrika Kusini na mara baada ya kurejea itashiriki kwenye Tamasha la Simba Day ambalo kilele chake kitakuwa ni Agosti 8 mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >